# Nipashe

Ijumaa Septemba 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580028

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Kunradhi Mamlaka Uendeshaji KIA kuhusu mashine ya ukaguzi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mjadala mzito kura polisi kabla uchaguzi

**CCM**, wapinzani watoa maoni kinzani, ZEC yawatoa hofu wananchi... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 5**

**AVEVA, KABURU WAPANGUA MAKOSA 2, WAPATA DHAMANA**

HATIMAYE vigogo wawili kati ya watatu wa Klabu ya Simba, akiwamo Rais Evance Aveva na makamu wake, Godfrey Nyange maarufu kama Kaburu...

**UKURASA WA 8**

**UMATI WAMUAGA MHARIRI DILUNGA**

MWILI wa aliyekuwa Mhariri wa gazeti la Jamhuri, Godfrey Dilunga, umeagwa na umati wakiwamo viongozi wa serikali na vyama...


## Milioni 5 wasajili simu alama za vidole

UKURASA 2




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akiongoza kuagwa mwili wa mwandishi wa habari Godfrey Dilunga katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waingia matatani deni feki la bil. 70/-

UKURASA 22


TAIFA STARS VS SUDAN

SEPTEMBA 22, 2019 • UWANJA WA TAIFA




HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

245423702

# Tigo yaahidi makubwa IPP

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, imeahidi kuongeza ushirikiano wa kibiashara na vyombo vya habari vya IPP na kukuza ukaribu uliopo sasa.

Ofisa Biashara Mkuu wa Tigo, Tarik Boudiaf, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP.

"Tuna imani katika ushirikiano na tunahitaji ushirikiano. IPP ni moja ya washirika wetu katika biashara. Tunaahidi kuendeleza ushirikiano, nasi tunahitaji ushirikiano wenu na tunaomba tuendeleze ushirikiano," alisema Boudiaf.

Akiwa katika ziara hiyo, Boudiaf aliahidi kampuni yake kutoa ushirikano wa baadhi ya huduma kama vile vifurushi vya kuperuzi vitakavyowasaidia waendesha vipindi na watangazaji kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

"Nimefurahi kutembelea vyombo vya habari vya IPP. Sikutarajia kuona IPP ni kubwa sana. Katika ziara yangu hii nimeongeza maarifa katika masuala ya habari," alisema Boudiaf.

Kwenye ziara hiyo, Boudiaf ambaye aliambatana na Ofisa Mawasiliano wa Tigo, Umi Mtiro, walitembelea The Guardian Ltd na kuona namna uzalishaji na uandaaji wa habari unavyofanyika.

Pia walitembelea vituo vya runinga na redio vya EATV, East Africa Radio, Radio One, Capital Televisheni ITV.

# Mjadala kura polisi kabla uchaguzi

**Na Romana Mallya**

SUALA la vikosi vya ulinzi na usalama kupiga kura siku moja kabla ya uchaguzi, limepokewa kwa mitazamo tofauti huku baadhi ya vyama vya siasa vikionyesha hofu.

Wakati mjadala ukiibuka juu ya sakata hilo, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imetoa ufafanuzi juu ya suala hilo ambalo limesababisha mjadala mzito miongoni mwa wadau.

Huku hali ikiwa hivyo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeweka bayana kwamba hakuna ubaya wakati Chama cha Demokrasia na Maendeleo kikisema huenda ni njama za kuwakandamiza wapinzani.

CCM kupitia Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) anayeshughulikia Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, imeunga mkono suala hilo na kusisitiza kuwa jambo hilo ni zuri kutokana na dhamana watakayokuwa nayo askari hao siku ya uchaguzi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika warsha ya viongozi wa ngazi za juu wa vyama vya siasa waliokutana kujadili na kuridhia mapendekezo ya taratibu za uteuzi iliyoandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Kanali mstaafu Lubinga alisema haoni kama kuna tatizo la makundi hayo kupewa nafasi hiyo.

"Kwa nini hawakuwaambia wanajeshi? Kwa nini hawakuwaambia uhamiaji? Hii ni kwa sababu polisi watatawanywa kusimamia kwenye vituo ambavyo si vyao ndiyo maana wamefanya hivyo," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa Chadema na Mbunge wa Viti Maalum, Suzan Lyimo, alipopata nafasi ya kuzungumza kwenye warsha hiyo, alionyesha wasiwasi wa kura zitakazopigwa kuwa nani atakayezihesabu.

"Jambo lingine ni kwamba ile siku ya kupiga kura watakuwa huru, hivyo kwa namna yoyote ile watakuja kutudhibiti. Hili ni tatizo na linatupa hofu wanawake hata wanaume. Haya ndiyo mambo ambayo tunapaswa kuyaangalia kwa kina wanatoa wapi suala hilo, kwamba askari wapige kwanza kura siku moja kabla."

"Ninaamini semina hii itachukulia suala hili kama ni lenye nguvu ya kuona ni namna gani tunaweza kuliangalia ili nchi yetu iwe na amani tunapoelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu," alisema.

**WADAU WALONGA**

Wakitoa maoni yao kuhusu kura ya mapema, baadhi ya wasiasa na wanaharakati walisema nchi nyingi duniani zimekuwa na kura inayofanana na hiyo, hivyo iwapo sheria hiyo itatekelezwa vizuri hakutakuwa na tatizo.

Naibu Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mipango na Uendeshaji wa ADC, Juma Ali, alisema sheria hiyo si mbaya iwapo itasimamiwa vizuri na itawawezesha askari wanaosimamia uchaguzi kufanya kazi zao kwa ufanisi.

"Zanzibar tuna sheria nyingi na nzuri lakini tatizo linakuja katika utekelezaji wake. Nina imani kuwa sheria hii mpya ya uchaguzi

INAENDELEA UK.8



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Edward Mpogolo (kulia), akijumuika kupata kahawa na wananchi wa Kata ya Irisya ikiwa ni njia ya kujua changamoto zao baada ya kufanya mkutano wa hadhara katika kata hiyo, jana mkoani Singida. **PICHA NA DOTTO MWAIBALE**

# Mil. 5.2 pekee wamesajili laini kwa alama za vidole

**Na Mary Geofrey**

IKIWA imesalia miezi mitatu kabla ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuzifungia laini za simu ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole, watu milioni 5.2 pekee kati ya milioni 44 wanaomiliki simu ndio waliojisajili.

Kutokana na changamoto hiyo, kampuni za mitandao ya simu nchini kwa kushirikiana na TCRA, wamezindua kampeni ya pamoja kwa ajili ya kuhamasisha wateja wao kujisajili kwa alama za vidole kabla ya siku ya mwisho.

Takwimu hizo zilitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TCRA, Frederick Ntobi, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa pamoja wa wadau wa mawasiliano wenye lengo la kuhamasisha Watanzania kupata huduma hiyo.

Alisema tarehe ya mwisho iliyotolewa na serikali ni Desemba 31, mwaka huu, lakini hadi Agosti, mwaka huu idadi ya watu waliojisajili kwa kutumia kitambulisho cha taifa ni watu milioni 5.2.

"Kwa sasa usajili huu unaendelea katika maduka yote ya watoa huduma za mawasiliano na mawakala wenye vitambulisho maalum na unatarajia kukamilika Desemba 31, mwaka huu.

"Hadi mwishoni mwa mwezi Agosti mwaka huu, idadi ya laini zote za simu zilizosajiliwa kwa alama za vidole ilifika 5,222,721 ambayo ni sawa na asilimia 12 ya laini zote za simu zilizotumika Sh. 44,258,637," Ntobi alisema.

Alisema juhudi zinazofanywa na TCRA ni kuendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha kuwa watumiaji wote wa mawasiliano wanasajili laini za simu kwa mujibu wa sheria.

"Baada ya tarehe 31 Desemba mwaka huu, lakini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa upya kwa alama za vidole hazitaruhusiwa kutumika kwenye mitandao ya simu," Ntobi alisisitiza.

Kwa upande wa watoa huduma za simu, walisema changamoto ya watu kutojisajili inatoka na mfumo wa utoaji vitambulisho wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), kufanya kazi taratibu.

Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya Zantel, Rukia Mtingwa, alisema watu wengi hawajajiandikisha kupata vitambulisho vya taifa ndio sababu wanashindwa kusajili laini zao. "Tunaomba muhamasishe watu kujiandikisha kupata vitambulisho vya taifa ili waweze kusajili laini zao kabla ya Desemba 31 haijafika," Mtingwa alisema.

Naye Mwenyekiti wa watoa huduma za mawasiliano ya simu, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Vodacom, Alex Bitekeye, alisema wameamua kushirikiana kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

"Sisi watoa huduma ni jukumu letu kuhakikisha kwamba laini zote za simu zinasajiliwa upya kabla ya terehe ya mwisho na hii itasaidia wateja wetu kuendelea kuwa na mawasiliano, kupunguza usumbufu usiyo wa lazima hapo baadaye," Bitekeye.

Naye Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, alishauri watumiaji wote wa simu kujitokeza kujiandikisha na kupiga namba *150*00# chagua namba 3, chagua namba 2, kuingiza majina matatu na nambari ya simu kama yalivyosajiliwa Nida kwa ajili ya kupata namba ya kitambulisho itakayowezesha kujisajili.

Aprili 26, mwaka huu, Rais John Magufuli, alipendekeza muda wa kusajili laini kwa alama za vidole usogezwe mbele kutoka Agosti hadi Desemba 31, ili kutoa fursa kwa Watanzania wengi kuendelea kujisajili.

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kulia) na Mkurugenzi wa Benki ya Kilimo, Japhet Justine kwenye mkutano wa kutangaza ushirikiano kati ya benki hiyo na Benki ya Kilimo (TADB) kwa lengo la kutoa mikopo kwa wakulima wa korosho, jijini Dar es Salaam jana.
**MPIGAPICHA WETU**

# Kunradhi KIA mashine ukaguzi mizigo

KATIKA toleo letu la jana, Nipashe tulichapisha habari yenye kichwa kilichosomeka 'Mashine ukaguzi KIA haifanyi kazi miaka 3'.

Habari hiyo ilieleza changamoto ya kutofanya kazi kwa kifaa maalum cha ukaguzi wa mizigo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa miaka mitatu.

Msingi wa habari hiyo ulitokana na kikao cha wadau wa utalii wanaotumia uwanja huo, uongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (Tato), Emmanuel Mollel, aliibua changamoto ya abiria kuibiwa mizigo, akieleza kuwa inachagizwa na kuharibika kwa kiambaza (screen) cha kifaa maalum hicho cha ukaguzi wa mizigo kwa miaka mitatu.

Licha ya mwandishi wetu kushiriki katika kikao hicho, Nipashe tumebaini kuwapo kwa upungufu wa kitaaluma katika habari hiyo.

Baada ya habari hiyo kulalamikiwa na mamlaka za serikali, Nipashe jana ilituma mwandishi mwingine kwenda kwenye uwanja huo kujiridhisha kuhusu changamoto hiyo na alikuta vifaa vya ukaguzi, kikiwamo kifaa maalum cha ukaguzi wa mizigo katika uwanja huo, vinafanya kazi. Nipashe tunaiomba radhi mamlaka ya uendeshaji wa uwanja huo na wasomaji wetu kwa usumbufu uliojitokeza kutokana na habari hiyo.

**MHARIRI**

# Kortini kwa kujifanya ofisa TRA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKAZI wa Dar es Salaam, Kitareti Muhuti, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma kwa tuhuma za kujifanya Ofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kujipatia fedha.

Mtuhumiwa huyo alifikishwa jana mahakamani hapo na kusomewa shtaka na Wakili wa Serikali Miyango Kezilahabi, akishirikiana na Wakili wa TRA, Hadija Senzia, mbele ya Hakimu Mkazi Rachel Magoti.

Akisoma maelezo ya kesi hiyo namba 170/2019 mahakamani hapo, Wakili Kezilahabi alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kwa nyakati tofauti kwa kujifanya ofisa wa TRA na kujipatia fedha.

Kezilahabi alidai kuwa mtuhumiwa huyo ametenda kosa hilo kinyume cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu namba 100(b) na 35.

Kutokana na madai hayo, alimwomba hakimu kupanga tarehe kwa ajili ya kutajwa kutokana na upelekezi kutokamilika.

Hakimu Magoti alikubali ombo hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 3, mwaka huu na kuruhusu dhamana kwa mtuhumiwa huyo.

Hata hivyo, mshtakiwa alimwomba hakimu huyo kumpunguzia masharti ya dhamana kutokana na kwamba yeye si mkazi wa Dodoma.

Hakimu Magoti alikataa ombi hilo na kudai kuwa masharti ya dhamana ni yale yale yaliyowekwa na mahakama, hivyo anatakiwa kuwa na wadhamini wawili ambao ni wakazi wa Dodoma.

# Serikali kuongeza ndege 2 aina ya Airbus

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesaini mkataba wa ununuzi wa ndege nyingine mbili mpya aina ya Airbus zitakazokuwa na muundo wa A220-300 zilizoboreshwa.

Makubaliano hayo yalifanyika kati ya Serikali na Mwakilishi wa Kampuni ya Airbus ya nchini Canada kwa lengo la kuongeza ndege hizo.

Tayari serikali imeshanunua ndege sita ambazo zinafanya kazi, mbili aina ya Dreamliner na Bombardier zinazotarajiwa kuingia nchini mwezi Oktoba au Novemba, mwaka huu.

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Ndege (ATCL), Ladislaus Matindi, akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, alisema makubaliano hayo yamewekewa uzito wa kisheria na kutoa haki kwa serikali kuanza kufuatilia ndege hizo.

Alisema ndege hizo zitakuwa na mwonekano wa tofauti kwa kuwekewa runinga kwa ajili ya kuongeza mvuto wa kibiashara na kuwapa wateja burudani.

"Makubaliano haya yanatupa uzito wa kisheria wa kuanza kufuatilia na wao kuanza kutengeneza ndege hizi ambazo tumezifanyia maboresho kwa kuweka runinga tofauti na za awali lengo ni kuwapa burudani wateja wetu," Matindi alisema.

Alisema serikali inaendelea kufuatilia hali ya usalama katika nchi ya Afrika Kusini kabla ya kuanza kuruhusu safari za ndege zilizositishwa kutokana na kuwapo kwa machafuko.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ndege za Serikali, Dk. Benjamin Ndimila, aliyesaini mkataba huo kwa niaba ya serikali, alisema serikali inajenga historia kupitia utendaji kazi wa Rais John Magufuli ambaye ni dira kuu ya kutekeleza hayo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Mauzo wa Kampuni ya Aibus ukanda wa Afrika na Asia, Hadi Akoum, alisema baada ya kuingia makubaliano hayo, wanatarajia kukamilisha ujenzi wa ndege hizo ndani ya mwaka mmoja hadi mmoja na nusu.

Alisema kuwapo kwa ndege hizo nchini kunaendelea kuleta manufaa makubwa ya kiuchumi kupitia sekta ya utalii na biashara.

Aliipongeza serikali kwa kukamilisha jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere na kusema kuwa ni kivutio kinachochea uchumi wa taifa.

**SIFA YA AIRBUS**

Ndege hiyo, ambayo inaundwa na kampuni ya utengenezaji wa ndege ya Airbus, itakuwa ya muundo wa A220-300.

Airbus A220 zilikuwa zinafahamika kama Bombardier CS100s kabla ya Airbus kununua mradi huo wa utengenezaji wa ndege za C Series.

Ina urefu wa mita 38.7, na kwa jumla inaweza kuketi abiria 141, urefu kutoka chini kwenda juu ni mita 11.5, na upana wa mabawa ni mita 35.1.

Airbus 220-300 inaweza kusafiri umbali wa 5,920 km safari moja, na inaweza kupaa ikiwa na uzani wa tani 67.6, na kutua ikiwa na uzani wa tani 58.7.

Ndiyo ndege kubwa miongoni mwa familia ya A220 na iliundwa kulenga soko la safari za ndege zinazobeba abiria kati ya 130-160.


Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

NAFASI ZA KAZI

MWANDISHI WA HABARI WA KUJITEGEMEA

Gazeti la Nipashe linatangaza nafasi kwa Mwandishi wa habari wa kujitegemea kutoka mikoa yote nchini.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe amefanyakazi angalau miaka mitatu (3) kwenye chombo cha habari
2. Ajue misingi, miiko na maadili ya uandishi wa habari
3. Awe mwenye kujituma na mbunifu katika kutafuta habari

Mwombaji awasilishe maombi yake kupitia barua pepe **nipashe.gazeti@gmail.com**

*Mwisho wa kutuma maombi ni Septemba 30*

615421902

# Wajanja wategesha mali uthamini Nyamongo

**Na Munir Shemweta,** NYAMONGO

KAZI ya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wa Nyamongo, Tarime Mkoa wa Mara kupisha upanuzi wa mgodi wa dhahabu North Mara kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la maji taka, imekumbwa na changamoto.

Hali hiyo imetokana na baadhi ya wananchi kujenga nyumba au kuongeza sehemu za nyumba zao maarufu kama 'tegesha' ili kujipatia faida kupitia thamani ya fidia.

Wathamini katika kazi hiyo, walibaini tofauti kubwa katika uthamini walioufanya awali na walipokwenda kwa mara ya pili kwa ajili ya uhakiki.

Katika awamu ya pili, wathamini hao walibaini baadhi ya vyumba katika nyumba zilizofanyiwa uthamini kuwa wazi baada ya waliokuwa wakishi kuondoka baada ya kuthaminiwa.

Imeelezwa kuwa lengo la wananchi wanaofanya ujanja wa 'tegesha' ni kujipatia posho ya makazi ambayo kwa kawaida hutolewa kama fidia kwa wamiliki kulingana na idadi ya vyumba kwenye nyumba husika.

Kwa mujibu wa wathamini hao, mbali na wamiliki walioathirika kulipwa gharama nyingine kama vile nyumba na mazao, pia hulipwa posho ya makazi kwa kipindi cha miezi 36 lengo likiwa kumwezesha mpangaji kupata mahali pa kuishi kabla ya kuondolewa.

Mwandishi wa habari hii alishuhudi moja ya nyumba katika kitongoji cha Kigonga A katika kijiji cha Matongo ikiwa na vyumba 21 wakati ilistahili kuwa na vyumba vitatu, huku baadhi ya vyumba vikiwa havina hata

INAENDELEA UK. 8



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (kushoto), akimwapisha Ayoub Mohamed Mahmoud kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ikulu Mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**




# PM aagiza majeshi EAPCCO kuimarisha ulinzi mipakani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kasim Majaliwa, ameliagiza Shirikisho la Wakuu wa Majeshi ya Polisi kutoka nchi 14 za Mashariki mwa Afrika (EAPCCO), kuimarisha ulinzi kwenye mipaka ili kudhibiti wahalifu wanaokwepa ukaguzi. Aliwaagiza wakuu hao kuongeza juhudi kwa kuwajengea uwezo watendaji wao kitaaluma na hoja kwenye serikali zao ili kupata vifaa na vitendea kazi vya kudhibiti vitendo vya uhalifu vinavyokwenda sambamba na ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) duniani.

Alitoa maagizo hayo jana jijini Arusha wakati akifungua mkutano wa 21 wa EAPCCO kutoka nchi hizo kwa niaba ya Rais John Magufuli.

"Wahalifu wengi wamekuwa wakikwepa ukaguzi kwenye mipaka rasmi niwahimize mwendelee kidhibiti mipaka ya nchi zetu kwa kufanya operesheni za pamoja mara kwa mara, kubadilishana taarifa za uhalifu na wahalifu, kufanya mafunzo ya pamoja na kubadilishana uzoefu wa kiutendaji kwa kufanya upelelezi kwa pamoja," alisema.

Aliagiza nchi hizo kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji bila kujali mipaka ya nchi wanachama kwa kuwa wahalifu wanatumia udhaifu wa kukosekana kwa ushirikiano madhubuti wa nchi hizo.

"Kuondolewa kwa vikwazo vingi visivyo vya kiforodha, kumesababisha athari za kiusalama na wahalifu wanatumia fursa hiyo kuimarisha magenge yao ya uhalifu unaovuka mipaka, ikiwamo dawa za kulevya, ugaidi, utengenezaji na utoaji wa bidhaa bandia, uharamia katika maziwa na bahari, wizi wa magari, ujangili, utoroshaji wa madini na biashara haramu ya binadamu yanayoambatana na utakasaji wa fedha zinazotokana na uhalifu huo," alisema.

Majaliwa alisema vitendo vya uhalifu visipodhibitiwa ipasavyo vinaleta athari kwa maendeleo na ustawi wa nchi wanachama, hivyo ni vyema wakaweka mikakati thabiti ya kukabiliana na magenge yote ya uhalifu unaovuka mipaka ili wasipate mahali salama pa kufanyia uhalifu huo.

Kuhusu teknolojia alisema moja ya changamoto kubwa zinazoukabili ukanda wa nchi hizo, ni kukua kwa teknolojia ya Tehama na mapinduzi hayo yanaleta mbinu na aina mpya ya uhalifu, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa wataalamu waliobobea katika teknolojia hiyo. Alitaja changamoto nyingine kuwa ni pamoja na utashi wa kisiasa na ili kuondokana na changamoto hiyo utashi wa kisiasa unahitajika ili kuvipa nguvu vyombo vya dola katika kusimamia sheria. "Niwatake wanasiasa wengine tutoe ushirikiano kwa vyombo hivi ili viwe na meno kwa kutunga sheria zitakazowawezesha kufanya kazi zao ipasavyo," alisisitiza Majaliwa. Changamoto nyingine alisema utofauti wa sheria baina ya nchi wanachama unatoa mwanya kwa wahalifu kufanya uhalifu kwenye nchi moja na kukimbilia nchi nyingine ambayo haiwabani.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni udhaifu wa utunzaji kumbukumbu za wahalifu katika kanzi data za Interpol pamoja na vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watendaji hali inayosababisha ugumu wa upelelezi na ukamataji wahalifu.

Pia alimpongeza Mwenyekiti mpya wa EAPCCO ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro na kumwagiza kusimamia utekelezaji wa mipango na mikakati ya maadhimio ya mkutano huo wa 21.

Awali IGP Sirro akimkaribisha Waziri Majaliwa, alisema mkutano huo ulitanguliwa na kamati ya utendaji mbalimbali ambazo maazimio na mapendekezo yao yatapitishwa leo na Mawaziri wa Mambo ya Ndani toka nchi hizo wanachama. "Nawashukuru wakuu wenzangu wa nchi wanachama kwa kuniamini na kunipa uenyekiti kwa kipindi cha mwaka mmoja na nitasimamia amani na usalama katika nchi zetu," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Interpol, Jurgen Stock, alisema ofisi yake itaendelea kufadhili mafunzo mbalimbali kwenye shirikisho hilo ili ziweze kudhibiti vitendo vyote vya uhalifu. Mwenyekiti wa EAPCCO aliyemaliza muda wake, Luteni Generali Adil Mohammed, alishukuru wakuu wenzake wa polisi kwa ushirikiano waliompa katika kipindi chake cha uongozi na kuomba wautoe kwa mwenzake.

# Aveva, Kaburu wapangua makosa 2, wapata dhamana

**Na Hellen Mwango**

HATIMAYE vigogo wawili kati ya watatu wa Klabu ya Simba, akiwamo Rais Evance Aveva na makamu wake, Godfrey Nyange maarufu kama Kaburu, wameondolewa mashtaka mawili ya utakatishaji Dola za Marekani 300,000 baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha na mahakama kuwaona hawana kesi ya kujibu dhidi ya mashtaka hayo.

Hata hivyo, washtakiwa hao pamoja na mwenzao Zacharia Hansppope wamekutwa na kesi ya kujibu katika mashtaka saba ikiwamo kughushi, kula njama, matumizi mabaya ya madaraka, kutoa nyaraka za uongo, na kutoa maelezo ya uongo.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Alisema bila kuacha shaka mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa Jamhuri imewaona washtakiwa hao hawana kesi ya kujibu katika makosa ya kutakatisha fedha.

"Ushahidi wa Jamhuri umeshindwa kuleta mashahidi wa kuelezea namna washtakiwa walivyotakatisha fedha hizo, mahakama yangu inawaona hamna kesi ya kujibu dhidi ya mashtaka hayo," alisema na kuongeza.

"Washtakiwa mahakama yangu imewaona mna kesi ya kujibu katika makosa ya kughushi, matumizi mabaya ya madaraka na kuwasilisha nyaraka za uongo."

Baada ya kuondolewa mashtaka ya kutakatisha fedha mahakama hiyo imewapa washtakiwa masharti ya dhamana kwa sababu mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo yaliwanyima dhamana yameondolewa.

Alisema baada ya kuchambua ushahidi wa mashahidi 10 wa upande wa Jamhuri ukiacha shtaka la tano na sita mahakama imeona kuwa washtakiwa wana kesi ya kujibu katika shtaka la 1,2,3,4,7,8 na 9 isipokuwa katika shtaka la tano na sita na shtaka la utakatishaji linaondolewa.

Wakili wa Utetezi, Nehemia Nkoko, aliiomba mahakama kuwapatia wateja wake dhamana kwani mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo yaliyokuwa yanawanyima dhamana washtakiwa hayapo.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leornad Swai, alidai upande wa Jamhuri hauna pingamizi la dhamana dhidi ya washtakiwa.

Hakimu alisema washtakiwa hao watakuwa nje kwa dhamana kwa kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 30 kwa kila mmoja pamoja na vitambulisho.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi kesho Septemba 20, 2019 kwa ajili ya washtakiwa kuanza kujitetea.

# Wenye benki wafichua vikwazo utoaji huduma

**Na Salome Kitomari**

UMOJA wa wenye benki nchini, umesema kuwa sheria zisizo rafiki, matumizi mabaya ya zuio la mahakama na ukosefu wa vitambulisho vya Taifa ni kikwazo kikubwa katika utoaji wa huduma za kibenki na kufikia wananchi wengi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Benki Tanzania, Abdulmajid Nsekela, aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wanachama na wadau mbalimbali kupitisha kamuni na kupanga mkakati wa kuongeza huduma jumuishi, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema pamoja na ushirikiano mzuri wa serikali lakini zipo baadhi ya sheria siyo rafiki ikiwamo sheria ya ardhi ya kutumia ardhi kama dhamana ya mkopo na kwamba kwa mabadiliko ya sasa yanazuia matumizi ya ardhi isiyoendelezwa kutumika kama dhamana.

"Ni vyema ingefanyiwa marekebisho alafu iruhusu wateja kutumia ardhi kupata mikopo kuliko kuzuia," alisema.

Nsekela alisema changamoto nyingine ni wateja wenye madeni kukimbilia mahakamani kuweka zuio ili wasaidiwe na kesi kuchukua muda mrefu na kila muda wa zuio unavyoisha wanaongeza jingine.

Aidha, alisema changamoto nyingine ni ukosefu wa vitambulisho vya taifa kwa wateja wengi kiasi cha kushindwa kuwatambua na kuwapa huduma za kibenki kwa wakati.

"Kutokana na mahitaji makubwa ya vitambulisho vya taifa imeshindwa kutoa vitambulisho hivyo, ushauri wetu wizara itumie ushawishi wake ili watu wapate namba ya utambulisho na kitambulisho," alisema.

Aidha, aliiomba Nida kuangalia uwezekano wa kutoa vitambulisho kama inavyofanyika kwenye nchi nyingine, itumie hatua mbadala na kufikia wananchi wengi kwa muda mfupi na kwa wakati. Sisi kama taasisi ya fedha tuko tayari kushirikiana na Nida kuhamasisha wananchi kuchukua namba za vitambulisho," alisema.

Akifungua mkutano huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliiagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kufuatilia kwa karibu taasisi za fedha zinazoshindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Aidha, alisema sekta ya benki inapaswa kupanuka na kwamba takwimu hizi zinaonyesha pia kuwa bado kuna asilimia 28 ya Watanzania ambao hawajafikiwa kabisa na huduma za kifedha kati yake asilimia 65 ya wananchi wanaofikiwa na huduma rasmi za kifedha, ni asilimia 16.7 tu wanaonufaika na huduma za kibenki.

Dk. Mpango alisema umuhimu wa matawi ya benki vijijini ni mkubwa licha ya uwepo wa teknolojia iliyosaidia kupanua huduma shirikishi za kifedha, lakini upanuaji huduma kwa nia ya matawi au mawakala bado una umuhimu mkubwa kwa maeneo ya vijijini.

"Na hii ni kwa sababu kwa mazingira tuliyo nayo kwa nchi yetu, kuna changamoto kwa wananchi wengi kuweza kutumia teknolojia za kidijitali. Pia tukumbuke siyo huduma zote za kibenki zinaweza kutolewa kidigitali," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa takwimu zinaonyesha kwamba karibu asilimia 33 ya matawi ya benki yako mkoa mmoja tu wa Dar es Salaam. Huku wakiwaacha kando wananchi wengi ambao wanaishi katika maeneo ambayo hawajawahi kupata bahati ya kuona hata tawi moja la benki.

Naye Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alisema benki hiyo kama msimamizi wa sekta ya fedha ina shauku kubwa ya kuona maendeleo na mchango zaidi wa sekta hiyo katika ukuaji wa pato la taifa.

"Napenda kukuahidi kuwa Benki Kuu itaendelea kuvisimamia vyombo vya fedha, ili kuhakikisha kuwa huduma kwa wateja zinazingatia tija, weledi na maadili bora," alisema.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (kushoto) na Mwenyekiti wa Chama cha Benki nchini, Abdulmajid Nsekela, akikata utepe kuzindua kanuni mpya kwa benki jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (kulia) na Gavana wa Benki Kuu, Prof. Florence Luoga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe ahoji uchaguzi wa mitaa

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chadema, Freeman Mbowe, amehoji uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu, huku akiuliza Chama Cha Mapinduzi kinakwenda kushindana na nani.

Akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, Mbowe alisema kwa miaka minne vyama vya upinzani vimefungiwa kufanya kazi za siasa za aina yoyote, huku upande mwingine ukiendelea kama kawaida.

"Kwa miaka minne vyama havijafanya kazi ya kisiasa na ghafla wanatangaza uchaguzi halafu unapewa siku saba za kufanya kampeni. Vyama hivyo vimekwenda kwa wananchi lini kujinadi na kujulikana kwa mambo yao?" Alihoji na kuongeza:

"Sasa kwa mazingira haya CCM inakwenda kushindana na nani kwenye kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa, wakati wanajua wazi wanayeshindana naye hakuwa na nafasi na muda wa kujijenga kama ilivyokuwa kwake?"

Kwa mujibu wa Mbowe, baadhi ya Watanzania hawaoni na wanaliona jambo hilo kuwa ni tatizo la Chadema pekee na si kwa mustakabali wa demokrasia na maisha yao kwa ujumla.

Wiki iliyopita, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilitangaza kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa utafanyika Novemba 24, mwaka huu, na jumla ya vitambulisho vinane vitaruhusiwa kutumiwa na wapigakura kutambulika kwenye kituo cha kupigia kura.

Kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na Tamisemi, kampeni zitaanza Novemba 17 hadi 23, vyama vya siasa vyenye wagombea vinaweza kuwateua wanachama wake kuendesha kampeni kwa niaba ya wagombea wa vyama vyao.

Mwongozo huo ulieleza kuwa kampeni za uchaguzi zitaanza saa mbili asubuhi na zitamalizika saa 12 jioni ya kila siku ya kampeni.

Pia ulieleza kuwa fomu za kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi huo zitatolewa kuanzia Oktoba 29 hadi Novemba 4, 2019 kuanzia saa 1: 30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

Aidha, vitambulisho vitakavyotumika ni cha mpigakura, cha kazi, hati ya kusafiria, kadi ya bima ya afya, cha shule au chuo, mifuko ya hifadhi ya jamii, leseni ya udereva na cha taifa.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, mpigakura katika uchaguzi huo ni lazima awe raia wa Tanzania, umri wa miaka 18 au zaidi, mkazi wa kijiji au kitongoji au mtaa ambao uchaguzi unafanyika, hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na serikali au Bodi ya Utabibu, amejiandikisha kupiga kura katika kitongoji au mtaa au kijiji husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kupima kila mtu dawa homa ya ini

**MOJA** ya taarifa zilizotikisa wasomaji wengi wakati huu tunapoelekea mwisho wa wiki ni kuwapo maambukizi mengi ya homa ya ini hapa nchiniUgonjwa ambao kitaalamu huitwa 'Hepatitis B,' unatajwa kuwa ni maradhi ya ini yanayosambazwa na kirusi kiitwacho 'hepatitis B virus.'

Taarifa za kitaalamu zinasema unaathiri ini na chanzo cha saratani ya ini na kwamba leo ni moja ya magonjwa hatari duniani, ikielezwa kuwa yanasambazwa kwa njia kadhaa kama kulishwa damu, kujamiiana, mama kuwaambukiza watoto wakati wa kujifungua na hata kumhudumia mwathirika bila kuwa na tahadhari. Ugonjwa huo hauambukizwi kwa kula ama kushirikiana vyombo vya kulia, hauingii mwilini kupitia kunywa maji wala kukumbatiana, kushika mikono au kupitia njia za kuumwa na wadudu kama mbu na wengine wanaoshambulia binadamu.

Ugonjwa huo una dalili kubwa ambayo inatambulisha tatizo la ini nayo ni mwili kuwa wa manjano. Macho, kucha na ngozi huwa na rangi ya machano. Dalili nyingine ni homa, kuumwa viungo, kuchoka, kuhisi kichefuchefu, kutapika, maumivu ya tumbo, kubadilika rangi ya mkojo na wakati mwingine kuwa na rangi nyeusi.

Kwa kuwa serikali inaliona hilo kama tatizo kubwa na la kutisha pengine ni lazima kuwachunguza wananchi kama ambavyo uchunguzi unafanyika kwa kila mtu anayekwenda hospitali kupata matibabu anavyopimwa VVU na Ukimwi.

Tunaona kuwa kama maradhi hayo sasa ni kitisho kikubwa kiafya pengine wakati umefika wa kuanzisha mkakati kama huo wa 'furaha yangu' wa kuwapima Watanzania wote Hepatitis B ili kufanikisha kuanza matibabu mapema.

Inawezekana watu hawana VVU wala Ukimwi, lakini kupitia kujamiiana wameambukizwa virusi vya homa ya ini. Lakini pia huenda tatizo hilo lilikuwapo kwa muda mrefu na watu walikuwa hawajafahamu kuwa ni homa ya ini.

Kwa vile maradhi haya yanatajwa kuwa ni ugonjwa unaotishia afya duniani zama hizi tunaamini kuwa huenda kuna mahali kulikuwa na tatizo la kiudhibiti pengine kwenye kuchunguza damu zilizokuwa zinatolewa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa. Tunaweza kujiaminisha kuwa pengine ni ugonjwa unaosambaa kwa kasi nyakati hizi, lakini huenda sivyo, ulienea siku nyingi kutokana na taratibu za kupima damu.

Tunajiuliza hivi taratibu za kuchunguza virusi vya Hepatitis B ndani ya damu zilianza lini kwa Tanzania na sehemu nyingine duniani? Inawezekana hapo awali utaratibu huo haukuwapo au pengine haukutiliwa sana maanani na huenda kipimo cha HIV na VVU kilipewa kipaumbele zaidi.

Aidha, wadudu hao wanasambaa zaidi zama hizi kutokana na siku za nyuma huduma za afya kutokuliona kama tatizo kubwa, lakini huenda kupitia kuwalisha wagonjwa damu, maradhi hayo yakasambaa kupitia kuongezewa damu tatizo linaloweza kuwa kubwa kwenye nchi maskini kama Tanzania.


Aidha, uwezekano wa ugonjwa huo kuwa kitisho zaidi cha afya duniani umetokana na kutokuupa kipaumbele kwenye matumizi ya chanjo?

Tofauti na miaka ya nyuma zama hizi ndizo zimekuwa na msisitizo mkubwa wa kuchunguza homa ya ini kwa kuwapima wajawazito na watoto wachanga iwapo wana virusi vya homa hiyo na kuwaanzishia matatibabu.

Ugonjwa huo sasa ni tatizo na ni moja ya mambo yanayotatiza afya za Watanzania. Hata hivyo si muda wa kulia, ni wakati wa kutafuta ufumbuzi.

Ndiyo maana tunashauri pamoja na kufikiria uwezekano wa kuanza kuwapa wagonjwa tiba ya kupunguza nguvu ya VVU za ARVs ni vyema pia kuanza kuwapima wagonjwa wote wanaokwenda hospitalini kama inavyofanywa kwa VVU ili kuwatambua na kuwahudumia walioathirika na homa ya ini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Somo zuri staili ya kutaarifu matumizi Musoma Vijijini



Na Sabato Kasika

**KUWAPO** fedha za mfuko wa jimbo ni utaratibu uliobuniwa na serikali, lengo ni kuchochea na kuongeza kasi ya miradi ya maendeleo inayoibuliwa na wananchi majimboni.

Fedha hizo zinasimamiwa na Sheria Namba 16 ya Mwaka 2009 inayomtaka mbunge kuzielekeza katika miradi inayoibuliwa na wananchi wake.

Serikali ilifikia hatua hiyo kuanzisha mfuko huo, ili kurahisisha maendeleo katika majimbo ya Bunge husika, kutambua kwamba wabunge wapo karibu na wapiga kura wao na itawawia rahisi kutekeleza maendeleo.

Kwa maana hiyo, miradi ya maendeleo inafanyika kwa juhudi za wananchi wanaoshirikiana na wabunge, pamoja na Serikali Kuu kama mchochezi mkuu anayetoa fedha hizo.

Sheria na mwongozo wa fedha za mfuko wa jimbo, vinamtaka mbunge kuunda kamati ya usimamizi wa fedha za mfuko huo, akishirikiana nao kwa karibu.

Hivyo, kamati huwa na wajumbe sita, mbunge akiwa mwenyekiti wake. Mchumi wa manispaa au halmashauri, ni katibu wa kamati na wajumbe ni madiwani wawili wa kata; mwanaume na mwanamke, watendaji kata wawili na mwakilishi wa taasisi zisizo za kiserikali.

Hivyo, ili kuondoa utata kuhusu matumizi ya fedha, baadhi ya wabunge wakishirikishwa na wananchi wao ili wajue hatua kwa hatua, jimbo lao linapata kiasi gani na kinatumikaje.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, ni miongoni mwa wabunge wanaozingatia hilo na amekuwa akifanya hivyo, kwa uwazi kwenye mikutano ya hadhara, kwa vile anatambua fedha hizo ni za umma.

Wiki iliyopita, mbunge huyo aliitisha mkutano katika Kata ya Etaro, kuelezea kiasi cha fedha ambacho jimbo limepokea katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 cha Sh. milioni 52.43 na jinsi zitakavyotumika.

Ingawa mkutano huo ulifanyika katika Kata ya Etaro, lakini ulishirikisha wajumbe kutoka kata zote 21 zinazounda Jimbo la Musoma Vijijini, ni kufikisha taarifa kwa wananchi.

Aliweka wazi kwamba miundombinu ya elimu kwenye shule za msingi na sekondari bado inahitaji kuboreshwa, hivyo fedha za mfuko huo zitachangia juhudi za wananchi kuboresha miundombinu hiyo jimboni. Profesa Muhongo, aliweka wazi kwamba, fedha taslimu hazitolewi kwa walengwa na badala yake wanapewa vifaa vya ujenzi vilivyoombwa na kununuliwa na halmashauri. Kwa uwazi huo, ninaamini unaweza kusaidia kuepusha manung'uniko kutoka kwa wananchi kama ambavyo yamekuwa yakisikika kutoka kwenye baadhi ya majimbo kwamba 'fedha hizo zinaliwa na wajanja wachache.'

Pia inakuwa si kuepusha manung'uniko kutoka kwa wananchi tu, bali inadhibiti matumizi ya ovyo ya fedha hizo, ambazo lengo ni kuchochea kasi ya maendeleo kwenye majimbo mbalimbali nchini.

Tangu achaguliwe, mbunge huyo anasema amekuwa akihamisha mikutano ya ugawaji wa fedha za mfuko kutoka kata moja kwenda nyingine huku wajumbe wa kata zote wakihudhuria.

Mjadala huo, ninaamini kwamba majimbo yote zaidi ya 200 yakiiga mfano huo wa Musoma Vijijini, hakutakuwa na manung'uniko kutoka kwa wananchi kuhusu matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo.

Mnamo Aprili mwaka huu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Simiyu, ilikaririwa na vyombo vya habari kudai imebaini ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu katika matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo.

Tuhuma hizo zilihusu majimbo ya Meatu, Itilima, Bariadi na Busega mkoani humo, kwamba fedha za mfuko huo zimetumika bila ya kuidhinishwa na vikao husika vilivyotajwa katika sheria na kanuni za matumizi yake.

Ni kauli ya Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Simiyu, Adili Elinipenda, katika taarifa ya utendaji kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Desemba 2018 hadi Machi mwaka huu.

Alisema matumizi ya fedha hizo yamekiuka Sheria ya Fedha za Kuchochea Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009.

# HABARI PICHANI



Ofisa Mkuu wa Biashara wa Kampuni ya Tigo, Tarik Boudiaf, akisalimiana na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, wakati alipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Masoko wa IPP, Joyce Luhanga (kushoto), Meneja Masoko na Mauzo, Kauthar D'souza (wa pili kushoto na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo.



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo, akifafanua jambo kwa Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf, alipotembelea chumba cha habari cha magazeti ya The Guardian na Nipashe jana.



Meneja Uchapishaji wa Kampuni ya The Guardian Ltd, Venkadachalam Balasubramanian, akimfafanulia jambo Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf, alipotembelea kiwanda cha uchapaji magazeti.



Meneja Vipindi wa Televisheni ya EATV, Sophia Mng'anyi, akimfafanulia jambo Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf, alipotembelea kituo hicho jana.



Mkurugenzi Msaidizi wa Capital Radio, Abdallah Mwaipaya, akifafanua jambo kwa Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf, alipotembelea kituo hicho jana.



Mkurugenzi wa Chaneli wa ITV/Radio One, Koigi Macharia, akielezea kazi zinazofanywa na moja ya studio za ITV kwa Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**

# Umati wamuaga Mhariri Dilunga Dar

Beatrice Moses

MWILI wa aliyekuwa Mhariri wa Gazeti la Jamhuri, Godfrey Dilunga, umeagwa na umati wakiwamo viongozi wa serikali na vyama vya siasa.

Dilunga (43) alifariki dunia usiku wa kuamkia Jumanne ya Septemba 17, mwaka huu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Dar es Salaam, alikokuwa amelazwa akipatiwa matibabu.

Viongozi hao ni pamoja na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, Msemaji Mkuu wa Serikali, Hassan Abasi na Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa.

Wabunge kadhaa wakiwamo Amina Mollel, Nape Nnauye na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa katika Serikali ya awamu ya nne, Bernard Membe. Mwakyembe alisema msiba wa Dilunga umewagusa viongozi wote akiwamo Rais John Magufuli, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kutokana na uandishi wake mahiri.

Membe alisema anathamini mchango wa vyombo vya habari, ndiyo maana amefika katika msiba huo, akiguswa na kumbukumbu ya namna ya uandishi wa habari alikuwa huru. "Nilikuwa nawasiliana naye mara kwa mara, alikuwa ananiuliza vitu kadhaa, alikuwa huru, ni afya vyombo vya habari vikiwa huru," alisema Membe.

Viongozi wengine wa siasa waliohudhuria ni pamoja Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Zanzibar, Salum Mwalimu. Viongozi hao kila mmoja alitumia nafasi yake kuelezea Dilunga alivyofanya nao kazi vizuri ambapo Polepole alibainisha kuwa alikuwa ni mwandishi pekee aliyemfanyia mahojiano mgombea wao wa urais wa mwaka 2015, Rais Magufuli. Zitto alieleza Dilunga alikuwa miongoni mwa waandishi waliobadili uandikaji wa kampeni za vyama vya upinzani kwa kuandika habari bila upendeleo. Dilunga alilazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Septemba 9, mwaka huu, akitokea Hospitali ya Mwananyamala kwa rufani kutokana na tatizo la maumivu ya tumbo.

Madaktari na wauguzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wamejitahidi kwa kila hali, ila Mungu amempenda zaidi.

Mwili ulisafirishwa jana kwenda mkoani Morogoro utazikwa leo.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, akikabidhiwa bendera ya Wenyekiti wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi wa Nchi za Mashariki mwa Afrika (EAPCCO) kutoka wa mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Mkuu wa Jeshi la Polisi Sudan, Abdi Mohammed Bashir, kwenye ufunguzi wa Mkutano wa 21 wa Wakuu wa Polisi wa nchi hizo, katika ukumbi wa AICC Arusha jana. PICHA: IKULU

# Mjadala kura polisi kabla uchaguzi

INATOKA UK. 2

iwapo itatekelezwa kama ilivyokusudiwa, itaepusha mitafaruku na migogoro," alisema.

Naye mwanaharakati wa masuala ya kijamii, Dadi Kombo Maalim, alisema hakuna haja ya kuwa na kura ya mapema na badala yake waliorodheshwa katika sheria ya uchaguzi kupiga kura hiyo, watengewe muda siku yenyewe ya uchaguzi kufanya hivyo.

Alisema kuwapo kwa kura hiyo ya mapema hakutakuwa na uchaguzi huru na haki kwa kuwa kuwapo kwa sheria hiyo ni kutoheshimu mabadiliko ya 10 ya kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

"Sheria hiyo ya uchaguzi haina tija na mantiki yoyote kwa sababu huwezi kutengeneza sheria kwa kikundi cha watu fulani kwa fursa ya kupiga kura," alisema.

Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa ACT Wazalendo, Salum Bimani, alisema hakubaliani na kuwepo kura ya mapema kwa kuwa ni utaratibu ambao umelenga kuvuruga uchaguzi.

Alisema utaratibu huo utasababisha kuingiza wapigakura hewa kwa lengo la kukilinda chama tawala kiendelee kubaki madarakani.

**ZEC YAFAFANUA**

Kutokana na mjadala huo, ZEC imetoa ufafanuzi huku Mkurugenzi wa Huduma za uchaguzi wa tume hiyo, Idrisa Haji Jecha, akisema kura hiyo itawahusisha askari na watendaji ambao watasimamia uchaguzi na wala si kwa askari wa jeshi lote kama ilivyodhaniwa na baadhi ya wanasiasa.

Akizungumza jana na Nipashe, alisema upigaji kura huo utakuwa na utaratibu maalum kwa askari au watendaji watakaosimamia uchaguzi kutakiwa kuiandikia barua tume hiyo mapema ili kupewa kipande maalum kitakachowatambulisha kupiga kura hiyo.

Kwa mujibu wa Jecha, askari au mtendaji yeyote atakayesimamia uchaguzi atakayeomba nafasi hiyo, ataruhusiwa kwenda kupiga kura katika kituo alichojiandikisha siku moja kabla ya uchaguzi.

"Hii kura ya mapema naona watu wameielewa vibaya. Haitakuwa na udanganyifu wowote kwa sababu kabla ya uchaguzi kutakuwa na orodha kamili ya watu wote watakaopiga kura ya mapema na majina yao yatawekwa hadharani," alisema Jecha.

Alisema kwa mujibu wa Sheria mpya ya Uchaguzi ya mwaka 2018 kifungu cha (82), tume itaweka utaratibu utakaoruhusu upigaji wa kura wa mapema ambao utafanyika siku moja kabla ya siku ya upigaji kura au siku nyingine yoyote kama itakavyoamuliwa na tume. Pia alisema kifungu hicho kinaeleza kuwa upigaji kura wa mapema chini ya kifungu kidogo cha (1) utatumika katika uchaguzi mkuu au uchaguzi mdogo wa urais pekee.

Alisema kura hiyo itawahusisha kura watakaotelekeza majukumu ya uchaguzi kama msimamizi wa uchguzi, msaidizi msimamizi wa kituo, askari polisi, mjumbe au mtendaji wa tume.

"Mpigakura ambaye atahusika na kazi za ulinzi na usalama siku ya kupiga kura," alisema Jecha alikinukuu kifungu hicho.

Alisema tume ya uchaguzi itakaa na wadau wa uchaguzi ili kuwapa elimu kuhusiana na sheria hiyo ili nao kwenda kutoa elimu kwa wanachama wao. Juzi, Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous, alisema lengo la vikosi hivyo na watendaji wa tume kupiga kura siku moja kabla ni kuruhusu makundi hayo kupata haki ya kupiga kura na kutekeleza majukumu yao ipasavyo siku ya uchaguzi.

Akifungua mafunzo ya siku tatu kwa waandishi wa habari kuhusu kuandika habari za uchaguzi mkuu, alisema hatua hiyo ya kura ya mapema imetokana na marekebisho ya Sheria Na. 4 ya Tume ya mwaka 2018 ambayo inatoa nafasi kwa makundi hayo.

Alisema marekebisho hayo yamekuja baada ya kubainika makundi hayo hayaitumii haki ya kidemokrasia kupiga kura na kuwachagua viongozi kutokana na kutingwa na majukumu ya kazi katika siku hiyo.

"Marekebisho hayo sasa yatawapa nafasi baadhi ya watendaji waliokabidhiwa majukumu, kupiga kura siku moja kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika," alisema.

## Wajanja wategesha mali uthamini Nyamongo

INATOKA UK. 4

madirisha.

Mthamni Mkuu wa Serikali, Evelyne Mugasha, ambaye juzi alitembelea baadhi ya nyumba hizo kukagua maendeleo ya uthamini katika eneo hilo, aliweka wazi kuwa ofisi yake inafanya kazi kwa kufuata sheria ya uthamini na hatua kali zitachukuliwa kwa mtu atakayeonekana kufanya udanganyifu kwa lengo la kujipatia kipato.

Kwa mujibu wa Mugasha, uthamini katika eneo la Nyamongo unaohusisha vitongoji vitatu katika kijiji cha Matongo, limekuwa likifanyika kwa uwazi na kushirikisha pande zote wakati wa kuorodhesha mali na kufafanua kuwa hata mwananchi asiyeridhika na uthamini, hupewa fomu maalum ya kujaza lengo likiwa kutoa haki.

"Tumeona watu walihamisha magodoro, vitanda na mizigo mingine ili kupata posho ya makazi na faida. Kushangaza baadhi ya wapangaji hawajui hata choo cha nyumba wanayooishi kilipo. Ofisi yangu haitavumilia vitendo hivyo, kila mtu atalipwa anachostahili," alisema.

Mthamini kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Lazaro Magumba, alisema wakati wa uthamini, kumekuwa na changamoto hasa wakati wa kukagua mali za wananchi.

Alisema changamoto hiyo hutokana na baadhi yao kuwa na dhana ya kujipatia utajiri kupitia mradi huo na hufanya maendelezo ya kuegesha maarufu kama 'tegesha' ili kulipwa fedha nyingi.

"Wananchi wanajenga nyumba zilizopangana na hakuna hata nafasi na wakati wa uthamini. Usiku kucha watu wanahamisha vyombo, magodoro na wengine hata wanyama ili ionekane ni makazi halali," alisema Magumba.

Alisema wanachokifanya wao ni kukagua kwa awamu kwa lengo la kujiridhisha kama kweli walionekana wakati wa uthamini kama ni wakazi halali ama walienda kutegesha.

Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Matongo, ambao hawakupenda majina yao yawekwe wazi kutokana na sababu za kiusalama, walikiri kuwapo mchezo huo wa 'tegesha' lakini walidai hufanywa na watu wasio wakazi wa muda mrefu katika kijiji hicho bali walienda kwa lengo la kujipatia faida kupitia uthamini huo.

Kwa mujibu wa wakazi hao, baadhi ya wananchi kutoka nje ya kijiji hicho walinunua nyumba au maeneo kwa wenyeji na kuongeza vyumba na kuwapangisha watu kuishi ili kuvizia uthamini kwa lengo la kupata faida.

Kwa muda mrefu, wananchi wa Nyamongo, hasa wale wanaoishi vitongoji vinavozunguka mgodi wa North Mara, wamekuwa wakilalamikia uchafuzi wa mazingira hasa maji yanayotiririka kutoka mgodi huo kuwa yana sumu inayoathiri afya zao jambo lililomlazimu Rais John Magufuli wakati wa ziara yake mkoani Mara, kuagiza kufanyika utafiti ili kubaini ukweli huo.

## HABARI KITAIFA

# Mradi wafagiliwa kutoa fursa kilimo cha alizeti

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SINGIDA

MKOA wa Singida umeipongeza programu ya kuendeleza mifumo ya kimasoko ya kilimo nchini (AMDT) kwa kushirikiana na wadau pamoja na serikali, katika kuhakikisha wakulima na wadau katika mnyororo wa zao la alizeti wananufaika kupitia zao hilo.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alipotembelewa na baadhi ya wajumbe wa bodi ya taasisi hiyo, katika ziara maalumu ya kikazi yenye lengo la kujionea mafanikio na kujifunza changamoto mbalimbali katika utekelezwaji wa miradi ya alizeti na mahindi ambayo inatekelezwa na taasisi hiyo mikoa mbalimbali nchini.

Dk. Nchimbi alisema jitihada zinazofanywa na AMDT kwa kushirikiana na Shirika la Faida Mali, kama mwezeshaji wa soko, zimekuwa na manufaa makubwa kwa Mkoa wa Singida, kwani zimechochea na kuifanya jamii ya wakulima wa mkoa huo kuona umuhimu wa kilimo cha alizeti.

Alisema kufuatia jitihada hizo pamekuwapo na mwitikio mkubwa wa vijana na wanawake katika kufanya kilimo cha zao hilo, hatua ambayo imechochea pia kuongezeka kwa uzalishaji na kuchangia katika kupunguza changamoto ya uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Alisema Mkoa wa Singida umejiwekea mkakati wa kuhakikisha alizeti inakua kwa kasi na kutoa rai kwa vijana wa mkoa huo wenye mawazo ya kutafuta maisha katika miji mingine mikubwa kuiga mfano wa vijana na wanawake waliochangamkia fursa kupitia kilimo cha alizeti mkoani humo. "Vijana wengi wanaamini maisha yako mijini, bila kujua kuwa fursa nyingi za kiuchumi zipo katika sekta ya kilimo, hivyo nitoe rai kwa vijana wa mkoa wangu kuona haja ya kuiga mfano wa vijana wenzao ambao wameshaanza na kuona mafanikio makubwa kupitia kilimo hiki kwa kutumia mbegu bora na kufuata kanuni bora za kilimo," alisema.

Baadhi ya wakulima wa zao la alizeti mkoani humo waliopata pia fursa ya kutembelewa na wajumbe wa Bodi ya AMDT, walishukuru taasisi hiyo kwa namna ambavyo imekuwa msaada kwao, hasa kupitia Shirika la Faida Mali ambalo limewaunganisha na wadau wanaotoa mafunzo mbalimbali kama kilimo biashara, matumizi ya mbegu bora, umuhimu wa bima ya mazao na namna ya kuongeza thamani ya mazao yao.

Felister John ni mkulima wa alizeti, kutoka Kijiji cha Mangida Kata ya Msange katika Wilaya ya Singida Vijijini, alisema amekuwa akijihusisha na kilimo cha alizeti kwa muda mrefu na ameyaona mafanikio kupitia kilimo hicho.

Jasmine Chumi, mkulima kutoka Kata ya Msenga katika Wilaya ya Singida Vijijini, alisema kupitia kilimo hicho ameweza kuwasomesha watoto wake pamoja na kujenga nyumba nzuri ya kisasa.

Meneja Mradi wa Faida Mali, Christopher Mkondya, alisema kwa kushirikiana na wafadhili wao ambao ni taasisi ya AMDT, wamelenga katika kuboresha mifumo ya masoko katika zao la alizeti mkoani Singida.

Mradi huo wa alizeti unaotekelezwa na Faida Mali kupitia ufadhili wa programu ya AMDT unatarajia kuwanufaisha wakulima takribani 32,000 katika Wilaya za Ilamba, Mkalama, Ikungi, Itigi na Singida Manispaa.



Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo (katikati), akipewa maelezo ya ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Muheza jana na Kaimu Mhandisi wa Wilaya hiyo, Ramadhani Mtinge (kulia). Wengine ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martini Shigela na Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Sera ya misitu yaiva, wadau wapendekeza

**Na Kelvin Innocent**

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imesema sera ya misitu imekamilika, lakini baadhi ya wadau hususan sekta binafsi wameomba wakae ili waipitie.

Hayo aliyasema jijini Dar es Salaam Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Sera hii imekamilika lakini wadau wa sekta binafsi waliomba tukae tena chini wajaribu kuiangalia na kuipitia tulikuwa na mazungumzo mazuri," alisema.

Alisema wadau walisema wafanye hivyo kama sehemu ya kuchangia uchumi wa viwanda na kuiangalia misitu kama fursa ya utalii.

"Tumekubaliana tutakuwa na mkakati ambao utachochea viwanda ambavyo vinatumia kwa ufanisi zaidi malighafi zitokanazo na misitu. Tunakaribia kukamilisha sera hii na kuiingiza kwenye mchakato ili iweze kukubalika serikalini," alisema.

Prof. Mkenda alisema sera hiyo italeta mageuzi na kwamba misitu itakuwa siyo suala la uhifadhi bali kwa ajili ya viwanda na utalii.

Kuhusu nyuki, alisema: "Zamani tulikuwa na kiwanda kimoja Kibaha cha kuchakata asali sasa kimekufa, kingine kilikuwapo Kipalapala nacho kimekufa."

"Sasa tumetenga takribani Sh. bilioni 1.8 kuanzisha viwanda vya kuchakata asali, tumekubaliana kabla ya kuanza kuwekeza kwa namna yoyote ile lazima tujue ni kwa nini vile viwanda vilivyokuwapo vimekufa," alisema.

Alisema kupitia Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania (TFS), halmashauri na vijiji wanaendelea kulinda misitu iliyopo kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya mvua, vyanzo vya maji.

# Wabunge kutoka Uingereza, Ujerumani watembelea nchini

**Na Mwandishi wetu**

WABUNGE kutoka nchini Uingereza na Ujerumani walio wanachama katika mapambano ya malaria, wametembelea umoja wa wabunge wa kupambana na malaria na magonjwa ya ukanda wa joto yasiyopewa kipaumbele (TAPAMA & NTD).

Wabunge hao watakuwapo nchini kwa mwaliko wa Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa Tapama kwa ziara ya siku nne hadi leo.

Aidha, wabunge hao wametembelea mkoa wa Kilimanjaro na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa huo, Anna Mghwira, na kutembelea Kituo cha Afya Karume, wilayani Rombo, juu ya miradi mbalimbali yenye lengo la kutokomeza malaria.

Mghwira aliwashukuru kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kutokomeza ugonjwa wa malaria na magonjwa yasiyopewa kipaumbele.

Wakiwa kituo cha Karume, walishuhudia wananchi waliokusanyika kwa ajili ya kupatiwa huduma za tiba ya macho kutokana na ugonjwa wa vikope.

Katibu wa Tapama, Dk. Raphael Chegeni, alisema lengo la ziara hiyo ni kutoa nafasi kwa wawakilishi wabunge hao kutembelea kukutana na wabunge nchini, ili kujadili njia za kushirikiana na kuweka mikakati ya pamoja ya kuisaidia Tanzania kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030 na magonjwa ya ukanda wa joto yasiyopewa kipaumbele (NTD).

Mkurugenzi Mtendaji wa Tapama, Dk. Hermengild Mayunga, alisema ziara hiyo pia itasaidia kutoa nafasi kwa wabunge hao kujifunza na kujionea changamoto ambazo serikali ya Tanzania inakumbana nazo katika harakati za kutokomeza malaria na NTD nchini.

"Fursa hii itasaidia kuongeza ufahamu kwa Bunge la Uingereza waweze kuishauri serikali yao kwa kupitia Shirika lao la Maendeleo (DFID) kuongeza usaidizi wa rasilimali na ushirikiano katika mipango ya kupambana na malaria kwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya mpango wa kupambana na malaria (NMCP) na mpango wa kutokomeza magonjwa ya ukanda wa joto yasiyopewa kipaumbele NTD," alisema.

# Wanakikundi walilia msaada

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAJASIRIAMALI wa kikundi cha 'Yarabi Tupe' kilichopo kijiji cha Furaha shehia ya Mvumoni Wilaya ya Chakechake, Pemba kinachojishughulisha na ushonaji wa mikoba ya ukili, wameiomba serikali na mashirika binafsi, kuwasaidia fedha za kumalizia ujenzi wa ofisi yao, ili iweze kukamilika na kulitumia kwa kufanyia shughuli zao.

Walisema jengo hilo limefikia hatua ya mwisho kumalizika, hivyo wanahitaji kusaidiwa fedha ili wanunue bati, milango pamoja na saruji za kupigia plasta au kusaidiwa vifaa vya kuweza kumalizia jengo hilo.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi wanaushirika hao walisema, wamehamasika sana katika kuanzisha vikundi vya ushirika, kutokana na kipato wanachojipatia ambacho kinawasaidia kujikwamua na hali duni ya maisha.

"Tumejitahidi kujenga mpaka tumefikia hatua ya mwisho, hivyo tunaiomba serikali na mashirika binafsi kutusaidia kumaliza ofisi yetu, tufanyie shughuli zetu za ushonaji wa mikoba, kwa sasa tunatumia nyumba ya mtu, jambo ambalo ni usumbufu," alisema mmoja wa wanakikundi.

Safia Hamad, Katibu wa kikundi hicho, alisema changamoto nyingine zinazowakabili ni ukosefu wa nyenzo za kufanyia kazi.

"Tunatumia soko la ndani zaidi kuuza mikoba yetu, huwa tunakwenda kuuza uwanja wa ndege, tunashukuru sana tunapata pesa angalau za kununulia chakula na kuwahudumia watoto wetu, japo ni kidogo lakini sihaba," alisema katibu huyo.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Asha Makame Alawi, alisema lengo la kuanzisha ushirika huo ni kujikwamua na umaskini, hivyo aliwaomba kusaidiwa nyenzo muhimu za kufanyia kazi, pamoja na kutafutiwa soko la nje na ndani ya nchi.

"Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa-Zanzibar) waliotupa mafunzo ya utengenezaji wa mikoba, sabuni, kilimo, ufugaji na ushonaji, ili tuweze kujikomboa na tunashukuru, ingawa soko bado linatutatiza," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, akitembelea miradi ya kilimo na ufugaji inayoendeshwa na vijana katika vijiji vya wilaya za Babati mkoani Manyara na Kondoa mkoani Dodoma. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Agizo halmashauri kutenga maeneo ya vijana

**Na Idda Mushi,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, ameziagiza halmashauri zote za wilaya nchini kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuwawezesha vijana kutekeleza miradi mbalimbali.

Miradi hiyo ni inayohusu kilimo, mifugo na uvuvi, na hatimaye kuwa na uwezo wa kujiajiri na kujikwamua na umaskini.

Mavunde alisema hayo baada ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo ya vijana kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika vijiji vya Dareda wilayani Babati mkoani Manyara na Hurui wilayani Kondoa mkoani Dodoma, inayotekelezwa na mradi wa uwezeshaji vijana Oye, unaotekelezwa na SNV kupitia Shirika la Maendeleo la SDC.

Akibainisha serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Waziri Mkuu, wamekuja na mpango mkakati mahususi wa kuwahusisha vijana kwenye kilimo kwa kutoa mafunzo na kubadilisha mitizamo yao kwa kuwa asilimia kubwa ya vijana wanaamini kilimo sio suluhisho ya matatizo yao na wanaamini katika kazi nyingine.

"Hatua ya kwanza ni kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Morogoro, kwanza kubadili mtizamo wa vijana na kuwafanya wakipende kilimo, lakini hatua ya pili tunafanya uwekezaji mkubwa kupitia ofisi ya Waziri Mkuu na tumeanza na mpango mkakati wa kuwajengea uwezo vijana 100 nchi nzima," alisema na kuongeza:

"Kati yao, 80 watafundishwa kilimo cha mboga kupitia Green House yaani kitalu nyumba, ambazo tayari zimeshafungwa katika baadhi ya maeneo katika mikoa 12 na vijana 20 watajifunza kutengeneza kitalu nyumba, ili iwe ni sehemu ya ajira na tusipate gharama kubwa kuagiza toka nje ya nchi."

Alisema hatua ya tatu wanayofanya ni kuwawezesha vijana kupitia mifuko ya maendeleo ya vijana na asilimia 10 za mapato ya halmashauri nchi nzima, hivyo alihimiza utengwaji wa maeneo hayo kusaidia miradi hiyo inayoanzishwa na vijana.

Alizitaka taasisi nyingine nchini kushirikiana na serikali kutatua changamoto kubwa ya ukosefu wa ajira kwa vijana kupitia sekta ya kilimo, na kwamba kwa kushirikiana pamoja wataweza kuleta mapinduzi makubwa na falsafa ya uchumi wa viwanda itafanyika kivitendo.

Mshauri wa biashara wa mradi wa Oye, Faustine Msangila, alisema wameweza kusaidia vijana zaidi ya 8,000 kati ya 6,500 waliolengwa katika awamu ya kwanza ya mradi huo iliyoanza mwaka 2016, katika mikoa ya Shinyanga, Manyara, Singida, Tabora, Dodoma, Morogoro na kwamba wana mpango wa kuendeleza awamu ya pili ya mradi huo ili kwa kushirikiana na serikali wawafikie vijana zaidi ya 20,000 katika mikoa mingi zaidi inayokadiriwa kuwa kati ya 10 hadi 15.

Mshauri wa ufuatiliaji na tathmini kutoka SNV, Rashid Byarushengo, alisema wamekuwa wakiwakusanya vijana na kuwapa mafunzo na zana mbalimbali za kilimo ikiwamo pampu za maji za kutumia mafuta, mipira ya mita inayokadiriwa kufikia 200 kwa kila kikundi, mbolea, viuatilifu, na kuanza kwa kuanzisha mashamba darasa ambayo huyatumia kama sehemu ya kujifunzia.

# Mamlaka zaelekezwa utoaji leseni za uvuvi

**Na Restuta Damian,** MULEBA

SERIKALI imezitaka mamlaka zinazohusika na utoaji wa leseni kwa mazao yatokanayo na sekta ya uvuvi kwa wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali za samaki wilayani Muleba mkoani Kagera.

Pia zimeagizwa utolewaji wa leseni hizo ufuate taratibu bila kuvunja sheria na kukwepa kulipa kodi.

Maelekezo hayo yalitolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipokuwa akizungumza na wavuvi na wachakataji wa samaki ili kutafuta ufumbuzi wa namna ya kuongeza uzalishaji wa thamani kwa pato la Taifa kupitia sekta ya uvuvi inayoonekana kuwa na kiwango cha chini cha uzalishaji ikilinganishwa na Uganda na Kenya.

Ulenga alisema mamlaka hizo ziache wananchi washindane katika biashara ya kuuza mazao ya samaki ilhali mradi wa leseni ya biashara ifuate taratibu za ulipaji mapato na kuonyesha kuwa taifa linapata mapato ya kukuza uchumi wake.

"Acheni watu wapambane kufanya biashara iwe za mifupa, mabondo, vichwa vya samaki, dagaa ilhali amepatiwa leseni ya biashara ambayo itamtaka alipie mapato ya zao analofanyia biashara," alisena.

Alisema lengo ni kuona pato la serikali linainuka pamoja na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

Alisema mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa unakadiriwa kuwa asilimia 1.5 hadi tatu kutoka katika Ziwa Victoria kutokana na samaki aina ya sangara, sato, dagaa na wengine, na kwamba kwa mwaka mmoja kwa nchi tatu ni Sh. trilioni sita.

Aidha, Ulega alisema licha ya kuwa Tanzania kuwa na eneo kubwa la Ziwa Victoria kwa asilimia 51 wakati Uganda ni 43 na Kenya ni asilimia sita pekee, nchi zinavua kwa kiwango cha juu na mapato, lakini Tanzania uzalishaji ni kidogo.

"Wenzetu wana eneo dogo sana, lakini uzalishaji wa thamani kwa makadirio kwa mwaka mmoja pekee ni mkubwa ukiangalia sisi tuna eneo kubwa asilimia 51, lakini bado tuko nyuma," alisema Ulega.



Diwani wa Tarafa ya Dongobesh wilayani Mbulu mkoani Manyara, Ester Joel, akiuliza swali kwenye taarifa ya kamati ya jamii katika Baraza la Madiwani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Matatizo ya umeme Arusha mwisho 2025

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SHIRIKA la Ugavi wa Umeme (Tanesco), limewahakikishia wateja wake kuwa limejipanga kutatua na kumaliza tatizo la kukatikatika kwa umeme mara kwa mara mkoani Arusha litakuwa limemalizika kabla ya mwaka 2025.

Hayo, yalisemwa na Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Raymond Seya, wakati akizungumza na waandishi wa habari, alipokuwa akifunga semina ya kuwajengea uwezo wahandisi wa matengenezo na mameneja wa shirika hilo wa mikoa na kanda ya kaskazini.

Alisema awali kulikuwa na tatizo la kukatika umeme mara kwa mara, lakini sasa hivi wamejipanga kutatua tatizo hilo, kwa kufanya maboresho zaidi kwenye sehemu mbalimbali ili usikatike mara kwa mara. Aidha, alisema shirika hilo, litaendelea kuboresha utoaji wa huduma hiyo kufikia viwango vya kimataifa ili wateja waridhike na huduma wanayoitoa na wanayoipata. "Lengo la semina hii ni kuhakikisha wahandisi wetu wanafanya kazi usiku na mchana kuwahudumia wateja ili kwamba watatue tatizo la kukatikatika kwa umeme ambayo ni kero inayolalamikiwa mara kwa mara kitendo kinachoisababishia serikali na shirika ukosefu wa mapato," alisema Seya.

"Mapato haya yanapotea viwandani wakati umeme unapokatika, mfano kwenye kiwanda cha kutengeneza plastiki umeme ukikatika wakati wanaendelea kuzalisha kinachotokea ni kuharibu mtiririko waliokuwa wakitumia kutengeneza bidhaa hizo," aliongeza Seya.

Alieleza kuwa ni matarajio yao kuwa watahakikisha kila mwananchi ananufaika na huduma ya umeme ambao utakuwa wa uhakika kila siku na kila wakati.

Hata hivyo, alisema kuwa sera ya serikali ni kufikia uchumi wa kati na wa viwanda hivyo ni lazima waboreshe huduma ya umeme kuwa ya uhakika ili kuwavutia wawekezaji wengi.

Meneja Mwandamizi na Usambazaji wa Tanesco, Mhandisi Mahende Mgaya, alisema mafunzo hayo yalianza kwa kufuatilia na kuangalia chanzo kikuu cha kukatika umeme, kuanzia mwaka 2015 na baada ya hapo wakatengeneza mpango mkakati wa kutatua changamoto hiyo. "Lengo letu ni kuweka mpango mkakati utakaoendana na sera ya nchi ili tuweze kufikia uchumi wa kati na viwanda ni lazima kwanza tuhakikishe tuna umeme wa uhakika na wakutosha na usio katikakatika mara kwa mara," alisema.

Aliongeza kuwa lengo ni kuboresha mipango ya Tanesco ili kupata na kuwavutia wawekezaji wengi kuwekeza viwanda hapa nchini," alisema Mgaya.

Aliongeza kuwa kama nchi nyingine za Afrika zimeweza kumaliza tatizo la kukatika umeme kwenye mataifa yao, basi hata Tanzania linaweza kutatulika kama walivyofanya nchi kama Misri.

## Mufti awapa neno Waislamu nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MUFTI wa Tanzania Sheikh Abuubakari Zuberi, amewataka Waislamu kujenga ushirikiano na kusaidiana ili kulijenga taifa na mshikamano ambao utaepusha migogoro kwenye jamii.

Mutfi Zuberi aliyasema hayo, wakati wa ziara yake ya siku mbili mkoani hapa na kuwataka Waislamu kuendelea kuidumisha amani ya nchi, kwa lengo la kuondoa migogoro baina yao.

Alisema kuishi kwa vifundo sio maagizo ya Uislamu na aliwataka wale wenye vifundo vyao waache na kurudi kwa Mwenyezi Mungu kwani hakuna anayeijua kesho yake hivyo, ni bora kuwa na busara kwa kuwa mcha Mungu na kuishi kwa kuvumiliana na subira ndiyo mwongozo.

"Sio busara kuwa na migogoro ambayo imekuwa ikirudisha shughuli zetu za maendeleo nyuma wala tusiwe watu wa kulalamika kila mara tuchape kazi kwa kujiletea maendeleo na kufanya ibada, hilo ndiyo lengo la Uislamu na hiyo ndiyo Jihad," alisema Mufti Zuberi.

Kwa mujibu wa Mufti huyo, aliwaomba Waislamu wote nchi kuishi kwa kupendana na kuheshimiana na kuwatendea wema wenzao ili kuwavuta kwenye dini.

Aidha, aliwaomba kuondokana na mitazamo yenye chuki baina yao na kuijenga jamii yenye ustaarabu kwani Uislamu unajengwa na mambo mawili makubwa kujitoa na kujitolea katika dini na maisha yao.

"Sasa naomba muishi kwa kufuata misingi ya dini kwa kuwa tuna Qura'an turudi huko pindi tunapohitilafiana," aliongeza Mufti.

Alisema amani ndiyo nguzo ya kuabudu kwa misingi ya kuijenga amani nchini, kwani bila amani ibada yenye utulivu haitakuwapo.

"Kwa kuwa Uislamu ulifika hadi Hispania, lakini walipopishana waliharibu kila kitu hadi bahari ikawa nyekundu, kutokana na wino wa vitabu hivyo, busara ndiyo iwe nguzo ya kuondoa changamoto na kuhakikisha amani inakuwapo," alisisitiza Mufti.

# Wafugaji wajengewa miundombinu ya elimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JAMII za wafugaji wa Lorkisale wilayani Monduli na Malambo wanaoishi katika Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, zimenufaika kielimu baada ya wadau kuwajengea madarasa, kuwapa samani na kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

Ofisa Miradi wa Shirika lisilo la kiserikali la ECLAT Foundation, Bakiri Angalia, alisema shirika hilo ndilo lililokamilisha kazi hiyo.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumzia ujenzi wa miundombinu madarasa mawili kwenye shule hizo, mbili tofauti zinazohudumia jamii ya wafugaji.

Angalia alisema taasisi ya ECLAT Foundation imejenga madarasa hayo yenye thamani ya Sh. milioni 236.

Alifafanua kuwa katika shule ya Lengijabe ya wilayani Monduli, shirika hilo limetumia Sh. milioni 102 kumalizia ujenzi wa madarasa sita. Alisema pia kwenye shule hiyo wametoa madawati 138, ujenzi wa matundu 16 ya vyoo na kuweka mfumo wa uvunaji maji ya mvua.

Aliongeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Msingi Malambo wilayani Ngorongoro gharama iliyotumika ni Sh. milioni 134.

"Tumejenga madarasa matatu na ofisi ya walimu, tumetoa madawati 69 na kuweka mfumo wa nishati ya umeme wa jua," alisema Angalia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Steven Ulaya, akizungumza wakati wa kukabidhiwa madarasa ya shule hiyo, aliipongeza ECLAT Foundation kwa kufanikisha ujenzi huo.

Ulaya alisema wanaahidi kuhakikisha walimu, wanafunzi na jamii ya eneo hilo wanatunza miundombinu ya shule hiyo kwa maendeleo endelevu.

Mwenyekiti wa ECLAT Foundation, Peter Toima, alisema wamekuwa wakizisaidia jamii ya maeneo mbalimbali nchini katika kufanikisha maendeleo.

"Tumefanikisha miradi mbalimbali ikiwamo wilaya za Monduli na Ngorongoro mkoani Arusha, Wilaya ya Simanjiro Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Tandahimba Mtwara na Kakonko mkoani Kigoma," alisema Toima.

# Kiama chaja waliovamia shamba

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI imesema itawaondoa kwa nguvu wananchi 48 waliojenga makazi ya kudumu katika Shamba la Fofo/Foo Estates, Hai, mkoani Kilimanjaro, ifikapo Septemba 23, mwaka huu, baada ya kukaidi amri ya kuhama eneo hilo.

Shamba hilo lenye ekari 46.6 lilifutwa hati yake na Rais na kutolewa kwa wananchi wa vijiji vya Urori, Mulama, Usari na Tella, vilivyoko Narumu, Tarafa ya Lyamungo.

Jana, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alisema: "Niliwapa siku saba hao wananchi wawe wamevunja nyumba hizo wenyewe na kuondoka lakini wamekaidi.

"Waziri wa Ardhi (Nyumba na Maendeleo ya Makazi), William Lukuvi, alishatoa maelekezo na hatuwezi kuacha kusimamia maelekezo ya serikali. Jumatatu ijayo (Septemba 23) nitakwenda kutekeleza operesheni ya kuwaondoa."

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, wananchi hao walijimilikisha shamba hilo wakiwa hawana haki ya umiliki kisheria. Shamba hilo lilifutiwa hati na Rais baada ya kubatilisha miliki Novemba 22, 1993.

Inaelezwa kuwa baada ya watu hao 48 kudaiwa kuvamia shamba hilo, mgogoro mkubwa wa umiliki wake ulizuka kati yao na wananchi wa vijiji vya Urori, Mulama, Usari na Tella ambao ni wanachama wa Chama cha Ushirika cha Narumu/Manushi.

Wiki iliyopita, wakati anazungumza na wananchi wa vijiji hivyo pamoja na waathirika hao 48, Ole Sabaya aliagiza kama kuna ujenzi wowote umeendelezwa usihamishwe na wananchi hao wabomoe nyumba zao.

"Nendeni kabomoeni nyumba zenu wenyewe ndani ya siku saba. Nawaapia kama Mungu aishivyo, nitakuja kusimamia ubomoaji wa nyumba hizo kwenye mashamba ya wananchi na kama mnadhani natania, nisubirini baada ya siku saba," alisema.

"Kama kuna mazao ya msimu nataka yaondoke na si vinginevyo. Kwa mujibu wa sheria hayo ndio mazao tunayoyatambua. Kama kuna nyumba mkabomoe, mali ya wananchi irudi mikononi mwa wananchi na hayo yalikuwa ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Waziri (Lukuvi) aliyekuja hapa kusimamia haki hiyo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. John Magufuli," alisisitiza.

Kumbukumbu zilizopo kwenye majalada zinaonyesha kwamba shamba hilo lenye mgogoro kati ya watu 48 na wanakijiji wa vijiji vinne, linatambulika kama Shamba la Fofo/Foo lenye namba 240 & 242 lenye hati namba NP 405 EP LOT 661 likiwa na ukubwa wa ekari 46.6

Kabla ya kuzuka kwa mgogoro huo, mmiliki wa awali, Dk. Athony Phones, alikopa Sh. 120,000 katika benki iliyojulikana The Land Bank of Tanganyika au National Development Credit Agency, Oktoba 18, 1961 na kuweka rehani shamba hilo.

Hata hivyo, inaelezwa kwamba Dk. Phones aliondoka nchini akiwa anadaiwa deni hilo na hivyo shamba hilo kuuzwa na benki kufidia mkopo huo.

Mwaka 1977, Chama cha Ushirika cha Narumu (kilichoundwa na vijiji vya Urori, Mulama, Usari na Tella) kilishinda zabuni hiyo na kutakiwa kulipa deni hilo.

Aidha, taarifa iliyotolewa katika mkutano wa hadhara na Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Hai, Jacob Muhumba, inaeleza kuwa chanzo cha mgogoro huo ni madai ya watu 48 kutaka kukabidhiwa Shamba la Fofo na benki, jambo ambalo lilipingwa na wanachama wa Chama cha Ushirika Narumu/Manushi.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Jackson Sipitieck, akipewa zawadi ya maziwa na mwanachama wa kikundi cha Sidai juzi, katikati ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Zephania Chaula. **PICHA: GIFT THADEY**

# Matukio ujauzito Hai yapungua

**Na Godfrey Mushi,** HAI

DAWATI la Polisi linaloshughulikia jinsia na masuala ya ukatili katika Wilaya ya Hai, limeeleza kuridhishwa kwake na kupungua kwa matukio ya wanafunzi kupewa ujauzito na madereva bobaboda na bajaj, kushuka kutoka matukio matano hadi kufikia moja.

Kupungua kwa matukio hayo, kunatokana na ushirikiano unaoonyeshwa na madereva hao kwa kufichua wale wanaowakodi wakijihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe jana, Mwenyekiti wa dawati hilo Wilaya ya Hai, Happyness Eliufoo, alisema awali kati ya matukio matano ya mimba za utotoni yaliyokuwa yakiripotiwa, matatu yalikuwa yanahusisha waendesha bodaboda.

"Jeshi la Polisi kupitia dawati la jinsia na watoto Wilaya ya Hai, kwa kweli tunaridhishwa na ushirikiano unaotolewa na madereva wa pikipiki maarufu kama bodaboda na bajaj katika kudhibiti ngono na mimba za utotoni. Sasa wameamua kuwa walinzi wa wanafunzi," alisema.

Tangu kuanza kwa usafiri huo nchini, waendesha bodaboda na bajaj wamekuwa wakituhumiwa kuwa kati ya makundi yanayochangia tatizo la mimba shuleni. Mwenyekiti wa Shirika la Wasaidizi wa Kisheria wa Wilaya ya Hai, Godfrey Mushi, alisema wakati mwingine si kwamba madereva hao wanataka au wanakusudia kufanya hivyo, isipokuwa wanakutana na vishawishi kutoka kwa wanafunzi jambo ambalo huwawia vigumu kuepuka.

"Wengi tunazungumza nao na kuwapa elimu na wanatumbia kwamba wanalaumiwa, lakini yako mazingira yanayowasababishia japo ni kweli kwamba wao ndio wana makosa," alisema Mushi.

Mmoja wa madereva wa bodaboda, Said Juma, alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo kuelekezwa katika kundi hilo, alisema ni rahisi kwao kuwarubuni wanafunzi wa kike, kwa sababu ya aina ya usafiri wanaoutumia.

"Kazi hii inahusisha kuchukua namba za simu za abiria, kuwapakia wanafunzi mpaka shule wanazosoma. Ni rahisi kwa dereva asiyetambua thamani ya mtoto wa kike kumrubuni," alisema.

## Mauzo ya kahawa yaingiza mabilioni

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BODI ya Kahawa Tanzania (TCB) imeuza tani 68,000 za zao hilo na kuingiza pato la taifa Dola 123,185,587 za Kimarekani kwa mwaka 2018/2019.

Gunia moja la kahawa yenye uzito wa kilo 50 limeuzwa kwa dola 110 kwa kahawa yenye ubora wa hali ya juu na msimu 2019/2020 TCB imeuza tani 20,000 za kahawa bora katika mnada wa ndani na soko la nje moja kwa moja.

Mkurugenzi wa Ubora na Uhamasishaji Kahawa wa TCB, Frank Nyarusi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusu maandalizi Siku ya Kahawa Duniani inayofanyika Oktoba Mosi kila mwaka. Alisema msimu huu wanatarajia kukusanya tani 50,000.

Alisema unywaji wa kahawa nchini umefikia asilimia nane kutoka asilimia nne na asilimia 92 inakwenda nje ya nchi na kwamba jitihada za makusudi zinahitajika kukuza matumizi ya unywaji wa kahawa hapa nchini ili kuimarisha soko la kahawa.

Alitaja faida za unywaji wa kahawa kuwa ni pamoja na kuimarisha afya, kiburudisho, kuchangamsha, kufikiri kwa haraka na kufanya uamuzi sahihi na kusaidia kuimarisha kumbukumbu.

Mkurugenzi huyo alitaja sababu nyingine ni pamoja na kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa ya gauti na tezi dume, kushambuliwa kwa figo, msongo wa mawazo, kansa ya ini na utumbo mpana.

Kwa mujibu wa Nyarusi, bei ya soko la kahawa msimu uliopita haikuwa zuri kwa wakulima kutokana na nchi mbali mbali ulimwenguni ikiwamo Vietnam kulima kahawa nyingi na hivyo kufurika katika soko la dunia.

Nyarusi alisema bodi imepata masoko mapya ya zao hilo India, China, Korea, Algeria, Afrika Kusini na nchi mbalimbali za Afrika yakiwamo mataifa ya kiarabu.

Alitoa wito kwa Shirika la Viwanda Vidogo (Sido) na Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi (Veta) kubuni na kutengeneza mashine ya kuandaa kinywaji cha kahawa papo hapo (instant Coffee) kwa matumizi ya nyumbani, hoteli na migahawa.

Alisema kutokana na jitihada za Rais John Magufuli katika kuimarisha zao la kahawa nchini, kumekuwapo na ongezeko la viwanda vya kuongeza thamani ya zao la kahawa.

Nyarusi alisema viwanda vimeongezeka kutoka 18 hadi 31 mwaka huu, vikiwamo viwanda viwili vikubwa vinavyotengeneza kahawa iliyo tayari kwa wanywaji.

Alisema viwanda vya kukobowa kahawa na kuongeza thamani ya zao la kahawa vimeongezeka hadi kufikia 26, wakati viwanda vya kuchakata kahawa kuanzia shambani vikiwa vimefikia 487.



## Ulega alipotinga Longido kukabili ufisadi sugu 'dili' uvushaji mifugo

Ukurasa 18


# BUFE

Ijumaa Septemba 20, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Stendi mpya ilivyobeba kilio cha abiria mjini Nachingwea

Ukurasa 16



HUSSEIN MSACKY

## Mwenye ulemavu alipelekwa shule mgongoni mwa mama, leo anamiliki kampuni ya ujenzi

Ukurasa 14

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

HUSSEIN MSACKY

# Mwenye ulemavu alipelekw mwa mama, leo anamiliki ka

- Achukia kupitiliza unyanyapaa kwao
- Akumbuka mateso alipothubutu ajira
- Kiu yake awe kileleni awainue wenzake

**Na James Lanka, MOSHI**

ELIMU, ajira na ujasiriamali kwa wenye ulemavu ni mambo ya msingi ya maisha ambayo yamekuwa yakipuuzwa na wazazi, jamii na serikali kwa ujumla, hivyo kuwaacha katika 'kiza kinene.'

Moja ya vikwazo hivyo, ni huduma sahihi za miundombinu kutokana na mahali waliko.

Pia familia zinazoamini ulemavu ama ni laana au mkosi, jambo linaloacha baadhi ya wanafamilia wenye mawazo duni, wanawaficha watoto wao.

Hilo likirejeshwa katika historia ya uvumilivu hadi mafanikio ya kijana mjasiriamali msomi ngazi ya shahada, Hussein Msacky, ambaye ni mlemavu wa miguu, hali ni tofauti, kwani amepiga vita hayo kwa vitendo na kuvuka vikwazo mbalimbali vizito vilivyomsibu katika safari ya hali yake.

**AIBUKIA NGO**

Mafanikio ya safari yake tangu elimu ya msingi hadi sekonbari, leo hii anamiliki kampuni ya ujenzi, sambamba na kujaribu kuwanyanyua wanaofanana naye, akianzisha asasi isiyo ya kiserikali iitwayo Miembeni Action and Passion for People with Disability.

Anasema, lengo la asasi hiyo ni kuwasaidia wenye ulemavu katika nyanja mbalimbali za kijamii, kichumi na hata kisiasa.

Msacky, ameiambia Nipashe katika mazungumzo maalumu mjini hapa, kuwa asasi hiyo inatarajia kutoa elimu endelevu kwa familia zenye watu walemavu mkoani Kilimanjaro, waondokana na unyanyapaa, pia ukiukwaji wa haki zao.

Msacky anasema unyanyasaji kwa wenye ulamavu ni wa asilimia kubwa na huanzia kwenye ngazi ya familia, hivyo kupitia asasi tajwa wameamua kujikita katika utoaji elimu maalumu ya haki zao.

Anasema, walemavu wanapaswa kupewa nafasi mbalimbali katika kizazi kilichopo, kwani 'wanaweza ikiwa watawezeshwa' na siyo kufichwa majumbani.

"Uchunguzi uliofanywa na asasi yetu tumegundua kuwa, unyanyasaji mwingi kwa watu wenye ulemavu kama kufichwa kwa kufungiwa ndani ya nyumba, huanzia majumbani mwao," anafafanua Msacky.

Mkurugenzi huyo anasema, binafsi amepitia changamoto mbalimbali tangu masomoni, shule za msingi hadi chuo kikuu, hata kufikia hatua ya kumiliki kampuni sasa, akiamini ulemavu siyo sababu ya kuwaficha au kuwanyanyapaa.

"Tutaanza kutoa mafunzo hayo kwa familia, baada ya hapo tutahamia kwa watu wenye ulemavu wa namna tofauti na kisha jamii yenyewe kwa ujumla, ili waweze kuzielewa na kuzitambua vyema haki za watu wenye ulemavu," anafafanua malengo yao.

Anaendelea kwamba, mazingira aliyopitia, anaamini wapo watu wengi wenye ulemavu kama wake ambao wakitunzwa vizuri, wana mchango mkubwa katika jamii zao.

Rai ya Msacky kwa wazazi na walezi ni kwamba, wasiwafiche watoto wenye ulemavu na badala yake



Mkurugenzi wa Kampuni ya Ujenzi ya Mchamchaka Construction na mwanzilishi wa asasi ya kusaidia watu wenye ulemavu ya Miembeni Action and Passion for People with Disability, Hussein Msacky, mwenye ulemavu wa viungo akiwa 'saiti' na mafundi wake.



> **"Tutaanza kutoa mafunzo hayo kwa familia, baada ya hapo tutahamia kwa watu wenye ulemavu wa namna tofauti na kisha jamii yenyewe kwa ujumla, ili waweze kuzielewa na kuzitambua vyema haki za watu wenye ulemavu," anafafanua malengo yao.**

wapelekwe shuleni kama walivyo watoto wengine wasio na ulemavu, kwani nao wana haki ya kupata elimu.

Anafafanua kwamba serikali imeweka mpango mzuri wa kuwapa kipaumbele watoto wenye ulemavu, hivyo ni jukumu la mzazi kuhakikisha mtoto mlemavu anapata elimu sawa na wengine.

**MAPAMBANO YAKE**

Akielezea alivyoweza kupiga hatua, licha ya ulemavu wa viungo, mwanaharakati huyo wa haki za walemavu wenzake, anatembea kwa kutumia kiti cha magurudumu mawili, anasema amepitia historia yenye changamoto lukuki, kutokana na ulemavu wake.

Hiyo ni katika safari ya maisha tangu kuisaka elimu shuleni hadi chuo kikuu, kusaka ujuzi na hatimaye kujiajiri na kuajiri vijana wengine ndani na nje ya Manispaa ya Moshi, kupitia kampuni yake ya ujenzi.

> **"Uchunguzi uliofanywa na asasi yetu tumegundua kuwa, unyanyasaji mwingi kwa watu wenye ulemavu kama kufichwa kwa kufungiwa ndani ya nyumba, huanzia majumbani mwao," anafafanua Msacky.**

Msacky anaiambia Nipashe kuwa, alikotoka na alikofikia, pia anakoenda ni kwamba, amefungua kampuni akishirikiana na ndugu zake, baada ya kukabiliana na changamoto akitaja mtazamo wa kumbagua kwa sababu ya ulemavu wake ulitawala huko nyuma.

"Kama unavyojua, watu wenye ulemavu tunaonekana kama mzigo katika jamii na hata mimi nakumbuka baada ya kumaliza masomo yangu ya uhasibu katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), jijini Dar-es-Salaam mwaka 2011. Nilisota sana pasipo kupata ajira kutokana na hali yangu ya ulemavu," anasimulia Msacky.

Mwekezaji huyo msomi wa biashara, anakumbuka mwishoni

# …a shule mgongoni …ampuni ya ujenzi

mwa mwaka huo alipata kazi katika kampuni moja jijini Dar-es-Salaam, katika nafasi ya uhasibu, hali iliyomfanya alazimike kumwajiri mtu wa kumsukuma kwenye kiti.

Anasema, hiyo ilikuwa safari kutoka nyumbani hadi kazini na kumpandisha na kumshusha ghorofani, kutokana na miundombinu ambayo haikuwa rafiki kwake katika ofisi zao.

"Kutokana na hali hiyo kulazimika kutumia fedha kidogo nilizokuwa nazipata kumlipa mtu wa kunipeleka na kunirudisha kutoka kazini, niliacha kazi katika kampuni hiyo na kurudi nyumbani Moshi.

"Niliajiriwa kama mhasibu msaidizi katika kampuni moja ya utalii, ambako huko nilikabiliana na changamoto nyingi za kimiundombinu, kutokana na aina ya ulemavu wangu na sikujali hilo, ila changamoto nyingine kubwa iliyonikera sana ni unyanyapaa," anasema Msacky.



Hussein Msacky, akizungumza ofisini kwake. **PICHA ZOTE: JAMES LANKA.**

Anaendelea kufafanua kwamba, alipambana huku akielekeza imani yake katika msaada wa Muumba na ndipo alipopata wazo la kujiajiri, kwa kushirikiana na ndugu yake ambaye kitaaluma nia mhandisi ujenzi, wakaanzisha kampuni iliyopo sasa.

Anarejea masomo yake katika Shule ya Msingi Mawenzi, katika Manispaa ya Moshi mwaka 1995, alipohitimu CBE mwaka 2011, mama yake mzazi alimtia moyo. Hapo anakumbuka namna alivyobebwa mgongoni, alipokuwa katika Shule ya Msingi Mawenzi, mjini Moshi.

Msacky anasema, ni changamoto itokanayo na kukosekana fedha za kumnunulia kiti cha magurudumu matatu, maalum kwa walemavu.

"Kutokana na kukabiliana na changamoto za kimiundombinu tangu nikiwa mdogo, kwa sasa sijali tena changamoto hizo. Kikubwa napambana nacho ni suala la 'unyanyapaa' kwa watu wenye ulemavu.

"Sipendi kabisa watu wanaotunyanyapaa, na ndoto yangu tangu nikiwa mdogo ni kuwa kiongozi mkubwa, ili niweze kuwatetea watu wenye ulemavu Tanzania na ulimwenguni kote," anasema.

Pia anawashukuru wadau wote wanaoshirikiana naye kwa kumpa kazi mbalimbali tangu alipoianzisha mwaka 2017 na jambo linalomsaidia yeye kutoa motisha kwa wengine wenye ulemavu kwamba wanaweza.

Msacky anafafanua kuwa, anakusudia kuanzisha taasisi ya kuwawezesha wenye ulemavu kupata vifaa vya kutendea kazi.

**JICHO LA UONGOZI**

Kuhusu fursa ya uongozi, Msacky anatoa wito kwa serikali kuwapa nafasi watu wa aina hiyo kwa ngazi mbalimbali hata bungeni, ili kutoa uwakilishi hai unaowahusu, kwani anaamini wanaweza kama ilivyo kwake.

"Nachukia sana tabia ya baadhi ya watu kuwanyanyapaa watu wenye ulemavu, kwani ulemavu siyo ugonjwa na mtu yeyote anaweza kupata ulemavu hata ajali. Ni vizuri serikali ikatoa nafasi nyingi zaidi kwa watu wenye ulemavu ili waweze kuwasemea wenzao matatizo yao," anasisitiza.

Katika historia yake, alishawahi kugombea nafasi ya udiwani, lakini hakufanikiwa mwaka 2015 na anatoa wito kwa walemavu popote walipo, wajitume kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

***• Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa anwani ya baruapepe: jlanka6@gmail.com na simu: (+255) 0752 691 129***



Kimberley Wadsworth. **PICHA: MTANDAO.**

# Ajiua kisa kamari imemlia mil. 103/-

## • Atafuna urithi, mama hana makazi

**Mwandishi Wetu**

MWANAMKE kijana raia wa Uingereza, amefariki baada ya kucheza kamari iliyommalizia fedha zote, paundi 36,000 ambayo ni sawa na dola 45,000 au Sh. milioni 103 na laki tano.

Katika matumizi hayo, paundi 17,000 ilikuwa kutoka urithi wa bibi yake.

Kimberley Wadsworth, mwenye umri wa miaka 32 alimwomba mama yake fedha za kulipa madeni katika mchezo huo, hali iliyomwacha mama yake bila sehemu ya kuishi.

Alianza kucheza kamari katika sehemu za starehe na kwenye mitandao mnamo mwaka 2015, alipopata sonona, baada ya kifo cha baba yake na kuwa na ndoa isiyokuwa na furaha.

Mtoto huyo alijaribu kumficha mama yake mwenye umri wa miaka 65 juu ya hali yake hiyo na ikashindikana.

"Hakulipa deni hata moja, bali aliendelea kucheza kwa muda wa wiki mbili mfululizo hivyo nikabaki bila mahali pa kuishi," anaeleza mama yake ambaye alipotambua tatizo hilo, alijaribu kumtafutia mtaalamu wa afya ya akili amsaidie, lakini hakwenda.

Badala yake alimwandikia ujumbe mama, 'tumechelewa sana mama' kabla hajajiua.

Nchini humo, kunaelezwa tatizo hilo ni kubwa sana hata kuhatarisha maisha ya wengi kudhamiria kujiua, huku takwimu ikitajwa kuwa wapo wapatao 340,000 wenye tatizo kubwa la uraibu wa kamari.

Hivi sasa kuna vituo kadhaa vya afya vimeanzishwa nchini humo, ili kuwasaidia watu walioathirika na tatizo la kamari.

Inaelezwa 'ulevi' wa kamari huongezeka kadri mtu anapozidi kupata fedha nyingi, kwani kuna simulizi nyingine ya kijana aitwaye Chris Murphy, alianza kupata hali hiyo alipopata paundi 350 akiwa na umri wa miaka 17.

Tangu wakati huo mpaka alipofika miaka 23, alishatumia zaidi ya paundi 100,000 katika kamari, huku afya yake ya akili haikuwa salama.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, jambo la muhimu katika kukabili hayo, ni kumtaka mtu mwenyewe kupambana kuacha mchezo huo wa kamari, anaodhani hawezi kuuacha na hakuna ubaya kwa mtu kukubali kuwa anahitaji msaada.

Inaelezwa, huenda mtu kuacha kucheza kamari ni jambo gumu zaidi ya mtu kuamua kuacha dawa za kulevya au pombe.

Inatahadhariswa, kamari inaweza kumfanya mtu afilisike, kupoteza uhusiano mzuri na wapendwa wake, kupoteza ajira na kupata msongo wa mawazo.

UCHUMI

MAENDELEO 'KUCHEELE'

# Stendi mpya ilivyobeba kilio cha abiria mjini Nachingwea

## DC:Vumilieni, miundombinu kote Mabasi 60, taa kote, vibanda 50 vyaja

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa NACHINGWEA**

***IJUMAA wiki iliyopita jarida hili lilikuwa na makala mbili, kati ya nne ambazo zimeshachapishwa kuhusu maendeleo ya wilaya, zikipata ufafanuzi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya Rukia Muwango, anayesaidiwa na kiongozi wake, Mkuu wa Mkoa, Godfrey Zambi. Ifuatayo ni makala ya mwisho, inayoeleza maendeleo ya ujenzi wa stendi mpya iliyoko nje ya mji.***

KWA aliyefika stendi ya mjini wa Nachingwea mkoani Lindi, kabla ya Agosti 10 mwaka huu, mtu akihoji kulikoni kuhusu uhalisia wa stendi ya mji huo, basi jibu ni dogo sana kwamba ni maarufu, tena hapafikii hata ukubwa wa nusu uwanja wa mpira, kila mahali pamejaa vumbi tupu.

Mahali hapo ndiko 'siku nenda rudi' pamedumu pakibeba umaarufu wa sifa ya stendi kuu ya mji huo mkongwe wenye mambo mengi ya kihistoria, katikati ya mji. Hiyo ni Nachingwea kongwe ambayo 'kipenga pyeee' cha kupatikana Uhuru wa Tanganyika, mnamo Desemba 9 mwaka 1961, mahali hapo palishakuwa wilaya.

Leo ikiwa zaidi ya mwezi mmoja, maisha na tafsiri ya stendi hiyo siyo moja pakoje? Nikiwa miongoni mwa abiria waliozoea kushuka kwenye stendi hiyo, lakini niliangukiwa na butwaa Agosti 30 mwaka huu, hapakuwa hivyo.

Nilipatwa na mshangao baada ya kuwasili mjini Nachingwea nikiwa na mtazamo basi litafikia stendi ya zamani, kumbe siko. Lilipitiliza stendi hiyo kongwe, kuelekea nje ya mji kwenye stendi mpya. Ni hali iliyonifanya nijidadisi 'kichwani' kwanini tupitilizwe?

Baada ya mwendo wa umbali fulani, nikaambiwa ndiko kwenye stendi mpya. Huko niliukuta uwanja mkubwa wa vumbi la wastani na kwa jicho la haraka, ukubwa wake ni wastani wa viwanja vitano vya mpira. Ni mahali penye mabasi kadhaa na bodaboda.

Nikasikia malalamiko ma minong'ona kutoka kwa baadhi ya abiria wenzangu kuhusu hatua ya kupitilizwa mjini hadi stendi hiyo mpya, kwamba 'watarudije huko' na nilipodadisi kwa kutumia uwanahabari, nilibaini mabasi yameelezwa kushusha abiria eneo hilo kisha yanarudi kulala stendi ya zamani.

Hiyo ndiyo Nachingwea mpya inayoandaliwa katika mpango mji wa Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango, ambaye Nipashe, ilichukua hatua kumhoji kulikoni?

**DC AFAFANUA**

"Maendeleo yana changamoto zake, hivyo abiria na Wanachingwea kwa ujumla hawana budi kuvumilia hali hii wakati serikali ikiendelea kuboresha huduma za usafiri," anasema Rukia.

Anakiri kupokea malalamiko ya umbali wa stendi kutoka kwa watu mbalimbali, lakini hawezi kukubali abiria washushwe kwingineko. Anawasihi wakazi wakubaliane na uhalisia kwa ajili ya maendeleo yao, vinginevyo ni kurudisha nyuma juhudi za viongozi wao.

"Tukisema abiria washuke stendi ya zamani au katikati ya mji, maana yake ni kuruhusu watu kutoizoea stendi mpya. Tumeamua wote washuke kule stendi mpya na kisha kila mmoja aende na njia zake," anasema.

Mkuu wa Wilaya huyo anasema, mji wa Nachingwea unazidi kukua na ndio sababu ya kujenga stendi mpya pembeni mwa mji, akiwa na uhakika itazoeleka, pindi itakapokuwa na huduma zote za msingi.

"Bado ni mapema mno, ndio maana baadhi ya abiria wanalalamika, lakini nina uhakika watazoea tu, kwani maeneo mengi hapa nchini stendi zimejengwa nje ya miji ili kupisha shughuli nyingine za maendeleo," anasema.

> **"Tukisema abiria washuke stendi ya zamani au katikati ya mji, maana yake ni kuruhusu watu kutoizoea stendi mpya. Tumeamua wote washuke kule stendi mpya na kisha kila mmoja aende na njia zake," anasema.**



Stendi mpya ya mjini Nachingwea na mandhari yake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**




Baadhi ya mabasi yanayoenda safari fupi yakiwa katika stendi mpya.

Anasema mwanzoni baadhi ya abiria na wasafishaji walikuwa wanatishia kuandamana kususia kutumia stendi mpya kwa sababu ya kutokamilishwa miundombinu, ikiwamo sehemu ya kupumzikia abiria.

"Sasa jengo la kupumzikia abiria lipo na serikali inaendelea kuboresha stendi hiyo kila inavyowezekana, ili kuhakikisha inakamilika yote na nirudie kuwataka abiria kuwa wavumilivu," anasema.

**ABIRIA WALALAMA**

Kuna malalamiko ya abiria wanapodai kushushwa mbali na wanalazimika kutumia usafiri wa bodaboda kurudi katikati ya mji, hali inayowaongezea gharama zisizo za lazima.

Agosti 30 mwaka huu, Nipashe ilishuhudia namna madereva wa bodaboda wakichangamkia abiria kuwatoza nauli ya Sh. 3,000 na Sh. 5,000 kwa kila abiria. "Kwanini wamehamisha stendi kutoka mjini, halafu haturuhusiwi kushuka njiani. Tunaletwa huku na kulipa nauli nyingine ya usafiri wa bobaboda," analalamika msafiri anayejitambulisha kwa jina, Somoe Juma.

Pia Shaban Mrope, analalamika sababu ya kutokuwapo mbadala wa mabasi yangefika stendi mpya kisha yarudi na abiria wanaoshukia mjini, kuliko kuwaacha huko.

"Tunashushwa huku, halafu basi linarudi tupu mjini kwenda kulazwa kwenye stendi ya zamani ambayo hatutakiwi kushuka hapo...tunaongezewa gharama," analalamika.

Katika sura nyingine, madereva wa bodaboda wako kinyume wakifurahia kuwa 'kipindi cha mavuno' hasa kutokana na ukweli kwamba anayeshuka stendi hiyo analazimika kutafuta usafiri wa kumrudisha mjini.

Usafiri unaopatikana stendi hiyo ni wa bodaboda na mmoja wa madereva ambaye alimbeba mwandishi, Juma Hamis anasema nauli wanayotoza ni halali kutokana na eneo ilipo stendi hadi mjini.

Madereva hao wanasema hali hiyo kwao ni fursa kwa vile wanaingiza kipato kikubwa kwa kusafirisha abiria kutoka mjini hadi stendi hiyo mpya au kuwatoa stendi mpya kwenda mjini kwa Sh. 3,000 hadi Sh. 5,000.

"Siku za nyuma anaweza kushinda kutwa nzima na kuambulia fedha kidogo, lakini kwa sasa angalau tunaingiza kingi, kwani abiria wanaoshuka hapa stendi ni lazima wachukue usafiri wa bodaboda," anasema Hamis.

**MHANDISI AFAFANUA**

Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, Khalifa Kimbendera, anaeleza stendi husika ilianza kujengwa mwaka 2009 na kutumika mwaka 2013, lakini kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wao, waliifunga.

Anasema, stendi ilifunguliwa upya Agosti 10 mwaka huu, ingawa miundombinu yote bado haijakamilika, lakini ana uhakika baadaye kila kitu kitakuwa sawa, kwa vile kazi ya uboreshaji bado inaendelea.

Mhandisi huyo anataja sababu ya kuhama kutoka mjini, ni kwamba stendi ya zamani ilikuwa ndogo na sasa hakuwa na uwezo wa kuchukua mabasi mengi, hivyo wakaona ni bora ianze kutumika mpya huku maboresho ya sasa yakiendelea.

"Stendi mpya ina uwezo wa kuchukua mabasi zaidi ya 60 itakapokamilika na itakuwa imezungukwa na vibanda vya biashara na huduma zote za muhimu kuanzia chakula, nyumba za wageni," anasema Mhandisi Kimbendera.

Anataja huduma nyingine kuwa ni za fedha, choo na anafafanua kuwa halmashauri itajenga vibanda 50 vya biashara vitakavyokodishwa, ili fedha kwamba zitakazopatikana ziweze kuhudumia stendi hiyo.

"Halmashauri tutajenga idadi hiyo ya vibanda na 26 vitakamilika, hivi karibuni na pia tutagawa maeneo kwa wafanyabiashara ili nao wajenge vya kwao na tumeshapokea maombi ya watu 60," anasema.

Mhandisi Kimbendera anasema, stendi hiyo itakapokamilika itakuwa ya kisasa na mfano kwa mikoa ya Kusini, akiwataka abiria na wengine kukubaliana na hali ilivyo kwa sasa.

Anasema, mipango yao inalenga kukamilishwa ndani ya miaka mitatu, pia kutegemea mapato ya halmashauri kama imefanikiwa kukusanya fedha za kutosha kupitia vyanzo vyake vya mapato.

"Stendi itafungwa taa za usalama kila kona na kutakuwa na huduma ya maji na nyingine zote za msingi na itachangamka tu, ingawa kwa sasa baadhi ya watu wanaiona kama haifai," anasema.

# BIASHARA KATIKA PICHA



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Mlozi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa programu mpya ya kozi ya uratibu wa matukio ambayo itaanza mwaka huu. Wengine ni Mkurugenzi wa Fedha na Utawala, Bonface Mwaipaja (kushoto) na Mkurugenzi wa Mafunzo na Kazi za Kitaaluma, Stephen Madenge. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Meneja Uhusiano wa Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, wakati kampuni ya Airtel Tanzania ikitangaza kugawa faida ya jumla ya Sh. bilioni 2.5 kwa wateja na mawakala wake wote wanaotumia huduma ya Airtel Money baada ya kupata kibali kutoka Benki Kuu ya Tanzania(BOT). Airtel imekuwa ikizirudisha kwa wateja wake waliotumia huduma hiyo, kwa kila robo ya mwaka kulingana na kiwango ambacho kipo kwenye akaunti zao za Airtel Money kila siku. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Airtel Money, Isaack Nchunda.




Mkurugenzi wa Biashara na Wateja Wadogo na wa Kati wa Benki ya BancABC, Joyce Malai, akizungumza jijini Dar es Salaam, wakati wa kutangaza kuzindua akaunti ya IZZE ya benki hiyo. Benki ya BancABC imezindua akaunti mpya ya IZZE ambayo ni rahisi kufungua na haina makato yoyote ya mwezi na mteja atapata riba hata akiwa na kianzio cha Sh. 10,000.

BIASHARA

# Ulega alipotinga Longido ufisadi sugu 'dili' uvushaji

- Nao wafunguka tabu kodi mpakani
- Awapa darasa kuzinasa pesa halali
- Kiwanda kipya, sheria EAC mbioni

**Novatus Makunga, aliyekuwa LONGIDO**

KITUO cha Forodha cha Namanga kilichopo katika mpaka ya Tanzania na Kenya, kwa sasa kimeshamiri biashara ya mifugo, hususani ng'ombe.

Lakini, malalamiko makubwa yanayojitokeza hapo ni kuwapo kwa tozo kubwa zinazowafanya wafanyabiashara na wafugaji kutorosha mifugo.

Mpaka huo kwa upande wa Tanzania upo katika Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha na upande wa Kenya, ni kaunti ya Kajiado. Malalamiko ya ushuru wa kuuza nje mifugo iko upande wa Tanzania.

**NAMNA ALIVYOWAIBUKIA**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, katika nyendo za ziara zake alitembelea mpaka huo na akakutana na dai la kero hiyo. Aliyeanza kuliibua ni Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, akifuatiwa na jumuiya ya wafanyabiashara wilayani humo na wafugaji wenyewe.

Hali halisi ya kibiashara ilivyo upande wa Kenya inahitaji mifugo mingi hususani ng'ombe, kwa kuwa kuna kiwanda kikubwa cha kuchakata nyama, eneo la Kajiado. Katika kutafuta ufumbuzi wa kudhibiti kufanyika biashara isiyokuwa na kero, serikali ilijenga soko la kimataifa la mifugo upande wa Tanzania.

Hata hivyo, soko hilo mpaka sasa halijaweza kushika kasi iliyotarajiwa, badala yake kunashuhudiwa vitendo vya kutorosha mifugo, wanaovushwa kupitia kunakojulikana kama njia za panya na kwenda kuuzwa katika nchi jirani, kukwepa ushuru huo unaolalamikiwa kuwa mkubwa.

Kwa mujibu wa maofisa wa mifugo katika Wilaya ya Longido, biashara katika mpaka huo kwa siku ni kati ya ng'ombe 40 hadi 100 na mbuzi kati ya 1000 na 1,500.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Wilaya ya Longido, Saluni Laizer, anaeleza namna kodi kubwa ilivyofanya hata soko hilo la kimataifa la mifugo lililojengwa hivi karibuni, kukosa wanunuzi katika kiwango kinachopaswa kuwapo.

Soko hilo lililopo katika kijiji cha Eworendeke kata ya Kimokuwa, lilijengwa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa gharama ya Sh. milioni 65.

"Mnada huu ulianzishwa kwa lengo la ndugu zetu wa Kenya kuja kila Jumatano na Jumapili kununua ng'ombe na kupeleka kwao, ambako kuna mahitaji makubwa kutokana na kuwa na kiwanda cha kuchakata mifugo," anasema Laizer.

Anasema, kuwapo tozo rafiki kutawashawishi hata wafanyabiashara kutoka nchi jirani, kufuata mifugo na kuinunua katika sehemu rasmi ambayo pia itaiwezesha serikali kuingiza mapato yatokanayo na ushuru.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akizungumza na wafanyabiashara wa mifugo katika Wilaya ya Longido. **PICHA ZOTE: NOVATUS MAKUNGA.**



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mwaisumbe (kushoto) na M Shabbir Virje (kulia).

> "Tunayoyafanya sasa ni mambo ya ajabu sana. Inawezekana vipi mfugaji ukauze ng'ombe wako kwa kukadiria, wakati huyo anayenunua akifika bucha anauza nyama, utumbo na maini kwa kipimo cha kilo, hata ngozi mpaka kwato?" Anahoji Ulega.

**USHURU ULIVYO**

Viwango vya ushuru hivi sasa kwa ajili ya kusafirisha mifugo nje kwa kila kichwa au mfugo mmoja ni Sh. 35,000 kwa ng'ombe, pia mbuzi na kondoo wanatozwa Sh. 9,000 kila mmoja.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Longido, Joseph Sadira, anasema tayari walishawasilisha mapendekezo ya kuomba kupunguzwa viwango hivyo vya ushuru, katika mamlaka zote kuanzia wilayani, mkoa mpaka taifa.

Anasema walipendekeza kwamba tozo ya ushuru kwa ng'ombe uwe Sh. 15,000; mbuzi na kondoo kwa Sh. 4,500 kila mmoja.

Sadira anabainisha kwamba kushusha viwango hivyo vya ushuru, kutawachochea wenyeji wa wilaya hiyo ambao asilimia 90 ni wafugaji kufanyabiashara halali, huku wanunuzi wakiutumia mnada wa kimataifa kupata ng'ombe na mbuzi badala ya kusubiri wapelekwe kupitia 'njia za panya.'

**OPERESHENI ZAGAMBA**

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa muda sasa inaendesha operesheni maalumu ya kudhibiti utoroshaji mifugo inayofahamika kama 'Operesheni Zagamba' inayoelezwa imekuwa na mafanikio makubwa.

Wasimamizi wa wizara hiyo wa 'Operesheni Zagamba' wanaeleza kwamba, katika wilaya hiyo kuna minada ya kawaida ya mifugo tisa, ambazo awali serikali haikutoza kodi, lakini sasa ni tofauti kwani makusanyo yameongezeka kutoka Sh. milioni 6.5 mpaka Sh. milioni tisa kwa siku.

Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, licha ya kukiri kwamba sheria ni msumeno, bado analia na wanaokamatwa wakitoroshwa mifugo wanaishia kutozwa faini anazozieleza ambazo zinasababishia wengi kuwa maskini katika jamii hiyo inaundwa kwa kiwango kikubwa, kabila la Wamasai.

Viwango vya faini kwa anayebainika kukutwa akitorosha mifugo kwa ng'ombe mmoja ni kati ya Sh. 300,000 hadi Sh. 500,000, huku mbuzi na kondoo wakitozwa kati ya Sh. 25,000 na Sh. 30,000.

**DC LONGIDO**

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, anasema ili kuondoa malalamiko, hivi sasa wataanza kutumia Sheria ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), katika kuwashu-

BIASHARA



, alipokuwa katika ziara wilayani Longido akiwa na Mkuu wa Wilaya, Frank
lkurugenzi wa kiwanda cha kuchakata nyama cha Eliya Overseas Food Limited,

# kukabili
# i mifugo

ghulikia wote watakaobainika kutorosha mifugo kwa kuwafikisha mahakamani.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha katika EAC ya mwaka 2004, inaeleleza anayepatikana na hatia ya kutorosha mifugo atakabiliwa na adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano au faini ya asilimia 50 ya thamani ya mifugo yake au adhabu zote mbili.

Naibu Waziri Ulega anatoa wito kwa wafanyabiashara na wafugaji wa Longido pamoja na wilaya ya jirani ya Ngorongoro, kuacha kutorosha mifugo na badala yake watumie taratibu zilizopo, wakati serikali ikishughulikia kilio chao.

**ULEGA ALIVYOWAFUNDA**

Naibu Waziri Ulega, katika hoja yake alienda mbali zaidi akiwataka wafugaji wilayani Longido na nchini kote, kuacha kuuza mifugo, hasa ng'ombe, mbuzi na kondoo kwa kukadiria, badala yake kuingia katika mfumo rasmi wa vipimo vya uzito.

Wenyeji wa Wilaya ya Longido, ambao sehemu kubwa wanaundwa na jamii ya wafugaji wa kabila la Wamasai, uchumi wao kwa zaidi ya asilimia 95 unategemea mifugo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Huduma ya Mifugo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Hezron Nongo hadi mwezi Machi mwaka huu, Longido ina jumla ya ng'ombe 222,909, mbuzi 423,818 na kondoo 322,295.

Pia anasema Longido inapokea mifugo kutoka wilaya ya jirani ya Ng'orongoro, ambayo inaongoza kwa kuwa na mifugo mingi mkoani Arusha, ikiwa na ng'ombe 659,276, mbuzi 791,285 na kondoo 856,646.

Huku akitumia mfano linganishi, Naibu Waziri Ulega anaeleza kama ilivyo kwa wakulima wa mahindi, maharage mchele na mazao mengine ya nafaka, katika mauzo yao hutegemea vipimo maalumu kwa kila gunia kukadiriwa kuwa na uzito wa kilo 100.

"Tunayoyafanya sasa ni mambo ya ajabu sana. Inawezekana vipi mfugaji ukauze ng'ombe wako kwa kukadiria, wakati huyo anayenunua akifika bucha anauza nyama, utumbo na maini kwa kipimo cha kilo, hata ngozi mpaka kwato? " Anahoji Ulega.

Kupitia mazungumzo hayo, Ulega anaziagiza halmashauri zote za wilaya ambazo zinamiliki minada ya awali ya mifugo kuhakikisha zinafunga mizani kwa ajili ya kupimia mifugo, kwani anaeleza minada yote inayomilikiwa na wizara yake nchini tayari ina mizani.

Huku akionekana kutofurahishwa na biashara hiyo ya mifugo kuendeshwa kienyeji, hivyo anasisitiza umuhimu wa kuondoka katika mfumo wa kukadiria bei na kuingia katika vipimo sahihi vya uzito wa ng'ombe.

Inaelezwa, kwamba kutawezesha taifa kuwa na mifugo bora zaidi, sehemu kubwa wanapatikana kwa matunzo mazuri na kutosheleza soko la viwanda vya mifugo, vilivyoanza kujengwa kwa kasi.

Mtaalamu wa mifugo, Elisa Binamungu, anaeleza ili ng'ombe awe na thamani, anapaswa kunenepeshwa na manufaa yake ni kwamba inamwongezea thamani, akitoa mfano wa wastani ng'ombe anayeuzwa kwa bei ya Sh. 300,000 sokoni, anapanda bei kuifikia Sh. 700,000.

Binamungu anafafanua kwamba, gharama za kunenepesha ng'ombe kwa miezi mitatu, huwa ni kati ya Sh. 70,000 hadi Sh. 110,000 kwa kila mmoja na mahitaji anayataja kuwa virutubisho, pumba za mahindi, mashudu, madini na chumvi.

Ulega anaeleza kwamba, hali ya kuwa na mifugo bora itawaongezea uwezo wa mauzo ndani ya soko la ndani, kupitia viwanda vya kuchakata nyama, hatima ya mwisho ni pato kubwa la fedha, tofauti na ilivyo sasa.

**KIWANDA KIPYA**

Hivi sasa kuna kiwanda kinachojengwa wilayani Longido, katika kijiji cha Eworendeke, eneo mkabala na soko la kimataifa la mifugo na taarifa iliyopo ni kwamba, kinatarajiwa kufunguliwa mwezi Oktoba mwaka huu na kiongozi wa juu serikalini.

Ni mradi uliojengwa ukuichukua eneo la ekari 20 na uwezo wake unatarajiwa kuwa wa kuchinja ng'ombe kati ya 500 na 1000 kwa siku, vivyo hivyo mbuzi na kondoo kati ya 2000 na 5000 na asilimia 80 ya mauzo ni kukidhi mahitaji nje ya nchi.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Shabbir Virje, anasema ni mradi unaochukua eneo zaidi ya ekari 300 kwa ajili ya kupumzishia mifugo kabla ya kuchinjwa, unatarajiwa kuajiri zaidi ya watu 300.

Licha ya kiwanda hicho cha Longido, vingine vipo wilayani Mvomero mkoa wa Morogoro na kiwanda kinachotajwa kuwa kikubwa zaidi katika Afrika Mashariki, kilichopo Soga Wilaya ya Bagamoyo, mkoa wa Pwani ambacho matarajio yake kitakamilishwa ujenzi wake, Septemba mwaka huu, kikiwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 14,000 kwa siku.

Viwanda vingine vinaelezwa kuwapo Chato Mkoa wa Geita na Ruvu, mkoani Pwani.

Jitihada hizo za ujenzi wa sasa, zinajitokeza baada ya takribani miaka 26 tangu Tanzania kufungwa kiwanda kikubwa cha nyama cha Tanganyika Packers (TPL), kilichokuwapo Kawe jijini Dar es Salaam, ambacho kilikuwa na uwezo wa kuuza nyama hadi nchi za mbali, ikiwamo soko la Ulaya.

Historia ya kiwanda hicho kilikuwa tanzu kwa Shirika la Uingereza la Kusindika Nyama liitwalo Liebigs Extract of Meat Corporation (LEMCO), ambayo baada ya kutaifishwa mwaka 1974, iliamua kuondoa alama yake ya biashara katika leseni ya soko la kimataifa na kukifanya kiwanda kifungwe mwaka 1993.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mwaka jana Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania inashika nafasi ya pili barani Afrika kwa kuwa na jumla ya ng'ombe milioni 30 na laki tano, nyuma ya Ethiopia yenye ng'ombe milioni 54.

Kwa upande wa Afrika ya Mashariki, Kenya ndio inayoifutia Tanzania kwa kuwa na ng'ombe milioni 18.1; Uganda (milioni 13); Sudan Kusini (milioni 12); Rwanda (milioni 1.4); na Burundi ng'ombe 777,786.



Baadhi ya wafugaji jamii ya kabila la Wamasai, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega (hayupo pichani).**PICHA ZOTE: NOVATUS MAKUNGA.**

UCHUMI

Na Yasmine Protace

## MAGEUZI UCHUMI WA MWANAMKE

# Robo karne ya TGNP na Beijing, Mama Mongella akiwapa mawili ya kihistoria

• Hatua za 'kukokotoa' uongozi nyumbani na ugenini

MWAKA huu ni wa harakati za ukombozi kwa wanawake.

Azimio la Mkakati wa Beijing ukitimiza miaka 25. Ni mpango kazi ulioshtua na kuanza kusukuma harakati za ukombozi kwa wanawake.

Hapo pakashuhudiwa kuanzishwa mashirika mengi nchini ya kijamii kutetea haki za kinamama na watoto. Hapo ndipo penye historia ya kuzaliwa kwa asasi ya utetezi wa haki za kijinsia na watoto - TGNP Mtandao.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Lilian Liundi, anafafanua historia kwamba ilianzishwa mwaka 1993 na mpaka sasa imefikisha miaka 25 au robo karne, katika kumpigania mwanamke na mtoto. Umri rasmi unatimizwa rasmi wiki ijayo.

Anasema, walichoamua katika dhihirisho ambalo katika sura pana linamuinua mwanamke kiuchumi, maandalizi yake ikijumuisha kinamama 1500.

"Tamasha hili litazungumzia masuala ya (mkutano) Beijing (China) ambapo watafanya mikakati ya pamoja na kuona walipo sasa na walikotokea," anasema.

### OFISA PROGRAMU

Anna Sangai ni Ofisa wa Programu na Harakati za Ujenzi wa Nguvu za Pamoja wa TGNP Mtandao, anasema lengo la maadhimisho ni kuhakikisha sera mwongozo uliopo unafuatwa.

Mama huyo anaeleza TGNP Mtandao ilianzishwa na wanachama wachache waliohudhuria mkutano wa Beijing, wakilenga kuwatetea wanawake na haki zao.

"Mwaka 1991 hadi 1995 watu waliratibu safari kwa ajili ya kwenda Beijing," anasema Anna, mwenye taaluma ya ualimu na anafafanua zaidi: "TGNP ilianza na sera moja ya kukusanya taarifa na kusambaza taarifa zinazohusu masuala ya jinsia."

Anarejea mzizi wa historia iliyopo, watu wengi hawakujuwa dhana za jinsia na kuona kama neno linalomuhusu mwanamke pekee.

Kutokana na hilo, anasema idara ya pili ilianzishwa baada ya kuonekana uhitaji wa kufahamika kwa kina masuala ya jinsia, ndipo TGNP Mtandao ikaanza kutoa uelewa kwa makundi mbalimbali, serikali na asasi za kiraia.

Anasema, idara ya tatu ilisaidia ushauri na utetezi, kusukuma mabadiliko ya kutoa ushawishi na utetezi katika sera, baada ya kuonekana mkwamo wake.

"Hamasa imekuwa kubwa na watu wameanza kufahamu na sasa kuna klabu za masuala ya kjinsia katika shule za msingi na sekondari," anasema.

### CHANGAMOTO

Anataja changamoto yao kwamba, wanafanya ushawishi wa kisera na bajeti, lakini utekelezaji unakwama, kwani fedha zinazotengwa kutetea jinsia ni ndogo.

Pia anazungumzia ufuatiliaji duni, wakati wao wanaharakati wahitaji kuwa na kundi kubwa la jamii yenye ufahamu sahihi wa masuala ya jinsia, hali ni kinyume.

Anna anaenda mbali, akitaja mila na desturi katika jamii nayo ni changamoto , kwani inapunguza idadi ya wanawake wasomi, kwani hawapati fursa za kusoma.



Balozi Getrude Mongella akizungumza. **PICHA: MAKTABA.**

### TAMASHA LIKOJE?

Ofisa Habari wa TGNP Mtandao, Monica John, anasema tamasha la jinsia linawakutanisha wanawake wa maeneo mbalimbali na kupaza sauti zao, kuhusiana na maisha ya kinamama.

Anafafanua: "Tamasha ni la 14 kwa mwaka huu kufanyika. Ni kubwa na litakuwa linasherehekea miaka 25 ya TGNP Mtandao, pia kuelimisha jamii kuhusu miaka 25 ya mikakati ya Beijing."

Monica anaeleza malengo yaliyoko ni kutafakari na kupeana taarifa za kujifunza, kuzitambua nyanja mbalimbali na mada kuu ni "Harakati za wanawake zinavyoweza kuleta mabadiliko."

Anasema, mbali na mijadala, washiriki wataleta bidhaa zao, watabadilisha mawazo kupitia bidhaa hizo, kutokana na kuelekea uchumi wa viwanda.

Deo Mushi, ni mdau mwingine kutoka TGNP Mtandao anayesema maazimio 12 yaliyofikiwa jijini Beijing, wameyafikia katika kusaka haki za wanawake.

Kwa mujibu wa Mushi, eneo mojawapo la kisera ni kuwaelimisha wanawake kiuchumi, katika mtazamo wa kumwengua kutoka katika umaskini.

> "Sasa leo watapata simulizi juu ya Beijing, tunaamini kuwa ile simulizi inaleta picha na kujua nini kilichosababisha watu kwenda Beijing. Huu ni mwaka wa 25 kuhusu safari ya Beijing," anasema.

### MAMA MONGELLA

Getrude Mongella, aliyesimamia Mkutano Mkuu wa Wanawake Duniani na mdau mwasisi wa TGNP Mtandao, anadokeza undani uliowafikisha kinamama waliko sasa.

Anasema, kikao cha TGNP Mtandao kinalenga kila atakayejua simulizi ieleweke katika kada tofauti ya vijana, wakiwamo wanafunzi waliopo vyuoni, pia kinababa wengi hawajui vyema historia ya Beijing.

"Sasa leo watapata simulizi juu ya Beijing, tunaamini kuwa ile simulizi inaleta picha na kujua nini kilichosababisha watu kwenda Beijing. Huu ni mwaka wa 25 kuhusu safari ya Beijing," anasema.

Getrude anasema, kinamama wa Kiafrika walipigania haki na usawa katika mapambano yote ya kudai uhuru wa kinamama wa Kiafrika walipambana.

Anasema wamepambana katika kumkomboa mwanamke kwa kuwa walimu wengi ni wanawake, huku akilalamika wamesahaulika kuwekwa katika vitabu vya historia, wakati alichangia kutengeneza historia hiyo.

Kiongozi huyo mstaafu, anasimulia harakati zake za kuwania uongozi, akianza hati ya kugombea uenyekiti wa tawi na akajitosa kugombea nafasi kama hiyo kwa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ngazi ya mkoa na akafanikiwa.

Mama Getrude hafichi upendo wake kwa asasi hiyo ya TGNP akisema alikwea zaidi kufanikiwa kufikia Rais wa Bunge la Afrika Mashariki katika mapambano aliyokumbana na waliombeza kugombea nafasi hiyo.

Anasema, hakukata tamaa na alifanikiwa kutwaa nafasi hiyo na historia ikaenda mbali, hadi kuwa Mkuu wa Mkutano wa Kimataifa wa Nne wa Umoja wa Mataifa, uliofanyika Beijing, China.

Getrude anasema ni kikoa kilicholeta mapendekezo ya uhusiano wa wanadamu; wanaume na wanawake.

Asen Muro ni Mwenyekiti wa TGNP Mtandao, anayemsifu Getrude, kwamba amewainua wanawake wengi katika mapambano yao nchini mwao, barani Afrika.

Kwa mujibu wa Getrude, mapambano yalitokea kwa sababu uhusiano haukuwa sawa na anafafanua: "(mwaka) 1949 Umoja wa Mataifa ulisema wanawake na wanaume wapo sawa, baada ya tamko hilo mwaka 1975 Umoja wa Mataifa ukatangaza Siku ya Wanawake Duniani."

Anasema, katika mkutano uliofanyika nchini Mexico, wa kwanza ulifanyika mwaka 1975 na uliwaleta wanawake na wanaume kuwa kitu kimoja. Ni mkutano ulioongozwa na wanawake katika kudai haki zao.

Anaongeza kuwa mkutano huo ulitoa tamko la kuwapo maazimio 10 kwa wanawake, ikihusisha usawa kwa wanawake waliotajwa kuchangia kuleta maendeleo ya nchi.

Kwa mujibu wa Mama Getrude, mkutano wa pili nchini Denmark, walikubaliana kufuta ubaguzi kwa wanawake wa nchi zote, hasa kupitia elimu, nafasi sawa ya ajira na huduma muhimu kama za afya.

Anasema, mkutano wa tatu ulifanyika jijini Nairobi mwaka 1985 anaokumbuka walisumbuliwa katika kudai haki zao, kwa kuwa wengi walikataliwa haki ya kuhudhuria mkutano huo.

Getrude anamsifu Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kwamba alisisitiza lazima waende ana anaendelea:

"Tuliruhusiwa wanawake wengi kwenda na hapo tulikuja tukiwa na ajenda dhidi ya mapambano."

Anasifu ni mkutano uliosaidia kuwapo siasa na kuwekwa katika sehemu za maamuzi. Baada ya hapo wakaenda na ajenda ya kumlinda mwanamke na walifanya utafiti, wakagundua wasichana wengi wanabaguliwa na familia zao.





# Wakimbia makazi yao kwa kuhofia msako

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

WANANCHI wa Kijiji cha Msesule kilichopo katika Kata ya Mapogolo, Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wanadaiwa kuyakimbia makazi yao kufuatia msako mkali uliokuwa unafanywa na Jeshi la Polisi kijijini hapo, kutokana na wananchi hao kudaiwa kuwacharanga mapanga wakulima wa kikundi cha Mahalala.

Kijiji hicho kwa sasa kimebakiwa na wanawake, watoto na wazee ambao hata hivyo wanadai kuwa hawana utulivu kutokana na misako ya kushtukiza kuendelea kufanyika mara kwa mara na kudai hata shughuli za maendeleo zimesimama.

Wananchi hao waliingia kwenye mapigano na kikundi cha wakulima wa Mahalala kutokana na mgogoro wa kugombea mashamba ya umwagiliaji yenye ukubwa wa ekari 300 uliodumu kwa zaidi ya miaka 25.

Katika mapigano hayo yaliyokuwa ya kutumia silaha za jadi, watu 11 wa kikundi cha Mahalala wanadaiwa kujeruhiwa pamoja na pikipiki tano walizokuwa nazo kuharibiwa na wananchi wa Msesule.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msesule, Adamson Mwasubila kutokana na sekeseke hilo shughuli mbalimbali za maendeleo zimekwama kijijini hapo na wananchi wanatishia kutoshiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba, mwaka huu.

Alisema katika Shule ya Msingi Msesule wananchi walikuwa wanaendelea na ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa pamoja na ofisi ya walimu, lakini kwa sasa wananchi wamegoma kuendelea na ujenzi kutokana na vurugu hizo.

Vilevile alisema walikuwa wanajenga nyumba ya mganga wa zahanati ya kijiji ambayo imefikia hatua ya kuezeka na hakuna kinachoendelea kwa sasa kutokana na nguvu kazi kubwa kukimbia eneo hilo.

"Naiomba serikali itusaidie kumaliza mgogoro huu maana ni wa muda mrefu sana, ulianza tangu mwaka 1993, kila Mkuu wa Wilaya hii amepambana nao imeshindikana, sasa hivi hapa kwetu maduka yote yamefungwa na tunaelekea kwenye msimu wa kilimo," alisema Mwasubila.

Kwa upande wake aliyewahi kuwa Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Peter Kitha, alisema kwa sasa wananchi wote wa kijiji hicho wamekubaliana kutofanya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sababu wamebaini kuwa hawatambuliki kama kijiji.

Alisema mgogoro huo umedumu kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi wa kudumu na kwamba kwa sasa umefikia hatua mbaya kwa kuwa ni mara ya kwanza kupigana tangu ulipoanza.

Alisema mashamba yanayogombaniwa yapo ndani ya ramani za kijiji chao na wao ndio wenye hatimiliki, lakini kikundi cha Mahalala kimekuwa kikishirikiana na wenzao wa mtaa wa Mayota kuwahujumu.

"Wakuu wote waliowahi kuongoza wilaya hii wamehangaika na mgogoro huu, lakini bado mwafaka haupo, tunataka serikali itueleze kama sisi ni kijiji ama ni kitongoji, kwa sasa msimamo wetu ni kutoshiriki uchaguzi wa aina yoyote," alisema Kitha.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema chanzo cha mapigano hayo ni pande zote mbili kupuuzia maagizo yake ya kuzuia shughuli zote kufanyika katika mashamba hayo mpaka mahakama itakapotoa hukumu na kutoa tafsiri ya mmiliki halali.

Alisema kwa sasa ataendelea kutoa elimu pamoja na kuhakikisha amani na utulivu vinakuwapo kwenye maeneo hayo, huku akiwashauri wananchi wa Msesule kusitisha uamuzi wa kutoshiriki uchaguzi kwa madai kuwa watakuwa wanajikomoa wenyewe.

Kuhusu miradi ya maendeleo waliyotelekeza aliwataka kuendelea nayo kwa vile ni kwa ajili ya faida yao wenyewe na wanaosoma katika Shule ya Msingi Msesule ni watoto wao na katika zahanati ya kijiji watatibiwa wao wenyewe.

"Nitafanya ziara katika kijiji hicho kwa ajili ya kutoa elimu, wanatakiwa kushiriki uchaguzi na kuchagua viongozi bora ambao watawasaidia kutatua changamoto zao," alisema Mfune.





Mratibu wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Hope Center for Children, Girl & Women Tanzania (HCCGWT), Salha Ng'amilo (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi (hawapo pichani), kuhusu safari ya vijana sita kuzunguka mikoa 13 kupeleka ujumbe unaohusu afya ya uzazi. Kushoto ni Mkurugenzi Mkazi wa Taasisi ya Engende Health, Prudence Masako na baadhi ya vijana hao, Augustino Julius na Jackline Rwegasira wote kutoka PSI. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Ukarabati daraja lililovunjika waleta matumaini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa vijiji vya Iwala, Idugumbi na Iwanga katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, ambao walikosa mawasiliano baada ya daraja la Mto Nzovwe kuvunjika, wamepata matumaini baada ya ukarabati wa daraja hilo kuanza.

Ukarabati wa daraja hilo ulianza juzi na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), huku Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Orani Njeza ambaye aliambatana na wataalamu hao akiomba likamilike haraka na wananchi waendelee na shughuli zao.

Pia Njeza aliwaomba kukarabati Barabara ya Mbagabe – Wambilo katika kata ya Utengule Usongwe, daraja la Mto Mbalizi lililopo jirani na Machinjio ya nguruwe pamoja na daraja dogo la kuelekea Nsalala.

Alisema miundombinu hiyo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi kwa kuwa inasaidia kusafirisha mazao kutoka mashambani kupeleka sokoni pamoja na kusafirisha pembejeo kwenda mashambani wakati wa kilimo.

Alisema atahakikisha anasimamia ujenzi huo pamoja na kuomba fedha serikalini kwa ajili ya miundombinu mingine ya barabara katika jimbo hilo ambalo ramani yake haijakaa vizuri.

"Madaraja haya ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu hivyo lazima tuwekeze nguvu kubwa kuhakikisha yanakuwa yanapitika katika kipindi chote cha mwaka ili wananchi wasihangaike," alisema Njeza.

Vilevile, alisema serikali ya awamu ya tano imefanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu ya barabara pamoja na huduma zingine ndani ya wilaya hiyo na baadhi inaendelea kuboreshwa.

Alisema baadhi ya huduma za kijamii ambazo miundombinu yake imeboreshwa ni pamoja na vituo vya afya, elimu pamoja na miradi ya maji kwa ajili ya kuwahakikishia wananchi huduma bora.

Alisema baadhi ya miradi inayoendelea kuboreshwa ni pamoja na machinjio ya kisasa ambayo inajengwa katika Kata ya Utengule, Usongwe ambayo alisema ikikamilika itasababisha wananchi wengi wa Mji wa Mbalizi kupata ajira.

# Ashikiliwa tuhuma za kuua kichanga, kujaribu kujiua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWANAMKE mmoja mkazi wa Kijiji cha Nzongwi Juu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa kosa la kumuua mtoto wake mchanga na kujaribu kujiua kwa kunywa sumu ya kuulia wadudu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alimtaja mwanamke huyo kuwa ni Silvia Sande (28) na kwamba alimuua mtoto wake aitwaye Asifiwe Baini, mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi miwili.

Alisema tukio hilo lilitokea Septemba 16, mwaka huu majira ya saa 4:00 asubuhi katika Kijiji cha Nsongwi Juu, kilichopo Kata ya Ijombe na mwanamke huyo akiwa chumbani kwake alikunywa sumu hiyo na nyingine kumnywesha mtoto wake ili wote wafe.

Alisema baada ya majirani kubaini tukio hilo walimkimbiza mwanamke huyo pamoja na mtoto wake katika Kituo cha Afya cha Igawilo, jijini Mbeya kwa ajili ya kuokoa maisha yao, lakini mtoto alifariki wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Kamanda Matei alisema, chanzo cha tukio hilo hakijajulikana na wanaendelea kumshikilia mwanamke huyo kwa ajili ya mahojiano kabla ya kumfikisha mahakamani kujibu shtaka la kumuua mtoto na yeye mwenyewe kutaka kujiua.

"Wakati mwingine inakuwa ni msongo wa mawazo, hasira zinazosababishwa na ugomvi wa wanandoa, sasa yawezekana hasira zake ndio zilimfanya aamue kuchukua hatua hiyo ambayo imegharimu maisha ya mtoto wake," alisema Kamanda Matei.

Aliwashauri wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi ikiwa ni pamoja na kujiua huku akiwataka kuripoti kituo cha polisi endapo mtu anabaini kuwa anakabiliwa na msongo wa mawazo ili asaidiwe kabla hajafanya uamuzi wa kujiua.

Alisema watu wote wenye ugomvi wanatakiwa kutafuta haki kwenye vyombo vinavyotakiwa kutoa haki na kwamba endapo ikitokea mtu mwenye msongo wa mawazo ana hasira akaenda kuomba msaada Jeshi la Polisi anaweza akasaidiwa moja kwa moja ama kushauriwa hatua za kuchukua.

Alisema katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia watu tisa mkoani humo kwa kosa la kufanya biashara ya mafuta aina ya dizeli na petroli bila kuwa na kibali kutoka kwenye mamlaka zinazohusika.

Aliwataja watuhumiwa kuwa ni Majaliwa Edward (30), Hamis Anyimike (32), Edson Kalinga (32), Assa Mwambelo (33), na Kambela Mwaipopo (30), wote wakazi wa jijini Mbeya.

Wengine ni George Mwakalobo maarufu Mwadada (40), Lwitiko Mwaipopo (38) na Jakobo Mwakilelma (47), wote wakazi wa Ipinda wilayani Kyela.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa kwenye msako maalumu ulioendeshwa na Jeshi la Polisi Septemba 17 na watuhumiwa wote walikutwa na lita 1,500 za petroli na 2,500 za dizeli wakiwa wanauza.

Alisema watuhumiwa wote wanaendelea kushikiliwa na jeshi hilo, wakati maandalizi ya kuwafikisha mahakamani yakiendelea huku akiwatahadharisha wananchi kuachana na biashara hiyo kama hawana vibali.





# Mikononi mwa Takukuru kwa tuhuma

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) kuwafikisha haraka mahakamani watendaji wote waliohusika kutengeneza deni feki la Sh. bilioni 70 la mawakala wa usambazaji wa pembejeo za kilimo na ufugaji.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, wakati akijibu hoja za wasambazaji hao alipokuwa akifunga kongamano la nne la kitaifa la wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo na mifugo, jijini hapa.

Alisema madai mengi yanayodaiwa ni feki hivyo Takukuru inapaswa kuwasilisha haraka majina yote yaliyochunguzwa na kubainika yamehusika kwenye udanganyifu huo, ili hatua za sheria na wale watakaobaki ambao ni wasafi watalipwa fedha zao.

"Kumekuwa na udanganyifu mwingi sana kwenye malipo ya mawakala na si nyie tu udanganyifu umeanzia wizarani kwenye kilimo unakuta madai mengi kinachozalishwa ni kidogo," alisema Hasunga.

Aliongeza: "Unakuta madai Sh. bilioni 70 ukiangalia deni linalodaiwa na kilichozalishwa ni tofauti, wizara ilipoona hivyo ilipeleka mtu wa kuhakiki na kukuta asilimia 80 ya madai ni feki na 20 iliyobaki ndio hayo madai nayo bado yanastahili kuchunguzwa," alisema.

Hasunga alisema Takukuru inapaswa kufanya haraka uchunguzi na kuwapeleka mahakamani ili watakaobainika wachukuliwe hatua na wale watakaosalia ambao ni wasafi utaratibu wa malipo yao utashughulikiwa.

Alisema serikali inahitaji kubaki na watu safi ambao watakwenda kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ambazo zitawasaidia kubadilisha kutoka kilimo cha kujikimu na badala yake kuwa kilimo cha faida.

Alisema wakifanya hivyo kwa pamoja anaimani watapiga hatua kubwa kupitia chama hicho cha ushirika cha uuzaji na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima na wafugaji badala ya hasara ambayo wanailalamikia.

Aliwataka mawakala hao kwenda kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora ya pembejeo za kilimo na ufugaji ili kuisaidia jamii hiyo kupata uelewa wa dhana hizo.

Kuhusu malalamiko ya mbegu zisizo na ubora, Waziri Hasunga alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya kuwa mbegu wanazopata sio bora, lakini imebainika inatokana na kutokuwa na uelewa wa jinsi ya kuzitumia wakati wa msimu wa kupanda.

Aliagiza kupanua wigo wa utoaji elimu ya matumizi ya pembejeo kwa wakulima na wafugaji ili kupiga hatua kwenye sekta hizo.



Mtuhumiwa Kitareti Mwita akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika chumba cha Mahakama ya Wilaya ya Dodoma jana, alipofikishwa hapo kwa kosa la kujifanya ofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kujipatia fedha. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# UWT yaelimisha wanawake uchaguzi S/Mitaa

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

JUMUIYA ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), imewataka wanawake kujiepusha na makundi yanayojitokeza ndani ya chama hicho katika kuelekea kampeni za uchaguzi za serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Wito huo ulitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa UWT Taifa, Jesca Mbogo, katika ziara Wilaya ya Chamwino alipokutana na wanawake na makundi ya watu wenye ulemavu.

Alisema wanawake wanatakiwa kijiepusha na makundi hao ambayo mengine yanaweza kusababisha mpasuko ndani ya chama.

Aliwataka kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uongozi kwa kuwa ni haki yao ya kimsingi.

"Ninawaomba nendeni mkagombee kwenye nafasi hizo acheni woga, pia muache kubaguana bali muwe kitu kimoja inapotokea mmoja wenu akigombea mpeni ushirikiano ili aweze kushinda nafasi hiyo," alisema.

Mbogo aliwataka kujiepusha na wagombea wanaowaletea pochi na mikoba ili waweze kuchaguliwa. "Kitendo hiki kinaashiria wameletwa kwa njia ya rushwa na matokeo yake wanaweza kuwatumikisha badala ya kuleta mabadiliko ya maendeleo," alisema.

Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, aliwataka wanawake hao kuhakikisha ushindi unapatikana kwenye kata zote mbili ikizingatiwa kuwa wao kwa umoja walionao wanaweza, tena ni jeshi kubwa.

Alisema kwa nafasi waliyo nayo wanaweza kuhakikisha ushindi unapatikana.

## Jamii yatahadharishwa ugonjwa wa kifafa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JAMII imetakiwa kuacha tabia ya kuwapeleka kwa waganga wa kienyeji wagonjwa wa kifafa kwa kuwa hali hiyo inasababisha kukomaa kwa ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Huduma za Afya ya Akili katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Alphoncina Mahoma, takwimu za ugonjwa huo kwa mwaka 2018, Mkoa wa Dodoma zinaonyesha takribani watu 9,000 waliugua kwa mwaka huo, na kudai kuwa idadi hiyo bado ni ndogo kwa kuwa wengi wanaishia kwa waganga hao.

Alisema idadi hiyo ni ndogo kwa kuwa wagonjwa wengi wamekuwa wakipelekwa kwa waganga wa kienyeji na kusababisha ugonjwa huo kukomaa na kuchukua muda kutibika au kutotibika badala ya kuwapeleka hospitali.

"Unamkuta mtu amehangaika kwa waganga wa kienyeji miaka miwili au mitatu, akiletwa hospitalini tayari ugonjwa umekomaa na akifika hapa tayari amekuwa na shida kubwa sana," alisema.

Aliongeza: "Hii idadi ni ndogo kwa kuwa jamii ya watu wengi wanaishia kwa waganga wa kienyeji na tiba za asili hawaji katika vituo vya kutolea huduma."

Alisema zipo sababu mbalimbali zinazochangia ugonjwa huo ikiwamo mtikisiko wa ubongo ambao unatokana na mtu kuzalia nyumbani na kupatwa na homa kali.

Alibainisha kuwa ugonjwa huo unasababishwa na seli zilizopo katika mishipa ya fahamu kwenye ubongo kutoa umeme mwingi, kwenda kwenye misuli na sehemu zingine za mwili na hivyo kusababisha mtu kuishiwa nguvu, kichwa kuuma, kuchanganyikiwa, mwili kukakamaa na hata kupoteza fahamu.

"Sababu kubwa inayochangia ni mtu kuzalia nyumbani au kumchelewesha mtu amepatwa na homa kali kama degedege, mtu anafikiri ni nguvu za giza au amerogwa anampeleka kwa waganga wa kienyeji badala ya hospitali," alisema.

Alifafanua kuwa dalili za ugonjwa huo zinaweza kutambuliwa na daktari kulingana na historia ya mgonjwa.

"Hata ukipata `stroke' tayari ule ubongo chemchemu za damu zimegusa na kama zimepata mgongano na kusababisha kovu sasa ile hali ndio inayotengeneza na kusababisha shoti, lakini sio kwamba wote wenye stroke wanaweza kupata kifafa," alisema.

Alisisitiza kuwa ugonjwa huo unatibika, lakini kumekuwapo na uelewa mdogo kwa jamii.





## Wizara yaandaa mpango kuhifadhi chakula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imesema kuwa imeandaa mpango maalum wa kuhifadhi chakula cha akiba kwa ajili ya kukabiliana na majanga.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Makame Ussi, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarahan, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuweka chakula cha akiba.

Alisema katika kutekeleza lengo hilo, serikali kwa mara ya kwanza imehifadhi tani 386 za mchele katika ghala lililopo bandarini Malindi mjini Unguja, unaotoka Pakistan.

Alisema mpango huo ni kuhifadhi mchele utaonunuliwa kutoka kwa wakulima, wizara yake hivi sasa inatekeleza mradi wa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji kwa kuoengeza eneo la umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 1,524 ili kuongeza uzalishaji wa mpunga na kupunguza utegemezi.

Alieleza kuwa katika kutekeleza mpango wa hifadhi ya chakula cha akiba, iliamuliwa kwamba maghala yatakayotumika ni ya Malindi lililopo bandarini Unguja na ghala la Tibirinzi, Pemba.

Alisema kwa sasa ghala la Malindi lenye uwezo wa kuhifadhi mchele tani 500, linatumika kuhifadhia mchele tani 386.

Alieleza kwa upande wa Pemba, ghala la Tibirinzi bado halijakarabatiwa ingawaje taratibu zinaendelea.

"Pia wizara imo katika matayarisho ya ujenzi wa maghala mawili ya kuhifadhia mpunga," alisema.

# Muswada kuwaenzi viongozi kitaifa kujadiliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya kusimamia viongozi wakuu wa kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, imesema imetumia weledi katika kujadili na kuchambua muswada wa sheria ya kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa ili kuhakikisha inawasilisha maoni mahiri na yenye kujali uzalendo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Panya Ali Abdalla, alieleza hayo wakati akiwasilisha hotuba ya kamati ya kusimamia viongozi wakuu wa kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu muswada huo na mambo mengine yanayohusiana na hayo, katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Alisema michango iliyotolewa na wadau hao imedhihirisha wazi dhamira ya kuwapenda, kuwajali na kuwaenzi kwa dhati viongozi hao kutokana na mchango wao wa maendeleo yanayopatikana nchini kupitia uongozi wao.

Alisema, lazima viongozi hao wapewe hadhi yakipekee na waendelee kuthaminiwa kwa kile walichokifanya ambacho kimeimarisha maslahi ya taifa.

Alieleza kuwa miongoni mwa mambo ya msingi ambayo wadau waliyoyasisitiza na kuzingatiwa na kamati hiyo, ni pamoja na kuwa na utaratibu mzuri wa kuweka maelezo shaksia (CV) ya viongozi kitaifa ili kuzipata kwa uhakika na kwa usahihi pale zinapohitajika.

Alisema jambo jingine ni kuhakikisha sheria zinazotungwa katika kuwaenzi viongozi hao na zinapewa uzito unaostahiki ili kuthamini michango yao pamoja na wenza wao.

Alieleza kwamba vitu vitakavyowekwa kwenye makumbusho kwa ajili ya kuwaenzi viongozi hao, ni vyema viwe vitu maalumu ambavyo vitakuwa vinamtambulisha na kuonyesha uhalisia na upekee wa kiongozi husika katika kipindi chake.

Katika hatua nyingine alisema ni vyema kuzingatiwa utaratibu wa kushusha bendera nusu mlingoti kwa maombelezo iwapo utatokea msiba wa kiongozi wa juu madarakani hasa ikizingatiwa nafasi wanazozitumikia ni miongoni mwa mihimili mikuu ya nchi.

Mwenyekiti huyo alikiri michango iliyotolewa na wadau hao imesaidia kutoa mwangaza na taswira nzima ya mambo ambayo yanatakiwa kuzingatiwa katika muswada huo, huku akisisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wadau hao katika kamati wakati wanapopitia miswada yenye umuhimu kwa maslahi ya taifa.

"Iiwapo muswaada huu utapitishwa na chombo hiki na kukamilika utaratibu wa kuwa na sheria utasaidia kuondoa changamoto zilizopo," alisema Panya.

Pia alisema kamati hiyo inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na muswada huo pamoja na marekebisho madogo yaliyopendekezwa na kamati wakati ilipokaa na wizara husika kwa nia ya kuimarisha muswada huo.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohammed Abudu Mohamed, akitoa majumuisho alisifu umakini, busara na hekima kubwa zilizochukuliwa na baadhi ya wajumbe wa baraza hilo katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi na tija ndani ya muswada huo. "Yapo baadhi ya mambo yalioshauriwa na wajumbe hao serikali itayafanyia kazi kwa kuzingatia matakwa ya kisheria," alisema.

Mapema, akiwasilisha waraka wa muswada wa kufuta sheria za viongozi wa kitaifa namba 10 ya mwaka 2002 na kutunga sheria ya kuwaenzi viongozi wa kitaifa, alisema umuhimu wa muswada huo unatokana na haja ya kuzitafutia ufumbuzi kasoro mbalimbali za kisheria na kiutendaji zinazojitokeza katika usimamizi wa kuwaenzi viongozi.

Alisema miongoni mwa kasoro hizo ni pamoja na kutokuwapo uwiano wa viongozi wa kitaifa wanaohitaji kuenziwa kati ya wale waliotajwa katika sheria inayopendekezwa kufutwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010.

"Sheria iliyopo sasa kumtambua Waziri Kiongozi kuwa ni Mwenyekiti wa kamati ya mazishi badala ya Makamu wa Pili wa Rais," alifafanua.

Alisema kasoro nyingine ni kutokuwapo kipengele kinachoruhusu ukusanyaji na utunzaji sahihi wa kumbukumbu za kiongozi mkuu wa serikali na viwango vya adhabu kutoendana na ukubwa wa makosa na wakati uliopo.



Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum, Juma Ali Khatib (kushoto), akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nje ya ukumbi wa baraza hilo, Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jamii yatakiwa kuzingatia chanjo kwa watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAMII imetakiwa kuwa tayari kuwapeleka watoto kupatiwa chanjo ya kitaifa dhidi ya maradhi ya surua, rubella na polio ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na maradhi hayo.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Fadhil Mohammed Abdalla, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Wizara ya Afya, mjini hapa.

Alisema jamii ikijitokeza kwa wingi kuwapeleka watoto wao kupatiwa chanjo hiyo, itawakinga na madhara mbalimbali ikiwamo kupoteza baadhi ya viungo na kusababisha ulemavu.

Alieleza kuwa kampeni ya chanjo hiyo itazinduliwa rasmi Septemba 26 hadi 30, mwaka huu huko Kivunge Mkoa wa Kaskazini `A' na itawalenga zaidi ya watoto kuanzia umri wa mwaka mmoja hadi miaka mitano ambao ndio waathirika zaidi wa maradhi hayo.

Naye Mkufunzi wa Kampeni ya Chanjo ya maradhi ya surua, rubella na polio, Fathiya Saidi Bedui, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuzuia na kupambana na maradhi yanayozuilika kwa chanjo.

Alisema dalili za maradhi ya surua na rubella, mtoto kuwa na homa kali kuchuruzika mafua, macho kuwa mekundu na kutokwa machozi, hivyo kinamama wanapoona hali hiyo wafike katika vituo vya afya kwa uchunguzi zaidi.

# Wagonjwa walalamikia watumishi kituo cha afya

**Na Said Hamdani,** KILWA MASOKO

WAKATI serikali ikijitahidi katika kuboresha huduma kwa raia wake, wagonjwa wanaokwenda kutibiwa Kituo cha Afya cha Mji mdogo na Kata ya Masoko, Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, wanalalamikia uduni wa upatikanaji huduma na lugha mbaya kutoka kwa watumishi wa kituo hicho.

Malalamiko hayo yalitolewa na wananchi waishio Kijiji cha Kisangi kwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi) Dk. Doroth Gwajima, alipofanya ziara wilayani humo.

Wakiwasilisha malalamiko yao, Rafa Salum Ally, Fatuma Mohamedi Duka, Alawi Bakari na Fatu Abdallah, walimweleza kuwa miongoni mwa kero wanazozipata upande wa afya ni huduma zisizoridhisha na lugha chafu kutoka kwa baadhi ya watumishi wa kituo hicho.

Pia walisema kutokana na changamoto hizo, wanalazimika kutembea umbali zaidi ya kilomita saba kwenda Kijiji cha Mpara kufuata huduma za matibabu, ikilinganisha na kilomita tano kwenda Masoko kilipo kituo cha afya.

Hata hivyo, waliwapongeza watumishi wa Zahanati ya Mpara kwa huduma nzuri na lugha walizoziita ni za kiungwana kutoka kwa watumishi wake, hali inayowapa faraja wagonjwa wanaokwenda kupata matibabu.

Changamoto zingine zilizotajwa ni watoto wadogo walio na umri chini ya miaka mitano na wagonjwa wanaosumbuliwa na kifua cha pumu kutakiwa kulipia matibabu kinyume cha Sera ya Afya inaelekeza watibiwe bure, madai ambayo yaliungwa mkono na Dk. Gwamaka.

Dk. Gwajima alikiri kupokea malalamiko yanatolewa na wananchi hao, huku akimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kuchukuwa hatua ya kufanya mabadiliko.

"Malalamiko dhidi ya kituo hiki cha Afya Masoko tunayasikia sana, sasa Mkurugenzi nakuagiza wale watumishi walio na muda mrefu wabadilishwe," alisisitiza Dk. Gwajima.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Godfrey Baraza Jafari, akipokea maelekezo hayo kutoka kwa Dk. Gwajima, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wake, aliahidi kulitekeleza haraka.



Maji yakiwa yametuama kwenye moja ya mitaro ya barabara za Mikocheni, jijini Dar es Salaam, juzi, baada ya mtaro kuziba, hali ambayo inaweza kuwa ni mazalia ya mbu na kuhatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakubaliana kusambazia wakulima viuatilifu

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KAMPUNI ya Petrobena inayosambaza pembejeo za kilimo nchini, imeungana na BASF Tanzania Limited kusambaza viuatilifu na dawa zenye ubora kwa wakulima ili kuongeza tija katika uzalishaji mazao.

Kampuni mbili hizo jana zilitiliana saini mjini hapa makubaliano ya kuwa na ushirikiano huo baada ya mafunzo kwa maofisa kilimo wa kampuni ya Petrobena juu ya matumizi bora ya dawa ya kilimo yanayotengenezwa na BASF.

BASF ni kampuni ya kimataifa inayotengeneza viuatilifu na aina nyingine za dawa za kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya makubaliano hayo, Ofisa Mkuu wa Mauzo wa BASF Kanda ya Afrika ya Mashariki, Lincholn Asembo, ameyaeleza makubaliano hayo kuwa ni chachu katika kuboresha uzalishaji mazao nchini Tanzania. "Kampuni ya Petrobena imekuwa ni mdau mkubwa katika kuchagiza mapinduzi ya kilimo Tanzania, hivyo ushirikiano huu utasaidia kuinua uzalishaji na kukuza kipato cha wakulima kupitia kilimo," alisema Asembo. Alisema kilimo Tanzania kimekuwa kikikabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo wadudu waharibifu wa mazao, na kuongeza kuwa viuatilifu kutoka BASF vinalenga kuondoa tatizo hilo.

Alieleza kuwa kampuni ya Petrobena inamtandao mkubwa na uzoefu katika usambazaji wa mbolea, hivyo haitakuwa ngumu kwao kusambaza viuatilifu ambavyo vitamsaidia mkulima kuongeza tija katika shughuli yake ya kilimo. Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Peter Kumalilwa, aliishukuru BASF kwa kukubali kufanyakazi na kampuni yao ili kwa pamoja kushiriki katika kuimarisha mapinduzi ya kilimo nchini.

"Tunafuraha kuanza kufanya kazi na kampuni kubwa ya kimataifa ya BASF yenye kutengeneza viuatilifu vyenye viwango vya hali ya juu ambavyo vikitumiwa vizuri vitakuwa ni mkombozi wa mkulima. Lengo la serikali sasa hivi ni kuinua tija katika kilimo ili wakulima wauze malighali bora kwa viwanda nchini na ziada isafirishwe nje ili kuliingizia taifa fedha ya kigeni," alisema Kumalilwa.

# Waanza kujifungulia vituo vya uzazi salama

**Na Gurian Adolf,** NKASI

BAADHI ya wajumbe wa kikao cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2018 ya mradi wa kukabiliana na mimba za ututoni wilayani Nkasi, wamepongeza hatua iliyo fikiwa ambapo wanawake wilayani humo wamebadilika na kufahamu umuhimu wa kujifungulia katika vituo vya uzazi salama. Akichangia katika kikao cha siku moja cha nusu mwaka cha timu za ulinzi wa mtoto ngazi ya kata na wilaya hiyo, Marietha Mwanisenga alisema hivi sasa wanawake wengi wanahudhuria kliniki kutokana na elimu inayotolewa na mradi huo unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Plan International wilayani humo. Alisema kabla ya mradi huo wanawake wanne kati ya kumi ndio walikuwa wanaona umuhimu wa kuhudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vinavyotoa huduma za uzazi salama, kitendo kilichokuwa kikisababisha kutopungua idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi.

Mwanisenga alisema hivi sasa wanawake zaidi ya asilimia 90 ambako mradi huo unatekelezwa wamebadilika kwa kuwa wamekuwa wakihudhuria kliniki kutokana na elimu iliyotolewa na mradi.

Naye George Kayanda alisema mradi huo umesaidia katika kuleta mabadiliko chanya katika masuala ya uzazi, lakini changamoto kubwa ni mimba za utotoni ambazo zimekuwa zinaonekana kudumaza jitihada za mradi huo.

Naye mratibu wa mradi huo, Nestory Frenk, alisema lengo la kufanyika kwa kikao hicho ni kujitathmini ili kubaini changamoto zilizopo katika kutekeleza mikakati waliyojiwekea ili mradi huo uweze kufanikiwa.

Alisema suala la kuchukua hatua kwa watoto waliopata mimba linahitaji mikakati zaidi kwani licha ya kuwa wao wamekuwa wakiitoa, lakini linahusu zaidi udugu na mahusiano kwa sababu wengi wao wamekuwa wakimalizana nje ya sheria kwa kuzingatia maisha yao ya baadaye.

## Wanawake wawili wabadilishana wanaume

**NAIROBI, Kenya**

WANAWAKE wawili kutoka Jimbo la Busia Magharibi mwa Kenya wamewaacha watu na bumbuwazi baada ya kubadilishana waume zao kwa lengo la kutafuta furaha.

Lilian Weta mwenye umri wa 28, mama wa watoto watatu na Millicent Auma mwenye umri wa miaka 29, mwenye watoto wawili wamezua gumzo katika mtandao nchini Kenya kwa kuonekana kuwa wamefanya jambo la ajabu sana kwa wanandoa hao kuamua kubadilishana wenza.

Wiki moja iliyopita wapenzi hao waliandikishiana serikalini namna watoto watalindwa baada ya wanawake hao kubadilishana waume zao pamoja na watoto.

Wanawake hao wanadai walifikia maamuzi hayo baada ya kusukumwa na ugomvi usioisha katika familia zao.

Vyombo vya habari vya Kenya vilimnukuu Lilian akisema kuwa alifikia uamuzi huo baada ya mume wake kumleta mwanamke mwingine katika nyumba yao mwezi mmoja uliopita.

"Mume wangu alinidanganya kuwa binamu yake kutoka Bungoma anakuja kututembelea hivyo niandae chakula, na sehemu ya kulala mgeni. Muda mfupi tu ulipita kuna mwanamke aliingia na kuniambia nimuachie nafasi kwa sababu hiyo ni nyumba yake sasa au anichome kisu," aliema Lilian.

Alieleza kuwa: "Mwanamke huyu alikuja akilia na kulalamika kuwa mke wangu amemchukua mume wake na nyumba yake, nilimwambia kwamba kama mke wangu ndio amekufukuza kwako basi nenda ukachukue mizigo yako na watoto na uje ukae na mimi hapa," alisema Bwire ambaye alikuwa mume wa Millecent.

Ni wiki mbili sasa Lilian Weta alipoolewa na Christopher Bwire baada ya wapenzi wao kuwasaliti na wanadai kuwa hawajutii kitendo walichokifanya.

Bwire aliwaeleza waandishi wa habari namna maisha yake yalivyobadilika na kuwa ya furaha.

"Wabaya wawili wapatane na wawili wazuri wapatane, sina msongo wa mawazo. Siku hizi ninaamka muda ninaotaka na kulala muda ninaotaka, ninakula vizuri, nina furaha sana kuwa na Lilian," alisema Bwire.

Na upande wake Lilian pia anadai kuwa ana furaha sana kukaa na Bwire.

Barasa ambaye ni mume wake Lilian zamani anasema kuwa hana haja ya kumfuata mke wake na hataki kujua chochote kuhusu yeye kwa sababu yeye na Auma wana furaha sana.

***BBC***

# Netanyahu, Gants nguvu sawa uchaguzi

**YERUSALEM, Israel**

WAISRAELI hawana uhakika na mustakabali wa kisiasa nchini mwao, siku mbili baada ya uchaguzi ambao kwa mara nyingine, vyama viwili vikuu vya siasa havikufanikiwa kuwa na mshindi wa moja kwa moja.

Asilimia 95 ya kura zilizohesabiwa chama cha Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu cha Likud kimepata viti 32 na kile cha mpinzani wake, Benny Gantz cha Bluu na Nyeupe kimepata viti 33. Bunge la Israel lina jumla ya viti 120.

Katika matokeo ya uchaguzi huo, Avigdor Lieberman wa chama cha Yisrael Beiteinu, anabakia kuwa katikati ya wagomea hao wawili wakuu, akisisitiza kuundwa kwa serikali ya muungano huku akisema hawezi kushiriki kwenye serikali itakayoongozwa na Netanyahu.

Kutokana na hali hiyo, Rais wa Israel, Reuven Rivlin, atalazimika kushauriana na vyama vyote kabla ya kumchagua mgombea anayeamini kuwa ni bora kupewa nafasi ya kuunda serikali ya mseto thabiti.

Waziri Mkuu wa Israel, Netanyahu, ametoa wito kwa mpinzani wake mkuu, Jenerali wa zamani, Gantz, kuungana naye katika kuunda serikali ya mseto.

Msemaji wa Gantz, alisema hawatatoa majibu ya haraka kutokana na wito huo wa kushangaza wa Netanyahu. Gantz anatarajiwa kutoa tamko muda wowote.

Mabadiliko hayo ya mkakati yanaonyesha kwamba Netanyahu hana namna hasa baada ya kushindwa tena katika uchaguzi huo ambao umefanyika baada ya kura ambayo haikumpa nguvu kubwa iliyofanyika Aprili, mwaka huu ambapo chama chake hakikupata wabunge wengi.

Netanyahu aliwahutubia wabunge wa chama chake juzi na kusema kuwa amekutana na viongozi wa vyama vya mrengo wa kulia na wameahidi kushirikiana naye kuunda serikali chini ya uongozi wake.

Hakueleza namna walivyokusudia kushughulikia suala la kutokuwa na wingi wa wawakilishi bungeni.

Gantz alisema anatarajia kuundwa kwa serikali ya umoja nzuri na kwamba hataki kuunda serikali hiyo kwa kushirikiana na chama cha Likud kinachoongozwa na Netanyahu, kwa sababu ya mashtaka ya rushwa yanayomkabili waziri mkuu huyo.

Hata hivyo Netanyahu amekanusha kuhusika na makosa yoyote.

Kwa upande wake Netanyahu alisisitiza kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi, alipendekeza juu ya kuundwa serikali kati ya chama chake na chama cha mpinzani wake Gantz kwa sababu taifa linawategemea kuonyesha mfano bora wa uwajibikaji na kwamba wanaweza kushirikiana. ***DW***



Kiongozi wa Chama cha Bluu na Nyeupe nchini Israel, Benny Gantz, akiwahutubia wafuasi wake. **PICHA: REUTERS**

## Maswali lukuki kiongozi waasi kuuawa

**KINSHASA, Congo**

KATIKATI ya wiki hii Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (FARDC) lilitangaza kwamba lilimuua kiongozi mkuu wa kundi la waasi wa Kihutu wa Rwanda (FDLR), Sylvestre Mudacumura.

Maswali mengi yameibuka siku moja tu baada ya kuuawa kwa kiongozi huyo.

Advertisemen

Wengi wanajiuliza nani aliyemuua kiongozi huyo mkuu wa kivita wa kundi la waasi la FDLR? Kwa mujibu wa msemaji wa jeshi la DRC, Jenerali Léon-Richard Kasongo, Jeshi la DRC (FARDC) ndilo limefaulu kumwangamiza kiongozi huyo wa FDLR na ni ushindi kwao.

Lakini mashirika ya kiraia na wakazi wa Mkoa wa Kivu Kaskazini wanahakikisha kuwa wanamgambo wa kundi linaloongozwa na Jenerali Guidon, ambaye anakabiliwa na kibali cha kukamatwa na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), walishiriki katika operesheni ya kuwasaka wapiganaji wa FDLR.

Hata hivyo, serikali ya Kinshasa imekanusha madai hayo na kubaini kwamba askari wake pekee ndio walioshiriki katika operesheni ya kumwangamiza kiongozi huyo mkuu wa FDLR.

Fred Bauma kutoka Taasisi ya kutathmini kuhusu DRC alisema: "Kwa hatua hii, bado ni mapema kusema ni nani hasa aliyefanya operesheni hii, je! ni FARDC ndio waliendesha operesheni hii? Je, waliiendesha peke yao? Na ni makundi gani au vikosi gani vingine ambavyo vilishiriki katika operesheni hii?"

Swali lingine linahusu mazingira halisi ya kuuawa kwa Sylvestre Mudacumura, msemaji wa Jeshi la DRC alibaini kwamba Mudacumura na maofisa wake waliingiliwa ghafla katika maficho yao kabla ya kuuawa kabisa, hata hivyo hakutoa maelezo zaidi.

Mtafiti kuhusu DRC kwa niaba ya Shirika la Kimataifa la Haki za Binadamu la Amnesty International, Jean-Robert Senga, alisema ni muhimu kwa jeshi la FARDC kueleza mazingira ya kifo cha Mudacumura.

Alisema ushahidi waliokuwa nao ni kwamba kiongozi huyo wa FDLR aliuawa kikatili.

"Angelipaswa kukamatwa na kukabidhiwa ICC ili haki iweze kutendeka," alisema Senga.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema kifo cha Mudacumura kitakuwa na athari kwa kundi lake, ambalo tayari limedhoofika.

Uwezo wa kundi la FDLR umepunguzwa kwa miaka kadhaa sasa, ameongeza Fred Bauma.

***RFI***

HABARI KITAIFA

# Waziri apigania ajira wahitimu Veta

Na Dege Masoli, TANGA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amewataka waajiri binafsi, mashirika na taasisi kuwatumia vijana wenye vyeti vya ujuzi kutoka vyuo vya ufundi stadi (Veta), ili watumike kujenga uchumi.

Mhagama alitoa agizo hilo jana, wakati akifunga mafunzo na kutoa vyeti kwa watihimu 468 wa fani mbalimbali kupitia mpango wa utambuzi na urasimishaji wa ujuzi wa mfumo rasmi wa mafunzo yaliyofanyika Tangamano jijini hapa.

Alisema lengo la serikali ni kuwawezesha vijana wenye ujuzi usio rasmi kutambulika na kuingizwa kwenye mfumo rasmi ili kunufaika na utaalamu wao na kwamba waajiri binafsi, mashirika na kampuni kuwatumia ni kufanikisha mpango huo.

Kabla, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Veta, Stella Ndimubenya, alisema mpango huo katika awamu ya kwanza, unalenga kuwafikia vijana 1,443 wenye ujuzi mbalimbali ambao hawamo katika mfumo rasmi hadi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Ndimubenya alisema mpango huo hadi sasa umeshawafikia vijana wa mikoa ya Mtwara, Lindi, Morogoro na Dar es Salaam ambao walisajiliwa mwaka 2001 na 443 ndiyo walioingia kwenye utaratibu huo wa urasimishwaji.

Hata hivyo, alisema awamu ya Agosti 5, mwaka huu, imeweka lengo la kuwafikia vijana 1,443 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu ikiwa ni kusudio la vijana 20,443 wa mikoa yote ya Tanzania Bara.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, alimhakikishia Waziri kuwa vijana wote waliopitiwa na mpango huo watatumika katika uzalishaji kwenye miradi mbalimbali ya serikali, ili kuingiza nguvu na michango yao katika uchumi wa nchi.

Shigela aliwataka vijana hao kutumia vyeti hivyo kama sehemu ya kubadilisha maisha yao kiuchumi na kujiendeleza kwa kusoma zaidi na kufikia madaraja ya juu kwa kuwa tayari wameshaingia kwenye utaratibu rasmi wa kutambulika kama ilivyo kwa mafundi wengine.



Meneja Mapato wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), Edgar Zawayo, akiondoa mabomba ya maji ya mamlaka hiyo yanayotumika kinyemela na wakulima wa mboga mboga kumwagilia katika Kata ya Bunju Mtaa wa Doyva. Dawasa baada ya kufika katika eneo hilo wakulima walikimbia. **PICHA: FRANK MONYO**

# Ushirika kuwezeshwa kuanzisha viwanda

Na Happy Severine, SIMIYU

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imesema iko tayari kuviwezesha vyama vikuu na vyama vya msingi (Amcos) vya pamba kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa vya kuchambua zao hilo na kuongeza mnyororo wa thamani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Japhet Justine, alisema hayo juzi kwenye kikao cha kujadili jinsi ya kuongeza thamani kwenye pamba kilichoandaliwa na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDP) na kukutanisha sekta mbalimbali za kifedha.

"Tunataka hivi vyama vya ushirika kuviwezesha ili kuwa na uwezo wa kuanzisha viwanda vikubwa na vidogo vya kuchambua pamba. Wawe na uwezo wa kuchambua, kupata pamba mbegu, kuzalisha mafuta na wataajiri watu wengi kupitia viwanda hivyo vidogo, lakini wakulima watanufaika moja kwa moja," alisema Justine.

"Leo hii mkulima anauza pamba Sh. 1,200 kwa kilo moja lakini anayechambua pamba anauza nyuzi, mbegu, mafuta na mashudu. Sasa hapo mkulima hanufaiki na zao lake badala yake anaendelea kunyonywa tu.

Tunataka hizi Amcos zikijengewa uwezo zianzishe hivi viwanda huko waliko wakulima vijijini, waongeze ajira lakini pia mkulima anufaike na pamba yake kwa uwapo wa kiwanda kijijini kwake ambacho kinachambua, kuzalisha mbegu, mafuta na mashudu," aliongeza.

Alisema benki hiyo imeona fursa hiyo na iko tayari kusaidia vyama hivyo ili viwe na viwanda vidogo na vikubwa kwenye maeneo ya vijijini kwa wakulima. Pia aliahidi kusaidia kujengwa kwa maghala makubwa ya kisasa ya kuhifadhi pamba iliyochambuliwa.

"Lakini ili kufanikisha haya yote lazima tuvijengee uwezo hivi vyama vya msingi na vyama vikuu viwe imara. Bila kuvibadilisha kuwa vyama vya kibiashara hatuwezi kufanikiwa hata kidogo. Lazima vibadilike viwe vyama vya kibiashara. Tunataka sasa kufanya hata hilo kuvibadilisha mtazamo na utendaji kazi wake, viwe vya kibiashara zaidi," alisema Justine.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa FSDP, Sosthenes Kewe, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili jinsi gani wanaweza kuongeza mnyororo wa thamani kwenye pamba na kumsaidia mkulima.

"Tumeona kuna haja ya kuwekeza katika zao hili kwa ajili ya kuongeza thamani kwenye mnyororo mzima. Ukiangalia mkulima anatumia nguvu kubwa kuzalisha au kulima lakini bado ameendelea kuwa maskini kutokana na kutokunufaika na mnyororo wa thamani," alisema Kewe.

Joshua Mirumbe, mmoja wa wadau wa pamba, alisema changamoto kubwa iliyopo ni upatikanaji wa soko la uhakika na kuwataka wataalamu wa masoko na fedha kukaa chini na kuja na majawabu ya tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema lazima wataalamu mbalimbali wabuni njia ambazo zitawezesha kilimo kiwe cha kisasa zaidi na teknolojia kutokana na kuwapo kwa mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia.

## Serikali yaipongeza NMB sapoti bil. 9.5/- za korosho

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imeipongeza Benki ya NMB kwa kuingia makubaliano ya ubia na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ambako NMB itatoa fedha za ununuzi wa zao la korosho kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu wa zao hilo wa 2019/2020.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati wa hafla ya kutangaza ushirikiano huo, ambako NMB imeidhinisha na kutoa Sh. bilioni 9.5 kwa wakulima wadogo 2,997 wa zao hilo katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, TADB imetoa dhamana ya asilimia 50 ya kiasi hicho, lengo likiwa ni kuwawezesha wakulima kumudu changamoto za manunuzi ya pembejeo za kilimo kwa ajili ya msimu mpya.

Naibu Waziri Bashe alisema kuwa, makubaliano hayo yamekuja wakati sahihi, kwani baadhi ya wakulima wa zao hilo katika mikoa hiyo hawajamaliziwa malipo ya korosho msimu uliopita, hivyo kuwapa wakati mgumu katika kumudu manunuzi ya pembejeo.

"Serikali haijamaliza malipo ya msimu uliopita, lakini iko mbioni kumaliza kabla ya msimu mpya, na ushirikiano huu sasa, unaenda kumaliza changamoto zinazowakabili. Shukrani pia kwa TADB kwa kutoa dhamana ya nusu ya kiasi ambacho NMB imetoa," alisema Bashe.

Aliongeza ya kwamba, ili kuwa na kilimo chenye tija kwa mtu mmoja mmoja na maendeleo ya taifa kwa ujumla, mkulima anapaswa kuwezeshwa katika upatikanaji wa pembejeo, unafuu wa gharama za uzalishaji na uhakika wa masoko, mambo yanayoenda kutekelezwa na makubaliano hayo.

Kaimu Mkurugenzi wa TADB, Filbert Mponzi, alisema sekta ya kilimo ni miongoni mwa vipaumbele vya benki yake, na kwamba hiyo ndio siri ya kutumia kiasi kikubwa hadi sasa katika uwekezaji wa Kilimo cha Mkakati na Kilimo Biashara.

"Baada ya NMB kuchaguliwa mwaka jana na TADB kuwa mshirika wa Mpango wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS), tumetoa jumla ya mikopo ya Sh. bilioni 14.3, fedha zilizotolewa kwa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) 32 zenye wanachama 14,310.

"Hao ni wakulima binafsi wanaojishughulisha na kilimo cha miwa, korosho na kahawa kutoka mikoa ya Pwani, Morogoro, Songwe, Arusha, Kilimanjaro, Lindi na Mtwara. Tunatambua kuwa wakulima wanahitaji mikopo ya kifedha, ili kununua pembejeo," alisema Mponzi.

Naye Mkurugenzi wa TADB, Japhet Justine, aliishukuru NMB kwa kujikita katika kukwamua sekta ya kilimo na kuongeza kuwa uwepo wa benki za biashara katika sekta ya kilimo, umetanua fursa ya uwezeshaji wakulima katika jitihada za kunyanyua pato lao na kukuza uchumi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH SEVERIN SINGUNDALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 262 AKA aina ya TOYOTA CARINA. Chassis namba AT1707043456 Engine namba 5A3799292.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi MBE/MBE/RB/290363/2019.

115425502

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**GODWIN EMANUEL MUSHI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Dyana T944 AUQ yenye Chassis namba BU1020105358 na Injini namba, 15B14514552

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

Polisi Taafifa : MS/TR/RB/1691/2019

115425702

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;180/2019

Ombi la VERONICA VICENT kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu VICENT LAUTELI MNG'ANDE

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/09/2019.

115425302

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;189/2019

Ombi la VICTORIA WILSON MAJANI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MELKZEDEK GERVAS NGONYANI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/09/2019.

115426302


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Tupigie**

**0767 223 311**

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# RONALDO

## ANAWEZA KUBADILISHA MATOKEO – SIMEONE

**MADRID, Hispania**

CRISTIANO Ronaldo alikosa nafasi nzuri ya kufunga bao dakika za majeruhi wakati Juventus ikitoka sare na Atletico Madrid kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Diego Simeone amebainisha kuwa Mreno huyo anaweza kuamua matokeo katika mchezo wowote wakati wowote.

Atletico ilitoka nyuma na kusawazisha mabao mawili zikiwa zimesalia dakika 20 mpira kumalizika pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano, kwa mabao ya Stefan Savic na Hector Herrera.

Mchezo huo ulichukuliwa ni kama wa kulipa kisasi kwa kikosi hicho cha Simeone ambacho kilitolewa na Juve kwenye michuano hiyo msimu uliopita, licha ya kupata ushindi wa mabao 2-0 kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16.

Mabao matatu 'hat-trick' ya Ronaldo kwenye mchezo wa marudiano yakaiondoa Atletico kwenye michuano hiyo, lakini mchezo wa juzi Jumatano ulikuwa mgumu kwa timu zote mbili.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid amefunga mabao 25 dhidi ya Atletico, huku Simeone akishukuru nafasi aliyokosa kumtungua Jan Oblak.

"Nilishahesabu ni goli," alisema Simeone akiiambia Movistar.

"Tunamjua ni aina gani ya mchezaji, kwamba anaweza kuamua matokeo kwa shuti lake wakati wowote."

Mabao ya Juan Cuadrado na Blaise Matuidi yaliwaweka mbele mabingwa hao wa Serie A.

Savic akaanza kusawazisha kwa shuti la adhabu ndogo kabla ya kona ya Kieran Trippier ya dakika 90 kumkuta Herrera aliyetokea benchi na kufunga bao la kusawazisha kwa kichwa.

## SARRI ATAKA JUVENTUS KUIMARIKA ZAIDI

**MADRID, Hispania**

MAURIZIO Sarri amekubali kwamba Juventus inatakiwa kufanyia kazi safu yake ya ulinzi baada ya kuruhusu mabao mawili ya kusawazisha katika sare ya kufungana 2-2 dhidi ya Atletico Madrid kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.



Sarri ambaye huo ulikuwa mchezo wake wa kwanza kuwaongoza mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, alionekana kama angeondoka na pointi zote tatu za Kundi D baada ya mabao ya Juan Cuadrado na lile la kichwa lililofungwa na Blaise Matuidi.

"Nafikiri tulicheza vizuri, lakini hatukuwa kwenye radha nzuri ya kimchezo na sababu tuliona kuwa mchezo ulikuwa mkononi mwetu," alisema Sarri.

"Tulihitaji kuwa mchezoni kwa asilimia zote, lakini kuna wakati tulionekana kutokuwa kwenye wakati mzuri.

"Niliamua kumwanzisha Cuadrado kwa sababu niliona kwamba ungekuwa mchezo wa wazi na wenye kasi na hivyo yeye angeweza kuhimili." Lakini safu ya ulinzi haikuwa kwenye ubora, kwani mwishoni niliona mambo yamebadilika tofauti na tunavyokuwa kwenye mazoezi."

Naye beki wa Juventus, Leonardo Bonucci alikubaliana na mtazamo wa Sarri kwa kusema kwamba safu ya ulinzi haikuwa kwenye ubora.

"Tulicheza mchezo mzuri, lakini hatukuwa makini, kwani tulitakiwa kucheza kwa umakini mkubwa zaidi hasa safu ya ulinzi," alisema.

## KANE ASIKITISHWA NA SARE YA OLYMPIACOS

**LONDON, England**

HARRY Kane amesema kuwa, Tottenham wanatakiwa "kuwa bora zaidi" kwani licha ya kuongoza kwa mabao mawili wakatoka sare na Olympiacos kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa, juzi Jumatano.



Ingawa Kane amebakiwa kuwa na imani kwamba, watafuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara nyingine tena.

Wakiwa wamefungwa kwenye fainali msimu uliopita, Spurs walianza kampeni yao ya Kundi B msimu huu 2019-20 kwa kupata pointi moja kwenye mchezo huo uliopigwa nchini Ugiriki.

Hata hivyo, mambo yalionekana kama yangekuwa mazuri zaidi kwa kikosi hicho cha kocha Mauricio Pochettino, wakati Kane alipofunga kwa penalti dakika ya 26 akifuatiwa na bao la Lucas Moura na kuwafanya kuongoza kwa 2-0.

Lakini bao la Daniel Podence katika dakika ya 44 likabadilisha mwelekeo na penalti ya Mathieu Valbuena ikawapa Olympiacos sare hiyo.

"Tulijiweka wenyewe kwenye nafasi nzuri, lakini bao kabla ya mapumziko lilituweka kwenye wakati mgumu. Sasa tunatakiwa kujiimarisha ili kuwa bora zaidi," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa England akiiambia BT Sport.

"Hatukucheza vizuri katika kipindi cha kwanza, lakini tulifunga mabao mawili, kitu ambacho hakikuwa kibaya."

## HABARI MICHEZO



# LEWANDOWSKI
## AIFUNGIA MABAO 200 BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

NYOTA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, amebainisha furaha yake baada ya kufunga bao la 200 katika mechi ya mashindano kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Lewandowski alifikisha idadi hiyo ya mabao wakati Bayern ikianza kwenye mchezo wake wa kwanza wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakishinda mabao 3-0 dhidi ya Red Star Belgrade mjini Munich, Jumatano.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye alifikisha mabao 199 kwenye mechi za mashindano kwa Bayern wakati wakitoka sare na wapinzani wao kwenye Bundesliga, RB Leipzig, wiki iliyopita, alifunga bao zikiwa zimesalia dakika 10 kumalizika dhidi ya Red Star.

"Mara zote mchezo tulikuwa tumeutawala na tulicheza vizuri, tulipata nafasi, tukatengeneza nafasi na tukazitumia vizuri," alisema Lewandowski akizungumzia mchezo huo wa Kundi B.

"Lakini hatukufunga mabao ya kutosha. Mara zote tulijaribu kwenda mbele. Wakati mwingine tulikuwa na maamuzi mabaya, lakini kuna vitu vichache. Mwishoni tukapiga mabao matatu, lakini yangeweza kuwa matano au sita.

"Unahitaji mchezo kama wa leo (juzi) kupata ushindi, kujiona wapi ulipokuwa bora na unavyoweza kufanya vizuri zaidi. Baada ya bao la pili mambo yalikuwa rahisi kwetu. Nina furaha kwa sababu nilifunga tena."

Lewandowski - ndiye mchezaji anayeongoza kutoka nje ya Ujerumani kuifungia mabao mengi zaidi Bayern - na anashika nafasi ya nne kwa kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo, nyuma ya Rainer Ohlhauser (215), Karl-Heinz Rummenigge (218) na Gerd Muller (564).

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland amekuwa na wakati wa kuvutia zaidi tangu alipotua hapo akitokea Borussia Dortmund mwaka 2014, akishinda mataji matano ya Bundesliga.

# Van Dijk: Liverpool tusipaniki kwa kipigo

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk amesisitiza kuwa hakuna sababu ya Liverpool kupaniki baada ya kupokea kichapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa Napoli, Jumanne wiki hii.

Ushindi wa Liverpool katika mechi sita mfululizo ulizimwa na kipigo cha mabao 2-0 kwenye mchezo wa Kundi E pale katika dimba la San Paolo, ambapo penalti ya Dries Mertens na bao la Fernando Llorente yalitosha kuwapa ushindi Napoli.

Ikiwa inaelekea kwenye mchezo wa Ligi Kuu England Jumapili dhidi ya Chelsea, Van Dijk amesema mabingwa hao wa Ulaya hawatakiwi kufikiria zaidi kipigo hicho.

"Sijui kama ilikuwa kutuamsha," amesema beki huyo akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

"Timu zote zilicheza vizuri na kutawala mchezo na ilifikiriwa kama ingekuwa sare. Bila shaka penalti ilibadilisha kila kitu na tukarudi nyumbani bila pointi, lakini sio jambo la kulifikiria zaidi.

"Tumekuwa tukicheza kwenye kiwango bora tangu kuanza kwa msimu huu, hivyo hakuna sababu ya kupaniki.

"Wengine kwenye mchezo ule walicheza vizuri, tuliwaweka kwenye presha kubwa na tulitengeneza nafasi na hatukuweza kuzitumia vizuri.

"Kuna mambo mengi mazuri ukiachana na matokeo yake. Tumejaribu kushinda mchezo na sasa akili yetu tunaielekeza kwa Chelsea."

# Zidane alia, Madrid kukosa morali

**PARIS, Ufaransa**

ZINEDINE Zidane ameishutumu Real Madrid kwa kukosa morali wakati wakifungwa mabao 3-0 na Paris Saint-Germain kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumatano.

Madrid walinyanyaswa pale Parc des Princes, wakati Angel Di Maria akifunga mara mbili na bao la dakika za mwisho la Thomas Meunier likawashuhudia miamba hao wa Ligue 1 wakipata ushindi mnono kwenye mchezo huo wa ufunguzi wa Kundi A.

Jitihada za Gareth Bale na Karim Benzema hazikuweza kuisaidia Madrid, ambayo ilichapwa na PSG iliyokuwa bila nyota wake, Neymar, Kylian Mbappe na Edinson Cavani.

Zidane, ambaye timu yake ilishindwa kupata hata shuti la maana la kulenga goli, hakuwa na furaha na morali ya Madrid pale jijini Paris.

"Wametunyamazisha kwa kila kitu, na kilichokikera zaidi ni kutokuwa na morali," alisema kocha huyo wa Madrid baada ya mchezo huo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Katika hatua hii, mashindano haya yanakuwa magumu kama unaingia uwanjani hujajiandaa vizuri. Walitunyamazisha."

Zidane aliongeza: "Walitengeneza nafasi nzuri. Kilichoniogopesha mimi ni kuona timu ikiwa bila morali yoyote.

"Tulijua kwamba, wapinzani wetu wangetupa presha kubwa. Tulionekana kama vile hatupo kabisa mchezoni. Tulikuwa na nafasi mbili tu na kutengeneza mabao mawili, lakini VAR iliyakataa."

Di Maria alianza kwa kuifungia PSG wakati mshambuliaji huyo alipomtungua golikipa wa Madrid, Thibaut Courtois kwenye kona ya kushoto dakika ya 14.

Hata hivyo, Zidane alikataa kumlaumu kipa wake kwa bao la pili la Di Maria alilolifunga kutoka umbali wa yadi 20, kabla ya Meunier kufunga la tatu dakika za majeruhi.

"Wote tupo kwenye boti moja. Tukishinda, tumeshinda wote. Na wakati tukifungwa, tunafungwa wote," alisema.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAJITOSA TENA KWA POGBA

Yaboresha maslahi yake ili kumshawishi akubali kubakia Old Trafford...

**MANCHESTER, England**

KWA mara nyingine, Manchester United imempa ofa mpya na nono kiungo wake, Paul Pogba, ili kumshawishi aendelee kubakia katika klabu hiyo ya Old Trafford.

Pogba aliweka wazi uamuzi wake wa kutaka kuondoka katika klabu hiyo kwenye kipindi cha majira ya joto mwaka huu kwa kueleza kwamba anataka kupata changamoto mpya, Real Madrid ikitajwa kumwinda mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Hata hivyo, Madrid haikuwasilisha ofa yoyote rasmi kwa ajili ya kumsajili Mfaransa huyo katika kipindi cha dirisha la usajili hadi lilipomalizika, na kuifanya United kujiandaa kumpa ofa mpya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26.

Pogba anatarajia kumaliza mkataba wake na klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu, lakini kuna kipengele kinachoipa nafasi United kumpa mkataba mpya wa mwaka mmoja.

Imeelezwa katika gazeti la jioni la Standard kuwa klabu hiyo maarufu kama Mashetani Wekundu hawako tayari kuona kiungo huyo waliyemsajili kwa dau lililoweka rekodi ya dunia anaondoka kama mchezaji huyo, kwa kujipanga kumpa ofa mpya ambayo imeboreshwa kwa lengo la kumshawishi kukubali.

Bado United inapambana na changamoto ya kumshawishi mchezaji huyo kubakia klabuni hapo, licha ya wakala wake, Mino Raiola pamoja na kaka yake, Mathias kumaliza utata kuhusu hatima ya Mfaransa huyo.

Mapema Jumanne wiki hii, kaka wa Pogba, alisema kuwa ni jambo lisilopingika na linalojulikana wazi kwamba Zinedine Zidane ndiye mtu anayeongoza kumhitaji kiungo huyo wa Manchester United.

Mathias, ambaye ni mchezaji wa klabu inayoshiriki Ligi Daraja la Nne Hispania, Manchego, alikiambia kituo cha Radio Marca kuwa: 'Zidane anataka wachezaji, hawezi kuwapata, lakini sina wasiwasi kuwa anatakiwa kuhakikisha anafanya kazi ambayo itaonekana ameirejesha timu kwenye hadhi yake ambayo anaihitaji.

"Ninavutiwa na Zidane na anavutiwa na kaka yangu, kila mmoja anajua hilo."

Mino Raiola alikiri kuhusu tetesi za uhamisho za mchezaji huyo zilizofanywa katika kipindi cha majira ya joto na kusema kuwa : "Kila mmoja anajua kuhusu mchakato wa uhamisho uliokuwa unamhusu Paul. Tuko katika mchakato wa kufanikisha hilo. Kila mmoja anajua mawazo ya Paul yaliko."

Mbali na Pogba, Manchester United pia iko katika mazungumzo na Kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard (26), na mshambuliaji chipukizi wa England (U-21), Mason Greenwood, ili wasaini mikataba mipya ya kubakia Old Trafford.

## KWA UFUPI

**ZIDANE AKALIA KUTI KAVU**

MASHABIKI wa Real Madrid wenye hasira wanataka kuona Zinedine Zidane anafukuzwa katika timu hiyo baada ya kufungwa na Paris St-Germain katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sun)***

**ALVES ALIKARIBIA JUVE**

JUVENTUS iliahirisha mchakato wa kumsajili Dani Alves (36) katika kipindi cha majira ya joto kabla ya beki huyo wa Timu ya Taifa ya Brazil kuamua kujiunga na klabu ya Sao Paulo kama mchezaji huru. ***(Calciomercato)***

**HAALAND ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United ilituma maofisa wake kwenda kumwangalia mshambuliaji raia wa Norway, Erling Haaland (19), ambaye ni mtoto wa straika wa zamani wa Manchester City, Alf-Inge Haaland. Nyota huyo alifunga hat-trick wakati Red Bull Salzburg ilipocheza dhidi ya KRC Genk kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Salzburger Nachrichten, via Sport Witness)***

**HOLTBY ATAJWA BLACKBURN**

BLACKBURN wameanza mazungumzo na kiungo wa zamani wa Tottenham na Fulham Mjerumani Lewis Holtby (29), ambaye kwa sasa ni mchezaji huru tangu alipoamua kuondoka Hamburg msimu uliopita. (Mail)

**EVERTON YAMWANIA PARKHOUSE**

MABOSI wa Everton wameonyesha nia ya kumsajili straika raia wa Ireland Kaskazini, David Parkhouse (19), ambaye kwa sasa anaitumikia kwa mkopo timu ya Derry City akitokea Sheffield United. (Football Insider)

**"BALE ANAELEWA KIHISPANIA"**

WINGA wa Real Madrid, Gareth Bale anazungumza kwa ufasaha lugha ya Kihispania, imeelezwa na Kocha wa zamani wa Wales, Chris Coleman. Bale amekuwa akidaiwa hajui kuzungumza lugha hiyo licha ya kujiunga na Real tangu mwaka 2013, mchezaji mwenzake kutoka Wales, John Toshack, ni mmoja wa watu wanaompa changamoto na kumshangaa kwa uamuzi huo. ***(Athletic, via Marca)***

**NEUER KUTANDIKA DALUGA**

GOLIKIPA wa Bayern Munich, Manuel Neuer (33), anatarajia kustaafu kuitumikia timu yake ya Taifa ya Ujerumani baada ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Ulaya hapo mwakani. ***(Bild - in German)***

**SANCHO: SIONDOKI DORTMUND**

WINGA wa Borussia Dortmund ambaye ni raia wa England, Jadon Sancho (19), anayetakiwa na Manchester United, ameweka wazi uamuzi wake wa kutoondoka katika klabu hiyo ya Ujerumani katika kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Viasport, via Metro)***

**SCHOLES AMPOTEZEA POGBA**

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Paul Scholes, amesema kuwa kama nyota Paul Pogba ataondoka katika klabu hiyo, basi "hataacha pengo kubwa" kwenye kikosi cha timu hiyo inayotumia Uwanja wa Old Trafford. ***(Talksport)***

**TUCHEL KUMRITHI SOLSKJAER**

MANCHESTER United imeanza kumfuatilia kocha Mjerumani Thomas Tuchel ambaye hatima yake katika kikosi cha Paris St-Germain haijafahamika kwa ajili ya kumrithi Ole Gunnar Solskjaer, endapo itataka kufanya mabadiliko. ***(Le10 Sport, via Sport Witness)***

**CHELSEA, ABRAHAM WATETA**

CHELSEA imeanza mazungumzo na mshambuliaji, Tammy Abraham pamoja na beki, Fikayo Tomori kwa ajili ya kuwapa mikataba mipya. The Blues inatarajia kuwapa wachezaji hao mikataba ya miaka mitano. ***(Guardian)***

**SZOBOSZLAI SOKONI**

ARSENAL imeanza mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Hungary ambaye ana umri wa miaka 18, Dominik Szoboszlai kutoka Red Bull Salzburg. ***(Football.London)***

HABARI MICHEZO

# MANULA AELEZA SIMBA SC ITAKAVYOTETEA UBINGWA

**Na Mwandishi Wetu**

KIPA chaguo la kwanza wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Aishi Manula, amesema kwamba anaamini kikosi chao kina nafasi kubwa ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya tatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Manula, alisema kuwa sababu inayofanya aamini Simba itafanya vema kwenye ligi hiyo, licha ya kutolewa mapema katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ni ubora wa kikosi walichonacho.

Manula alisema kuwa kila mchezaji aliyesajiliwa na Simba, ana uwezo wa kupambana na kuisaidia kupata matokeo mazuri kwenye mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo watacheza.

"Kiwango cha timu yetu hakikuwa duni, kwa namna mechi zetu mbili za mwanzo tulizocheza, tumecheza vizuri, nadhani tutaendelea kupambana katika mechi zote ili tutimize malengo yetu," alisema Manula.

Aliongeza kwamba wachezaji waliokuwa majeruhi wamerejea katika kikosi hicho, na wameendelea kuifanya timu hiyo kuonekana kuwa na mwanzo mzuri wa msimu.

Naye Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa kikosi chao kinaendelea vema na mazoezi kwa ajili ya kwenda kuwavaa Kagera Sugar.

Rweyemamu alisema kuwa kila siku, benchi la ufundi limekuwa likiboresha mapungufu waliyoyabaini kwenye mechi zilizopita, licha ya kupata ushindi na kubeba pointi zote sita.

"Kila siku mwalimu anafanya maboresho, anarekebisha na kuimarisha kikosi chake, mpira kila siku huja na vitu vipya na timu hujiandaa kulingana na aina ya mpinzani unayekutana naye, tunaamini tutakwenda Bukoba tukiwa tofauti na msimu uliopita," alisema meneja huyo.

Aliongeza kuwa muda wa mapumziko kupisha mechi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars) dhidi ya Sudan, umesaidia kuwaimarisha wachezaji wao wa kimataifa ambao walikwenda kutumikia nchi zao.

Simba ilianza msimu wa mwaka 2019/20 kwa kuifunga JKT Tanzania mabao 3-1 na mchezo wa pili iliwachapa Mtibwa Sugar magoli 2-1, mechi zote ikicheza kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.




Msanii wa kikundi cha Sanaa cha African Top, Amani Grem, akionyesha kazi zake alizotengeneza kwa kutumia shanga alipotembelea katika ofisi za Nipashe zilizopo Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Msanii huyo alisema kikundi chao kinatafuta wafadhili ili wajiendeleze na kufungua chuo kwa ajili ya kufundisha wasanii chipukizi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wadau wamlilia Jeba, azikwa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

RAIS wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, pamoja na wadau mbalimbali nchini wamesikitishwa na kifo cha kiungo wa Chuoni, inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, marehemu Ibrahim Rajab "Jeba".

Kiungo huyo wa zamani wa Simba, Azam FC na Mtibwa Sugar za Tanzania Bara, Jeba, alifariki juzi na jana mchana alizikwa katika makaburi yaliyoko kwenye kijiji cha Ndijani, Mkoa wa Kusini Wilaya ya Kati Unguja.

Marehemu Jeba alifariki akiwa kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja alikokuwa akipata matibabu kutokana na maradhi yaliyokuwa yanamsumbua.

Akizungumza na gazeti hili, Pandu, alisema kuwa ZFF inasikitika kupoteza mchezaji huyo ambaye alikuwa na kipaji kizuri na mchango wake bado ulikuwa unahitajika.

"ZFF tunapenda kutuma salamu za rambirambi kwa familia na uongozi wa timu ya Chuoni, kufuatia kifo cha mchezaji wake, Ibrahimu Jeba kilichotokea hapo jana (juzi)," alisema Pandu.

Taarifa iliyotolewa na Azam FC, ilisema kuwa klabu hiyo imepokea kwa masikitiko kifo cha mchezaji huyo na inaungana na Watanzania wengine katika kuomboleza msiba huo.

# Karume Boys matumaini kibao

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana chini ya umri wa miaka 20 (Karume Boys), imeondoka nchini jana na kuelekea Uganda kwa ajili ya kushiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ( U-20)ikiwa na matumaini ya kufanya vema kwenye michuano hiyo.

Mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), yanatarajiwa kuanza kesho kwenye vituo vya Jinja na Gulu, kwa kushirikisha timu 11 kutoka nchi wanachama wa baraza hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana kwenye hafla ya kukiaga kikosi hicho, Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa kwa Timu za Taifa za Zanzibar, Ayoub Mohammed, alisema kuwa wanaamini wawakilishi hao watakwenda kupeperusha vema bendera ya Visiwa hivyo, katika michuano hiyo kutokana na maandalizi waliyofanya.

Mohammed alisema kuwa katika sera ya michezo, serikali imejipanga kuhakikisha michezo inaendelea kukua pamoja na wachezaji husika wananufaika na vipaji vyao.

Alisema kuwa Wazanzibar wote wanapaswa kuhamasisha ili timu zote za Taifa ziweze kufanya vizuri katika mashindano wanayoshiriki na sio jukumu la kamati hiyo peke yake.

"Tunaamini timu hii itafanya vizuri katika michuano hiyo ya Cecafa huko Uganda, tunapaswa wote kuunga mkono juhudi za kocha pamoja na wachezaji waliochaguliwa katika kikosi hichi," alisema kiongozi huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Karume Boys, Nassor Salum, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kiko tayari kwenda kupambana katika michuano hiyo kwa sababu malengo yao ni kurejea na kikombe.

Salum alisema kuwa kikosi alichokichagua ni imara kutokana na ushindani walioonyesha wakati wote wa mazoezi na kilichobakia ni kuwaombea dua njema ili watimize malengo yao.

Karume Boys imepangwa katika Kundi B pamoja na "ndugu zao" Tanzania Bara, Ethiopia na Kenya.

## MAKOCHA KMKM, KVZ WATAMBIANA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa KVZ, Mohammed Seif, amesema kuwa kikosi chake kimejipanga vema kuhakikisha kinapata ushindi katika mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya "Mabaharia" wa KMKM utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan.

Seif aliliambia gazeti hili kuwa, kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na anaamini vijana wake watapambana kuhakikisha wanaondoka na pointi tatu na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunaidhibiti KMKM kwa dakika zote za mchezo ili isiharibu mipangilio yetu ya kupata alama tatu muhimu, ambayo kila timu inahitaji ushindi katika mechi za mwanzo wa msimu," alisema Seif.

Naye Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, aliliambia gazeti hili kuwa wamejiandaa kukutana na ushindani katika mchezo huo, lakini wao wanaamini wataibuka na ushindi ili waendelee kujiweka kwenye nafasi bora ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Msimu alisema kuwa katika mechi ya leo, watawakosa wachezaji wao wawili ambao ni beki, Haji Mwinyi anayetumikia adhabu ya kadi nyekundu na mshambuliaji, Adam Ibrahim, ambaye amefungiwa mechi mbili.

Michezo

Ijumaa Septemba 20, 2019

Nipashe



## United yajitosa tena kwa Pogba

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Angel Di Maria (katikati), akifunga bao katika mechi ya Kundi A Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid iliyochezwa kwenye Uwanja wa Parc des Princes jijini Paris, Ufaransa juzi usiku. Madrid ilichapwa mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# ZAHERA AISUKA TOFAUTI YANGA

Lengo ni kuhakikisha wanaimarika na kuimaliza Zesco nyumbani kwao...

**Na Somoe Ng'itu**

TUTAWASHANGAZA! Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema kuwa anaamini kikosi chake kitapata matokeo mazuri katika mechi ya marudiano ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco ya Zambia, kutokana na "dozi kali" ya mazoezi wanayoipata wachezaji wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema kuwa kila siku wachezaji wake wamekuwa wakiimarika na hiyo inatokana na programu za mazoezi wanazofanya.

Zahera alisema kuwa pia amewaandaa wachezaji wake kuongeza umakini katika mchezo huo, ambao timu itakayopata bado mapema, itakuwa imejiweka kwenye mazingira ya mazuri ya kusonga mbele.

Kocha huyo alisema kuwa kikosi chake sasa kimeimarika zaidi, tofauti na walivyokuwa katika mechi ya awali, baada ya baadhi ya nyota wake waliokosekana kurejea kikosini.

"Kuna mambo mbalimbali tunayafanyia kazi, tunajiandaa kuwa na kikosi bora na imara zaidi ya tulivyocheza mechi ya kwanza, tumejua nguvu yao na tumejua tulipokosea, kikubwa kwa upande wetu, tulishajiandaa kwenda kutafuta goli ugenini, hii ilishakaa kwenye mipango yetu, tukifanikisha, tutakuwa tumefanikiwa," alisema Zahera.

**Aliongeza kuwa anafurahi kuona kila mchezaji ana morali ya hali ya juu kuelekea mchezo huo wa marudiano na maandalizi ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara watakazokuja kucheza baada ya kurejea nchini.**

"Timu yetu inabadilika, ninamaanisha wachezaji wanaimarika, kuna tofauti kubwa inaonekana kila siku tunapofanya mazoezi, matumaini yetu ni kuwapa furaha mashabiki wa Yanga na Watanzania wapenda mpira," aliongeza kocha huyo.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka nchini kuelekea Ndola, Zambia Jumatatu, lakini kikitanguliza ujumbe kwa ajili ya kukipokea kikosi chao.

Timu hizo zitashuka kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa Septemba 28, mwaka huu, zikiwa na kumbukumbu ya sare ya bao 1-1 waliyoipata Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Wakati huo huo, wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ni Azam FC, ambao nao wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwafuata Wazimbabwe Triangle United, huku wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 katika mchezo wa kwanza uliochezwa Septemba 15, mwaka huu hapa jijini.

## Samatta afunguka alitamani Ulaya mapema

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa KRC Genk inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji na nahodha wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, amesema kuwa ndoto zake za kucheza soka Ulaya zilichelewa kutimia.

Samatta mshambuliaji wa zamani wa African Lyon na Simba zote za jijini Dar es Salaam, aliliambia gazeti hili kuwa alitamani kuanza kucheza soka la kulipwa mapema zaidi, lakini pia anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hiyo.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alisema kuwa juhudi zake na hali ya kutokata tamaa, ni moja ya sababu zilizomsaidia kufikia mafanikio.

"Nilitamani kupata nafasi ya kucheza soka Ulaya nikiwa hata kabla ya kutimiza miaka 18, hata hivyo haturuhusiwi kukosoa mipango ya Mungu," alisema Samatta, mshambuliaji wa zamani wa mabingwa wa Afrika, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Samatta ambaye Septemba 4, mwaka huu, aliiongoza Stars kutinga hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia zitakazochezwa Qatar mwaka 2022 kwa kuitoa Burundi, mapema wiki hii alifanikiwa kuweka rekodi ya kuwa Mtanzania wa kwanza kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika mchezo huo, Samatta, aliweka rekodi nyingine ya kufunga bao, licha ya timu yake kupata kichapo cha mabao 6-2 kutoka kwa Red Bull Salzburg ya Austria.

Ili kuhakikisha idadi ya wachezaji wa hapa nchini wanapata fursa ya kucheza soka la kulipwa barani Ulaya, mapema wiki, Samatta alionekana katika picha za video, akimwongoza straika chipukizi, Kelvin John, kujifua wakati alipokuwa Ubelgiji kwa ajili ya kufanya majaribio na KRC Genk, ambayo ilimtumia mwaliko wa kwenda huko.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >